# Nipashe

Ijumaa Juni 28, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579956

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Wabunge watofautiana mabadiliko sheria NGO

UKURASA 2



Bandari Kigoma inavyopaa sambamba na uchumi wa majirani Burundi, DRC Ukurasa 19

UCHUMI

BUFE

Ijumaa Juni 28, 2019 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

MIKOPO ELIMU YA JUU

Uwekezaji una maana inapotolewa, kipindi cha malipo tafsiri 'inafifia' Ukurasa 14

Kamanda wa Kikosi dhidi ya Ujangili Kanda ya Kaskazini-Arusha, Peter Mbanjoko. Kwa nyuma ni pikipiki na baiskeli zilizokamatwa zikisafirisha nyara za serikali. PICHA: SALOME KITOMARI, ARUSHA

OPERESHENI UJANGILI

Ujangili wa tembo umeshuka, tabu yahamia mitaa mipakani Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UKURASA 13

# Waliopenyeza majina JKT sasa kikaangoni

**NI** wale walioshawishi ndugu zao waingizwe, wamo vigogo kadhaa, JWTZ yaapa kuwaanika... *Endelea ukurasa wa 2*



Msemaji wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Luteni Kanali Gaudentius Ilonda, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kurudiwa upya kwa uhakiki wa kuandikisha vijana kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Kulia ni Kapteni Petro Ng'umbi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Bunge lafuta adhabu Sheria ya Takwimu

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### 56% YA WANAOUGUA TB HAWAJAFIKA VITUONI

SERIKALI imesema kuwa hali ya ugonjwa wa kifua kikuu bado ni tishio kwa kuwa asilimia 56 ya wanaoishi na ugonjwa huo hawajafika kwenye vituo...

UKURASA WA 4

### DAKTARI BINGWA WA MOYO AFARIKI DUNIA

DAKTARI bingwa ambaye pia ni Mwenyekiti wa Hospitali ya Regency ya Upanga jijini Dar es Salaam, Dk. Rajni Kanabar (78), amefariki dunia...

## Biteko acharuka wizi wa madini

UKURASA 3

MICHEZO KMC YAANGUKIA KWA TP MAZEMBE KAGAME CUP UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Vigogo waliopenyeza majina ya ndugu jeshini kikaangoni

**Na Romana Mallya**

JESHI la Wananchi (JWTZ) limetangaza kuwachukulia hatua viongozi wa ndani na nje ya jeshi hilo na vijana waliohusika katika vitendo vya udanganyifu katika uandikishaji wa majina ya kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Udanganyifu huo ulihusisha ukiukaji wa taratibu na kughushi nyaraka na vyeti vilivyotumika katika uandikishaji huo.

Mkurugenzi wa Habari na Uhusiano JWTZ, Luteni Kanali Gaudentius Ilonda, akizungumza jana jijini Dar es Salaam kwa niaba ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi (CDF), Jenerali Venance Mabeyo, alisema licha ya taratibu za uombaji kuwa wazi, baadhi ya viongozi wamebainika kutumia nafasi walizonazo kupenyeza majina ya ndugu, jamaa na rafiki ili wasajiliwe.

"Napenda kuwataarifu kuwa baada ya kubaini kuwako kwa udanganyifu huu, JWTZ/ JKT tutafanya uhakiki wa vyeti na nyaraka zote husika kwa vijana walioandikishwa tutashirikiana na ofisi ya Nida (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa), Baraza la Taifa la Mitihani, Takukuru na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ili kuwabaini waliofanya udanganyifu," alisema Kanali Ilonda.

Ilonda bila kutaja uhakiki huo utafanyika lini na wakati gani, alisema utahusisha kuhakiki wa vyeti, nyaraka mbalimbali zilizokuwa zikihitajika kwenye uandikishaji huo pamoja na vyeti vya kuzaliwa na vipimo vya afya.

"Kwa kuweka usawa tutafanya uhakiki huu kwa kushirikiana na JKT, Nida, Wizara ya Elimu, taasisi zinazohusika na masuala ya rushwa, vyombo vya ulinzi na usalama, ili tuweze kuwachuja, tunataka kujiridhisha je, ni Watanzania kweli, wana afya njema, wana akili timamu, ametoka eneo husika na ana sifa stahiki, wale wenye sifa watachukuliwa, hata kama idadi yao itakuwa ndogo tofauti na matarajio yetu," alisema.

Ilonda alisema wale ambao watabainika kughushi watakamatwa na kufunguliwa mashtaka.

"Hakuna atakayesalimika labda wahame nchi, aliyeghushi vyeti na nyaraka mbalimbali kiwe cha kuzaliwa au daktari aliyetoa

INAENDELEA UK.26

# Wabunge watofautiana mabadiliko sheria NGO

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WABUNGE jana walitofautiana mtazamo kuhusu malalamiko ya wadau kutoka asasi za kiraia nchini Tanzania (Azaki) ambao wanapinga marekebisho ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO), huku idadi kubwa ya wabunge ikiunga mkono mabadiliko hayo.

Tofauti hizo za kimtazamo zilijitokeza wakati Mbunge wa Kigoma Mjini (ACT-Wazalendo), Zitto Kabwe, aliposimama kuchangia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Namba 3 wa Mwaka 2019.

Katika mchango wake, Zitto alisema muswada huo ni mbaya na unakwenda kunyonga watu.

"Tunaenda kutunga sheria ambazo zinaendelea kunyonga watu na huu ni mwendelezo wa juhudi ya serikali kukandamiza ila bahati mbaya wengi ni maskini. Tulizungumza hapa kuhusiana na takwimu hatukusikilizwa. Benki ya Dunia wamesikilizwa leo watu wale wale wanasimama wanasema ni serikali sikivu, hapana," alisema Zitto.

Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Salome Makamba, kwa upande wake, alisema anaheshimu mchango mkubwa ambao umefanywa na Kamati ya Katiba na Sheria kwa vile hadi siku ya Jumapili walikuwa wanajadili sheria hizo nane zilizomo katika muswada huo.

"Lakini Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Sheria na Katiba haizidi watu 25, haifiki hata robo ya wabunge

INATOKA UK. 26



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mratibu wa kujengea uwezo asasi za kijamii kutoka KNCV, Yunisi Moturi, kuhusu matokeo yaliyopatikana kwa watu waliotumia njia ya simu kujichunguza kama wanamaambukizi ya ugonjwa wa kifua kikuu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Bunge lafuta adhabu Sheria ya Takwimu

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limefuta kifungu cha 37(4) cha Sheria ya Takwimu kinachotoa adhabu kwa mtu anayetoa taarifa za takwimu bila kupata kibali cha Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Hatua hiyo inafuatia baada ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, kupendekeza bungeni, kufutwa kwa kifungu hicho.

Pia katika marekebisho ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO's), Sura ya 56, Prof. Kilangi amesema marekebisho ya kifungu cha 31 yanaweka masharti ya kuhakikisha kwamba mashirika yasiyo ya kiserikali yanafuata kanuni za fedha za uwazi na uwajibikaji.

Jana, wakati anawasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali, Namba 3 wa Mwaka 2019, Prof. Kilangi alisema, sehemu ya saba ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Takwimu, inapendekezwa pia kuanzisha Kamati ya Kitaalamu (Technical Committee) ambayo jukumu lake litakuwa kupokea na kujadili malalamiko yanayotokana na wadau kuhusu usahihi wa takwimu zilizotolewa kwa umma.

Mabadiliko ya sheria hizo pamoja nyingine sita ziliingizwa bungeni jijini hapa jana kwa hati ya dharura.

Katika kifungu hicho cha 37 (4) kabla ya kupendekezwa kufutwa katika marekebisho yaliyopelekwa bungeni na kisha kupitishwa, adhabu kwa makosa ya jinai katika Sheria ya Takwimu ilikuwa ni miezi sita jela au kulipa faini isiyopungua Sh. milioni mbili au vyote viwili.

Makosa kwa mtu yeyote kutoa taarifa zilizopatikana isivyo halali, adhabu yake ni kifungo kisichopungua miezi 12 au faini isiyopungua Sh. milioni tano au vyote viwili.

Kuhusu mabadiliko ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayopigiwa kelele na wadau wa maendeleo nchini pamoja na wabunge kwamba yanalenga kuua asasi hizo, Prof. Kilangi alisema marekebisho yanayofanywa yatasaidia kuleta uwazi na uwajibikaji kwa kuhakikisha miradi na shughuli zote wanazotekeleza zinakuwa na tija kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, mashirika hayo ni yale tu yanayolenga kunufaisha jamii na sio wanachama wake. Zimo asasi za kiraia nchini Tanzania maarufu kama Azaki.

Katika maelezo yake, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema: "Sehemu ya tano ya Muswada yenye ibara ya 24 hadi 32 inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56, marekebisho yanafanywa kwenye kifungu cha pili kwa lengo la kutoa tafsiri ya maneno ambayo yametumika katika sheria, lakini hayakuwa na tafsiri.

"Marekebisho ya kifungu cha nne yanalenga kupanua wigo wa majukumu na wajibu wa Mkurugenzi wa Uratibu wa Mashirika

INAENDELEA UK.26


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
27/06/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATATU tarehe 01/07/2019** kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TUNDUMA kuelekea DAR ES SALAAM,** gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 374 DLQ / T 741 BLF**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **21** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.0** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.6** |

3. Njia itakayotumika: **TUNDUMA hadi DAR ES SALAAM kupitia VIGWAZA,** Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215299202

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Madini, Doto Biteko (katikati), akikagua madini yaliokamatwa Juni 26 mwaka huu, mpakani Namanga, wakati yakisafirishwa kwenda Kenya kinyemela, yakiwa yamehifadhiwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), tawi la Arusha jana. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Biteko acharuka wizi wa madini

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ameagiza kuwafutia leseni wafanyabiashara wote wa madini wanaotumia leseni moja kufanya biashara hiyo kinyume cha utaratibu.

Pia, ameshangazwa na watu wachache wenye mtandao wa kuiba madini hayo na kutorosha nje ya nchi.

Aliyasema hayo jana jijini hapa, baada ya kusafiri alfajiri na kuwasili mkoani Arusha kwenda kujionea madini ya Tanzanite na mengineyo yakiwa yamekamatwa juzi (Juni 26) kwenye mpaka wa Namanga, yakiwa na thamani ya Sh. milioni 958.

Watuhumiwa hao wametajwa kuwa ni mmiliki wa madini hayo Latifa Abdalah (42), mkazi wa Sakina, dereva Josephat Joseph (41), mkazi wa Olasiti na kondakta wa basi hilo, Mohamed Mndeme (36).

Kufuatia kukamatwa kwa watuhumiwa hao, Waziri Biteko alitoa Sh. milioni tano kwa askari waliofanikisha kukamata madini hayo na Sh. milioni tano zingine kwa mtoa siri aliyefanikisha madini hayo kukamatwa kwa kuonyesha uzalendo kwa nchi yake.

Vile vile, alimwagiza Kamanda wa Polisi mkoa huo, Jonathan Shana, kumfikishia salamu Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini IGP Simon Sirro, ili polisi waliofanikisha kukamatwa kwa madini hayo wapandishwe vyeo kwa kuonyesha uzalendo wa kulinda rasilimali za nchi.

Alimpongeza pia Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, Jeshi la Polisi na wanahabari kwa kukesha katika msako wa madini hayo.

Waziri Biteko alitembelea eneo la Elerai, lililopo Majengo na kujionea madini ya aina mbalimbali yaliyohifadhiwa katika nyumba mbili tofauti bila ya kuwa na leseni au kibali cha kuyahifadhi na alipouliza zaidi aligundua leseni moja inayomilikiwa na Hawa Bakari &Company kutumiwa kufanya biashara ya madini ya aina mbalimbali na zaidi ya mtu mmoja.

"Ukoo mzima unafanyabiashara kwa kutumia leseni moja, ukiwauliza wanajibu kwa dharau, haiwezekani wanasema wamepokea miaka na miaka kufanya hivyo, sasa hii awamu nyingine kila mtu lazima afuate sheria," alisema.

Akieleza kuhusu madini yaliyokamatwa juzi, alisema yamehifadhiwa Benki Kuu (BoT), ndani ya sanduku maalum la kuhifadhi rasilimali za serikali za madini yakiwa katika vifurushi tofauti.

Pia aliamuru Ofisi ya Madini Kanda ya Kaskazini, kwenda kuchukua shehena ya madini yaliyorundikwa kwenye nyumba mbili za baadhi ya wafanyabiashara na kwenda kuyahifadhi sehemu husika kwa kufuata taratibu na sheria za madini hayo.

Alisema ameshangazwa na tukio hilo lililofanywa na watu wachache wenye mtandao wao huku wakijua wanachafua wafanyabiashara wengine wa madini ambao wanalipa kodi.

"Nimeshangaa sana kwa tukio hili haiwezekani unaiba madini kisha unapeleka nchi jirani ya Kenya, nasema hivi waliofanya

INAENDELEA UK.8

# 56% ya wanaougua TB hawajafika vituoni

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imesema kuwa hali ya ugonjwa wa kifua kikuu bado ni tishio kwa kuwa asilimia 56 ya wanaoishi na ugonjwa huo hawajafika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Vile vile, Tanzania inakadiriwa kuna wagonjwa 154,000 huku uwezo wa kuwaibua ni asilimia 44 na kwamba kifua kikuu sugu ni tatizo linalohitaji jitihada za wadau wote katika kuwaibua wagonjwa hao.

Kadhalika, mashine za teknolojia ya kisasa ya utambuzi wa kifua kikuu sugu zimesaidia kuongeza idadi ya wanaogundulika kwa kuwa miaka ya nyuma ilikuwa ni wastani wa wagonjwa 29 hadi 40, lakini mwaka jana pekee tumegundua zaidi ya 438," alifafanua.

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Dk. Leonard Subi, aliwaambia waandishi wa habari jana baada ya kufunguliwa kwa mkutano wa kumaliza mradi wa kupambana na kifua kikuu uliokuwa unatekelezwa na Shirika lisilo la kiserikali la KNCV, kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Marekani (USAID).

Alisema licha ya ugonjwa huo kuwapo miaka mingi hali ya kifua kikuu nchini ni tatizo kubwa na kwamba inahitaji ushirikiano mkubwa kati ya wananchi kuelewa dalili na kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Dk. Subi alisema serikali imenunua darubini 800, huku jitihada zikifanyika katika kuyafikia makundi maalum yaliyopo katika hatari ya kupata kifua kikuu kama wenye virusi vya Ukimwi, wanaoishi kwenye kambi, wanaofanya kazi za uvuvi na wachimbaji wa madini.

"Ugonjwa huu unatibika, na Tanzania inafanya vizuri kwenye matibabu licha ya kuwapo kwa mzigo mkubwa wa wagonjwa huo duniani. Katika vituo vya afya vipya 352 kuna majengo ya maabara yenye vifaa vya kisasa ikiwamo vya ugunduzi wa kifua kikuu," alisema.

Pia, alisema kifua kikuu sugu ni tatizo nchini na wameimarisha huduma na sasa zinapatikana katika vituo 81, ikiwamo kuimarishwa kwa teknolojia ya kupambana na ugonjwa huo kwa kushirikiana na wanajamii na makundi yaliyopo.

Naye, Naibu Mkurugenzi

INAENDELEA UK.8

# Bunge labaini tatizo uandaaji miswada

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imeitaka serikali kuendeleza utamaduni wa kushirikisha wadau wakati wa kuandaa miswada mbalimbali ya sheria ili kuliwezesha Bunge kutunga sheria zenye mawazo jumuishi.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Najma Murtaza Giga, alitoa rai hiyo alipowasilisha bungeni maoni ya kamati yake kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2019.

Alisema ushirikishwaji wa wadau utachagiza ustawi wa nchi na kupunguza changamoto zisizo za lazima wakati wa utekelezaji wa sheria hizo miongoni mwa wadau zanaowagusa.

Giga ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bunge, alisema: "Kwa kuwa kamati imebaini uwapo wa mchakato wa sera ya usimamizi na uratibu wa mashirika ya kiraia nchini ambao bado haujakamilika.

Na kwa kuwa uwapo wa sera hiyo utasaidia kuwa na sheria imara na jumuishi kwa manufaa ya wadau wote na taifa kwa ujumla, kamati inashauri serikali ikamilishe mchakato wa sera hiyo, ili ianze kutumika kwa lengo la usimamizi na uratibu bora wa masuala yote ya mashirika ya kiraia nchini.

"Kamati imebaini changamoto ya ushirikishwaji wa wadau katika michakato ya uandaaji wa miswada mbalimbali ya sheria hususani miswada ya dharura.

"Na kwa kuwa maoni ya wadau ni muhimu kwa hatua zote za mchakato wa kutunga sheria zenye tija katika sekta husika, ni vema washirikishwe kwa kuwa ni wadau hao ndiyo wanajua changamoto za sekta husika na namna bora ya kuondoa changamoto hizo."

Kuhusu marekebisho yaliyopendekezwa na serikali kwenye Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Sura 230, Giga alisema kamati imebaini maeneo muhimu yenye kuhitaji kuboreshwa ambayo ni pamoja na kukosekana kwa sera mahsusi kwenye tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza pamoja na sanaa ya ufundi ambayo imeajiri idadi kubwa ya Watanzania.

"Kamati inaishauri serikali ikamilishe mchakato wa sera hiyo ili kuwapo mfumo rasmi wa usimamizi na uratibu wa tasnia hiyo kwa manufaa ya wadau wote na taifa," alisema.

Giga aliongeza kuwa kamati yake pia imebaini marekebisho yaliyopendekezwa katika sheria hiyo pamoja na Sheria ya Haki Miliki, yanajibu sehemu tu ya changamoto nyingi zinazohusu ulinzi na usalama wa rasilimali za ubunifu pamoja na rasilimali za kiutalii nchini.

Alisema wasanii wamekuwa wakipoteza fedha nyingi kwa kudhulumiwa haki zao na kusababisha kuendelea kuwa masikini na serikali kupoteza mapato.

"Kamati inashauri mara baada ya kukamilisha mchakato wa sera husika, serikali iandae sheria shirikishi itakayotoa majibu ya changamoto zote kuhusu masuala ya sanaa za ufundi, filamu na michezo na haki miliki kwa lengo la kukuza uwekezaji wa ndani katika tasnia hizo kwa manufaa ya wasanii wa ndani na wawekezaji wa taifa," alisema.

## Raia wa Nigeria matatani

**Na Hellen Mwango**

RAIA wa Nigeria, Tope Omoshola na mumewe, wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka manane yakiwamo kuingia na kuishi nchini bila kibali.

Mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni Alli Fupi raia wa Tanzania.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega.

Mwendesha Mashtaka wa Idara ya Uhamiaji, Khadija Masoud alidai, Juni 15, mwaka huu katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam washtakiwa hao walikutwa wakiishi nchini.

Ilidaiwa, katika tarehe hiyo mshtakiwa Tope alikutwa ameingia nchini bila kibali na kutoa taarifa za uongo kwa maofisa Uhamiaji wa Mwanza na hivyo kujipatia hati ya kusafiria Ab 312910 ya Januari, mwaka huu.

Pia mshtakiwa huyo anadaiwa kuwa, katika tarehe hiyo Tope na Fupi, walitoa taarifa ya uongo na kusababisha Tope kupata hati ya kusafiria.

Katika shtaka jingine, Fupi anadaiwa kuwa, katika tarehe hiyo alisababisha Tope kupata hati ya kusafiria wakati akijua hana vigezo huku akidaiwa kudanganya kuwa yeye ni raia wa Tanzania wakati akijua si kweli.

Mshtakiwa Tope pia anadaiwa kudanganya maofisa Uhamiaji kwa kuwasilisha cheti cha kuzaliwa cha kughushi.

Fupi pia anakabiliwa na shtaka la kumhifadhi Tope nyumbani kwake na kumsaidia kupata hati ya kusafiria kinyume cha sheria.

Washtakiwa hao walikana kutenda makosa hayo na wàliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza sharti la kuwa na wadhamini wawili waliosaini bondi ya Sh. milioni mbili.

Upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kesi itatajwa Julai 30, mwaka huu.

# Wawekezaji wachangamkia fursa Dodoma

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAWEKEZAJI kutoka nje na ndani wamechangamkia fursa za uwekezaji Dodoma, huku wakitajiwa sekta muhimu zinazohitaji uwekezaji ili kuinua uchumi wa nchi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Kessy Maduka, katika kongamano la siku mbili la fursa za uwekezaji linalofanyika jijini hapa.

Maduka alisema Mkoa wa Dodoma ambao uko katikati ya nchi, kuna fursa mbalimbali za uwekezaji ambazo bado zinahitaji uwekezaji na zinaweza kuwaingizia fedha nyingi wawekezaji.

Katibu Tawala huyo alizitaja

INAENDELEA UK. 8



Mbunge wa Iringa Mjini, Mch. Peter Msigwa, akihutubia wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Stendi Kuu ya Mabasi mjini humo juzi. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Dk. Kanabar wa Regency afariki dunia

**Na Joseph Mwendapole**

DAKTARI bingwa ambaye pia ni Mwenyekiti wa Hospitali ya Regency ya Upanga jijini Dar es Salaam, Dk. Rajni Kanabar (78), amefariki dunia.

Kwa mujibu wa mtoto wake, Amish Kanabar, baba yake alifariki usiku wa kuamkia juzi huko Dallas Marekani, alikokuwa akiugua kwa muda mrefu.

"Kwa masikitiko makubwa familia inawatangazia kifo cha mpendwa wetu Dk. Rajni Kanabar, kilichotokea nchini Marekani amefariki dunia akiwa amezungukwa na familia yake, mke wake Sarla na watoto wake wawili."

"Tumwombee kwa Mungu apumzike salama, mazishi yamepengwa kufanyika Dallas Marekani Alhamisi (jana)," alisema Amish.

Mwaka 1979 Dk. Rajni Kanabar alianzisha mradi wa kupeleka wagonjwa wa moyo nchini India na kila mwaka zaidi ya watoto 100 walikuwa wakipelekwa kutibiwa bure.

Kupitia mradi huo uliofahamika kama 'Tanzania Heart Babies Project' wagonjwa wengi wao wakiwa na matatizo ya valvu kwenye moyo walikuwa wakipelekwa kwenye hospitali mbalimbali za nchi hiyo ikiwamo Narayana na Hayderabad.

Dk. Kanabar ambaye alikuwa mwendeshaji wa mradi huo kupitia Klabu ya Lions ya Dar es Salaam (Host), alikuwa mstari wa mbele kutafuta wafadhili wa kutoa fedha kwa ajili ya kupeleka watoto hao nje ya nchi.

Miongoni mwa wafadhili wakuu kwenye mradi huo ni aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Hayati Dk. Reginald Mengi ambaye kila mwaka alikuwa akitoa fedha za kupeleka wagonjwa zaidi ya 50 nchini India.

Dk. Kanabar alizaliwa Novemba 9, 1940 jijini Mwanza na baadaye alisomea udaktari nchini India na Dublin Ireland na kisha kurejea nchini na alishiriki kuanzishwa kwa Hospitali ya Regency.

Kwa zaidi ya miongo mitatu, Dk. Kanabar amepata tuzo mbalimbali kutokana na mchango wake wa kuhudumia jamii hususan kwenye sekta ya afya.

Mradi wa 'Tanzania Heart Babies Project', aliouanzisha mwaka 1979 umekuwa msaada mkubwa kwa maelfu ya watoto wa Tanzania ambao wamekuwa wakipelekwa India bure kwa matibabu hadi 2015 ilipojengwa Taasisi ya Jakaya Kikwete Heart Institute (JKCI).

Dk. Kanabar kwa miongo kadhaa amekuwa akishirikiana na hospitali za nje ya nchi kupeleka wagonjwa wa Tanzania kwa matibabu hata yasiyo ya moyo kwa gharama za chini.


Kutokana na mchango wake kwenye sekta ya afya, Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete na Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa waliwahi kumpa Dk. Kanabar tuzo ya umahiri kwenye sekta hiyo kwa nyakati tofauti.

Mwaka 2010, Dk. Kanabar pia aliwahi kupewa tuzo ya heshima ya juu ya Rais wa India, Pratibhal Patil iitwayo 'Pravasi Bhartiya Samman.


***Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-***

- ***Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=***
- ***Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=***
- ***Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima***
- ***Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku***

215227501



## HABARI KITAIFA



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Afya (Tamisemi), Josephat Kandege (wa pili kulia), akizindua ripoti ya taasisi isiyo ya kiserikali ya Vodacom Tanzania Foundation ya mchango wa maendeleo ya jamii kwa miaka mitatu iliyopita (2014-2017) pamoja na mkakati mpya wa miaka mitatu 2019-2021, unaolenga kuchochea elimu jumuishi, ukuaji wa sekta ya kilimo, kuboresha mazingiza na ujumuishwaji wa watu kwenye mifumo rasmi ya kifedha. Wa kwanza kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (Tcra), Dk. Jones Kilimbe, katikati ni Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom Tanzania, Hisham Hendi, wa kwanza kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa Vodacom Tanzania Rosalynn Mworia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vodacom yaikuna serikali kusapoti miradi ya jamii

**Na Moshi Lusonzo**

SERIKALI imeipongeza kampuni ya simu ya Vodacom kwa kutumia zaidi ya Sh. bilioni 11 katika miradi ya kijamii katika sekta ya elimu na afya.

Pongezi hizo zimetolewa na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Josephat Kandege, jijini Dar es Salaam wakati akizindua ripoti ya maendeleo ya jamii na mkakati mpya kuchochea uchumi.

Waziri Kandege amesema ripoti hiyo iliyopewa jina la 'Alama za upendo wa Vodacom' imeonyesha kuwa kampuni na taasisi binafsi kwa kushirikiana na serikali zina uwezo mkubwa wa kubadilisha jamii maskini nchini.

"Jambo hili ambalo limefanywa na mfuko wa Vodacom Tanzania Foundation lina uzito mkubwa katika ustawi wa jamii zetu maskini, kama serikali tunaunga mkono na kutaka kampuni zingine za mawasiliano kuiga," alisema Kandege.

Alisema katika utekelezaji wa miradi hiyo Watanzania milioni tatu wameguswa jambo ambalo limesaidia kukuza uchumi na ustawi wa watu hao.

"Kazi kubwa hii iliyofanywa ni lazima iendelezwe kwani tunafurahi kusikia wanawake na watoto wa kike wenye matatizo ya kiafya wamesaidiwa ikiwamo kupewa elimu ya uzazi na kujengea mazingira rafiki watoto wenye ulemavu," aliongeza kusema.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom, Hisham Hend, alisema katika mkakati mpya wa 2019-2021, jumla ya shilingi bilioni tatu zitatumika katika kusaidia jamii kufikia uchumi wa kati.

Alisema katika mpango huo utazingatia upatikanaji wa huduma za kifedha, ubora wa elimu na kuchochea mabadiliko katika sekta ya kilimo.

Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Rosalynn Mworia, alisisitiza kampuni nyingine kuunga mkono mkakati huo kwa kuwekeza katika miradi inayolenga kutatua changamoto mbalimbali za kijamii.

# Waonywa wizi wa taa za barabarani

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MKURUGENZI wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Mwailwa Pangani, amewataka wananchi wa manispaa hiyo kuacha tabia ya wizi wa nyaya za taa za barabara ya Lumumba kutoka Kigoma Mjini-Ujiji, na kuonya kuwa watakaobainika watachukuliwa hatua kali.

Pangani alitoa maelekezo hayo alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo jana.

Alisema nyaya za taa ilizoibiwa ni eneo la Bakwata hadi Shule ya Msingi Ujiji, eneo la Shule ya Msingi ya Wakongomani na eneo la Mwanga sokoni hadi kwa Bela.

Alisema wizi huo umesababisha wameshindwa kuwasha taa hizo na kufanya wananchi wakabwe na vibaka kutokana na giza hasa usiku.

Mkurugenzi huyo aliwataka wananchi wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji wapende maendeleo, hivyo waachane na tabia ya kuharibu miundombinu kwa tamaa ya fedha kidogo.

"Kupitia kikao hiki nawataka wananchi wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji wawe ni walinzi wa taa za barabarani na si kuharibu miundombinu... tutakao wabaini tutawachukulia hatua kali pamoja na watu wanaowapelekea hizo nyaya za taa za barabarani kwa kuwauzia," alisema.

Mkurugenzi huyo aliyasema hayo baada ya Diwani wa Kigoma Mjini, Hussein Kalyango, kuuliza swali kuwa taa za barabarani zitawaka lini.

Mkurugenzi huyo alisema awali taa za barabarani zilikuwa zikiwashwa na mkandarasi wa kampuni ya Chotec General Supplies Co, lakini alishindwa na kukimbia kusipojulikana na kuacha deni la umeme wa Tanesco Sh. milioni 24.

Aliongeza kuwa baada ya mkandarasi huyo kukimbia, Manispaa ilifungua kesi mahakamani na kushinda, lakini mkandarasi huyo hajaonekana hadi sasa.

Alisema baada ya mkandarasi huyo kutoonekana Manispaa hiyo ililipa deni hilo laTanesco na kutoa Sh. milioni moja ili taa ziweze kuwaka, ndipo wakagundua kuwa taa haziwaki kwa sababu ya wezi wameiba nyaya za taa za barabarani.

# 'Amsha Ndoto' kuhamasisha uwekaji akiba

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Azania (ABL), imezindua kampeni inayofahamika kama, 'Amsha Ndoto' yenye lengo la kuwahamasisha wateja wake na Watanzania kwa ujumla kuwa na utamaduni wa kuweka akiba ili wawe na maisha imara kifedha baadaye.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari jana, kampeni hiyo itaendeshwa kwa miezi mitatu, kuanzia jana hadi Septemba 27, mwaka huu na itahusisha wateja wa zamani na wapya katika bidhaa mbili kuu za uwekaji akiba, ambazo ni: Ziada Akaunti(kwa ajili ya kila mmoja) na Watoto Akaunti (kwa ajili ya watoto tu).

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa ABL, Charles Itembe, ili kustahili kupokea zawadi, wateja wanapaswa kuwa na akiba yenye thamani ya Sh. milioni moja kwenye akaunti zao na kuendelea ili kuwawezesha kustahili kuingia kwenye fainali ya droo na hatimaye kushinda.

Alisema washindi watatu watapatikana kila mwezi, kupitia kampeni hiyo na wateja watawezakujishindia hadi mara mbili ya kiwango walichoweka kwenye akaunti na kiwango cha zawadi huweza kufikia Sh. milioni tatu.

Kuhusu vigezo vya washiriki, Itembe alisema kuwa wateja ni lazima waweke akiba ya Sh. 500,000 katika kipindi chote cha kampeni na mwaka mzima, na wale watakaoweka akiba kiasi cha Sh. milioni moja watapewa tokeni zitakazowawezesha kufuzu kwa ajili ya droo ya mwisho itakayowapata washindi.

"Tunawahamasisha Watanzania wote, wateja wetu wa sasa na wapya, wazazi na walezi kufungua akaunti hizi ili kuwa na uhakika wa maisha yao ya baadaye yaliyo salama. Kwa namna hii hawatahangaika kutafuta namna gani ya kuongeza mitaji, kulipia kodi za pango na kuwaandaa watoto wao kwa maisha ya baadaye," alisema Itembe.

Promosheni hiyo yenye kaulimbiu inayosema, 'Weka akiba ushinde, tumwezeshe ada ya shule', itawasilishwa kupitia radio na mitandao ya kijamii kama Facebook, Instagram, Twitter, LinkedIn, Google Display placement na tovuti za ndani.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuwadhibiti wapigadebe wa mabasi mikoani jambo jema

**MAENEO** mengi ya stendi za mabasi yaendayo mikoani na maeneo mengine yamekuwa yakisababisha usumbufu mkubwa kwa abiria.

Usumbufu huo umekuwa ukisababishwa na mawakala wa kampuni za mabasi na watu wengine ambao wanakaa vijiweni kufanya kazi ya upigadebe kwa ajili ya kujipatia kipato.

Mawakala na wapigadebe wamekuwa wakibughudhi abiria na watu wengine ambao ni wapita njia kwa njia mbalimbali zikiwamo kuwapigia kelele za kuwaita, kuwafuata nyuma, kupokea mizigo kwa nguvu ili kuipeleka katika ofisi za kampuni za mabasi husika na mambo mengine ambayo ni usumbufu na kero.

Kibaya zaidi ni kuwa kuna watu wanaojifanya mawakala wa kampuni hizo wanaosimama mitaani wakiwa na vitabu vya tiketi za mabasi, hivyo kuna baadhi ya abiria wanapewa risiti feki na matokeo yake kuwatapeli fedha zao.

Kuna matukio kadhaa ambapo baadhi ya abiria wanakatiwa tiketi zikionyesha namba za viti, lakini baadaye abiria hao hujikuta wakikosa viti kutokana na basi kujaa licha ya kuwa wanakuwa wameshalipia.

Stendi ya Ubungo jijini Dar es Salaam kwa mfano, imekuwa ni kero kwa abiria na wapita njia kutokana na vitendo vya bugudha kutika kwa mawakala na wapigadebe hao. Hali hiyo pia ni sugu katika stendi ya mabasi ya Nyegezi jijini Mwanza.

Kipindi cha mwisho Desemba hadi Januari hali huwa mbaya zaidi kutokana na vyombo vya usafiri husussan mabasi kutokidhi mahitaji. Mazingira hayo yasiyo rafiki ya utoaji wa huduma za usafiri yamekuwa yakitishia usalama wa wasafiri na mali zao, na ndiyo maana yamekuwa yakilalamikiwa.

Pamoja na kuputa muda mrefu bila hatua kuchukuliwa na mamlaka husika, lakini hatimaye zimesikika taarifa zinazotia moyo; kwamba hatua zimeanza kuchukuliwa kudhibiti hali hiyo. Serikali ilitangaza jana kuwa imeandaa mfumo rasmi wa kielektroniki katika ukataji tiketi za abiria wa mabasi yanayofanya safari zake mikoani utakaowaondoa rasmi wapigadebe na mawakala wa mabasi nchini.

Aidha, mfumo huo utaanza kutumika kwa majaribio katika njia itakayoainishwa na unataanza kutumika nchi nzima Septemba mwaka huu na baadaye kwenye mabasi ya mjini (daladala). Hayo yalibainishwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Kamwelwe alisema katika kuzishughulikia changamoto zilizopo katika sekta ya usafiri wa mabasi nchini, serikali kupitia Taasisi ya Udhibiti wa Usafiri Nchikavu (LATRA) na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Takwimu (NIDC) wameandaa mfumo huo ili kuzipatia majibu. Alisema mfumo huo umetengenezwa ili kuboresha utoaji wa huduma za usafiri kwa abiria na kuwaondolea kero ya ulanguzi wa nauli ambao unafanyika katika mazingira ambayo siyo rasmi kutokana na kukosekana kwa taarifa sahihi.

Alisema changamoto hizo huwaathiri watumiaji wa huduma hasa katika kipindi chenye mahitaji makubwa ya usafiri ambapo fedha nyingi za abiria huchukuliwa na mawakala au wapigadebe nje ya nauli halisi inayotakiwa. Pia, alisema kwa kuzingatia mahitaji ya wadau mbalimbali, mfumo huo itakuwa na taarifa zote muhimu zinazoweza kutumiwa na taasisi mbalimbali kama vile Latra, Polisi, Mamlaka ya Mapato (TRA), Uhamiaji, vyuo vya elimu ya juu na watafiti.

Tunaipongeza serikali kwa kuona changamoto hiyo na kuja na suluhisho, hivyo ni matumaini yetu kuwa wananchi sasa watapata huduma bora za usafiri bila usumbufu.

Tunatarajia mfumo huo utaandakiwa vizuri bila kusababisha usumbufu na mkanganyiko kwa wasafiri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Waathirika mnaotibiwa msirudie kula mihadarati

**MATUMIZI** ya dawa za kulevya yamekuwa yakipingwa kwa nguvu zote, kutokana na kwamba yana athari kubwa katika nyanja mbalimbali ikiwamo kiafya, kiuchumi na hata kijamii.

Ili kuhakikisha jamii inaepuka janga hilo, serikali kwa kushirikiana na wadau wa mapambano dhidi ya dawa hizo, imekuwa ikifanya kila njia, ambayo itasaidia kukomesha matumizi na biashara hiyo nchini.

Taarifa za serikali zinasema kwa sasa matumizi ya dawa hizo yamepungua kwa asilimia 90, na pia Tanzania ni ya kwanza katika nchi za Afrika za Kusini mwa Jangwa la Sahara kuanzisha vituo vya matibabu kwa waathirika wa dawa hizo.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ndiye anakaririwa na vyombo vya habari akisema hayo wakati akifungua mkutano wa 28 wa wakuu wa vyombo vinavyopambana na dawa za kulevya, kutoka nchi 54 za Afrika.

Mkutano huo ulifanyika Septemba mwaka jana, jijini Dar es Salaam, ambapo Waziri Mkuu alieleza kuwa matumizi ya dawa za kulevya nchini yameathiri sekta mbalimbali ikiwamo ya afya, uchumi na jamii. Anaongeza kwamba uchunguzi unabainisha kuwa kati ya asilimia 10 hadi 50 ya watumiaji wa dawa za kulevya wana maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), na kushauri nchi za Afrika kuweka mkakati imara wa kudhibiti dawa hizo.

Nikirejea kwenye hoja ni kwamba, jana ilikuwa ni Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Matumizi na Biashara ya Dawa za Kulevya, ambayo hufanyika kila mwaka Juni 26.

Maadhimisho ya mwaka huu yana kaulimbiu isemayo: "Waathirika wa dawa za kulevya wana haki ya kupata huduma ya afya", kwa maana kwamba kila mwathirika anaweza kwenda katika kituo cha matibabu na kupatiwa huduma.

Kimsingi ni kwamba serikali imefanya juhudi kubwa katika kukomesha matumizi na biashara ya kulevya nchini, kinachotakiwa sasa ni wauzaji wa dawa hizo kufanya biashara nyingine halali.

Kwa upande wa watumiaji, nao watambue kuwa dawa hizo ni hatari kwa afya zao hivyo wajitenge nazo ili kuepuka madhara mengine ya kiafya, ambayo wanaweza kuyapata yakiwamo ya ugonjwa wa akili.

Serikali imeanzisha vituo vya matibabu kwa waathirika wa dawa hizo, wahusika wavitumie inavyotakiwa badala ya kwenda kupewa huduma ya afya na kisha wanarudi mitaani na kuendelea kutumia dawa za kulevya.

Hivyo ni vyema wanaofanya hivyo watambue kuwa kwenda kupata huduma vituoni na kurudia matumizi ya dawa za kulevya ni sawa na kushindwa kutumia haki inayotajwa katika kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu.

Pamoja na juhudi za serikali na wadau wengine kuhakikisha biashara na matumizi ya dawa za kulevya vinakoma nchini, inasemekana baadhi ya watumiaji wabuni mbinu nyingine baada ya kuona wamebanwa.

Inaelezwa kuwa baada ya kuona wamebanwa, sasa baadhi ya watumiaji, hasa vijana wanatumia sumu ya kuua panya na kuitumia kama dawa ya kulevya kwa kuichanganya na dawa nyengine haramu za kulevya kama bhangi na kuvuta.

Hiyo inatokana na kwamba sumu ya panya inapatikana kirahisi katika maduka ya bidhaa za nyumbani na sokoni, na huuzwa kwa bei ndogo, hivyo watumiaji baada ya kubanwa wakaamua kugeukia huko.

Watumiaji na wale wanaojiandaa kujiingiza katika matumizi hayo watambue kuwa dawa za kulevya, ni janga linalotishia maisha ya vijana na kuathiri nguvukazi ya taifa ambayo ni vijana.

Walioathirika na dawa hizo wanajikuta wakipoteza dira ya maisha na taifa kukosa mchango wao unaouhitaji sana na wanakuwa watu wa kutegemea badala ya kujitegemea. Badala ya vijana kujikita katika shughuli za maendeleo na kukuza uchumi wao wameamua kujiingiza katika utumiaji na uuzaji wa dawa ya kulevya na mwisho wa siku wahusika pia wanajiingiza katika vitendo vya uhalifu.

Aidha, wakati huu wa maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Matumizi na Biashara ya Dawa za Kulevya Duniani, jamii na taasisi zisizo za kiserikali, kila upande ushiriki kikamilifu katika vita ya dawa za kulevya.

Watumiaji wa dawa za kulevya wapo mitaani, wanajulikana, wasaidiwe ili waunge mkono juhudi za serikali za kupambana na dawa hizo kwa kwenda vituo vya matibabu, na wauzaji watajwe wachukuliwe hatua za kisheria.

# HABARI PICHANI




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Waziri wa Uwekezaji, Angella Kairuki, Waziri wa Tamisemi, Suleiman Jafo (kushoto) na Mkuu wa mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Uwekezaji Mkoa wa Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akifafanuliwa jambo na Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, wakati akikagua mabanda, kwenye Kongamano la hilo. Kulia ni Mkuu wa mkoa huo, Dk. Binilith Mahenge. **PICHA: OWM**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiangalia mvinyo, katika banda la Benki ya Maendeleo (TIB), kwenye Kongamano hilo. Kutoka (kulia) ni Mkurugenzi wa Mipango na Mikakati wa TIB, Patric Mongela na Meneja Maendeleo ya Biashara, Joseph Chilambo. **PICHA: OWM**



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akioneshwa mkoba wa ngozi, uliobuniwa na wajasiriamali wa Kitanzania na Meneja Mzalishaji wa Fay Fashion, Gregory Mlay, kwenye Kongamano hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**




Mwekezaji wa kiwanda cha magodoro Dodoma, Asili, Haidar Gulamali (wa pili kulia), akimpa maelezo Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa (kushoto), alipotembelea banda la mwekezaji huyo, wakati wa Kongamano hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Baadhi ya wawekezaji wakifuatilia kwa makini Kongamano hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wawekezaji wachangamkia fursa

INATOKA UK. 4

fursa hizo kuwa ni viwanda, ardhi, hoteli, madini na utalii.

Alifafanua kuwa mpaka sasa kuna wawekezaji wengi ambao wameonyesha nia ya kuwekeza katika nyanja mbalimbali za viwanda, hoteli, nishati za umeme na gesi, hatua ambayo itasaidia katika kuinua uchumi.

"Mpaka sasa tumepokea maombi ya kampuni ya kuzalisha vinywaji ya TBL ambayo inahitaji heka 300 kwa ajili ya kujenga kiwanda kikubwa cha kutengeneza bia pamoja na vinywaji vingine kwa kutumia zao la mtama," alisema na kuongeza:

"Kwa hiyo kama kuna wakulima hapa wanaolima mtama nawataka waanze kuchangamkia fursa hiyo ili kitakapoanza uzalishaji waweze kupata sokola mazao yao," alisema Maduka.

Aliongeza kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limetuma maombi kwa ajili ya kujenga kituo cha kuhifadhi mafuta ya petroli na mgawanyo wa gesi jijini hapa.

Alitaja shirika jingine kuwa ni Sub Sahara Commercial limited ambalo linamilikiwa na raia wa China na Tanzania, ambao alisema wameomba eneo kwa ajili ya kujenga hoteli ya kifahari ya nyota tano karibu na uwanja mpya wa ndege unaojengwa jijini hapa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Uhamasishaji wa Uwekezaji wa Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), John Mnali, aliwataka wawekezaji wote wenye lengo la kuwekeza nchini wajue kuwa uwekezaji unaohitajika kwa sasa ni wa viwanda kwa kuwa serikali ya awamu ya tano inahamasisha nchi kuingia katika uchumi wa kati kupitia viwanda.

Alisema kwa lengo la kuwarahisishia kazi wawekezaji, serikali imeweka kituo cha pamoja kwa mamlaka zote zinazohusiana na wawekezaji kupata leseni na vibali vya kuwekeza nchini ili kuondoa usumbufu kwao.

Mnali alizitaja mamlaka hizo kuwa ni Brela, Uhamiaji, NEMC, Osha, TRA, TFDA na Wizara ya Ardhi ili mwekezaji apate huduma zote sehemu moja.

Aidha, alisema sifa kuu ya mwekezaji yeyote nchini awe wa ndani au nje ya nchi ni kutoa ajira kwa Watanzania ili kuwawezesha kujitegemea kiuchumi.



Kamishna wa Ustawi wa Jamii wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Naftali Ng'ondi (kushoto), akizungumza na viongozi wa dini wakati wa kikao cha kuwajengea uwezo kuhusu Ajenda ya Kitaifa ya Wajibu wa Wazazi /Walezi wa Malezi na Matunzo ya Familia, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WIZARA YA AFYA**

# 56% ya wanaougua TB hawajafika vituoni

INATOKA UK. 3

wa KNVC, William Mbawala, alisema mradi huo ulianza mwaka 2014, lengo likiwa ni kupambana na kutokomeza kifua kikuu kwa kushiriki mkakati wa kimataifa na Tanzania, na walihakikisha wanawafikia, kuwagundua na kuwaweka kwenye matibabu ili kupunguza uendelevu wa kusambaa.

"Katika nchi 30 duniani Tanzania ina kiwango kikubwa cha maambukizi ya kifua kikuu, huku Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) tunawafikia na kuwagundua wagonjwa kwa kiwango cha asilimia 44, huku asilimia 56 hawajafikiwa," alisema. Alisema kwa kushirikiana na jamii ikiwamo asasi sita nchini, asilimia 18 hadi 20 ya wagonjwa walipatikana kwa njia hiyo, na kwa kutumia teknolojia mbalimbali walifupisha muda wa uchunguzi wa mgonjwa hadi kupata majibu.

Kwa mujibu wa Mbawala kwa kipindi cha miaka mitano kitaifa kuna ongezeko la wagonjwa 13,000, ambalo limechangiwa kwa asilimia 53 na mradi huo kwa kuwa maeneo ya mradi yamechangia wagonjwa 7,000.

Alisema kifua kikuu sugu ni tatizo na matibabu yake ni ya muda mrefu ambayo ni ghali kwa serikali na mtu binafsi, na kwamba awali walisafirishwa kwenda Hospitali ya Kifua Kikuu Kibong'oto mkoani Kilimanjaro, lakini kwa sasa kuna vituo zaidi ya 100 vinavyowaanzishia dawa wagonjwa ambao zamani walisafirishwa hadi mkoani Kilimanjaro.

"Wengi wa wagonjwa wetu wanafikiwa na huduma za afya, wanapewa dawa na kurudi nyumbani, tumewajengea uwezo watumishi wa afya katika maeneo mengi nchini zaidi ya 2,000," alisema.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, mfumo wa takwimu wa kompyuta unawezesha watumishi kuingiza data na kupata ripoti kwa haraka na kwamba kwa Afrika inapatikana kwenye nchi mbili na umeunganishwa na mfumo wa kitaifa wa taarifa za afya," alisema.

Mbawala alisema kuna mashine 218 za teknolojia ya sasa za kutambua ugonjwa huo na jitihada zinafanyika kuhakikisha kila halmashauri inapata mashine moja, kwa ajili ya wagonjwa wa kifua kikuu sugu.

# Biteko acharuka wizi wa madini

INATOKA UK. 3

haya watachukuliwa hatua, halafu tunawahoji wanasema wanakibali, lakini ofisi ya kanda ya madini wala wizara hatuwafahamu," alisema.

Pia alisema katika tukio hilo, kuna watu waliohusika na kuagiza wachukuliwe hatua zinazostahili ili iwe fundisho.

Alisema, anashindwa kuelewa wachimbaji wanahitaji nini kwa sababu serikali imewafutia kodi halafu wamefungua soko la madini siku 12 zilizopita na soko hilo limeingizia serikali zaidi ya Sh. bilioni 2.5, lakini anashangazwa na baadhi ya wafanyabiashara kuharibu sifa ya soko hilo na kuanza kuyapeleka kwa njia za panya.

"Serikali kupitia rais wetu amefuta VAT na kodi zote zisizo rafiki, lakini bado watu hawajaridhika, wanatorosha madini sasa tutawafanya mfano kwa wenzao," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa Arusha, Mrisho Gambo, aliomba hatua kali za kisheria kuchukuliwa kwa wahusika wanaotorosha madini ili iwe fundisho kwa wafanyabiashara wajanja wa madini.

Alisema amesikitishwa na kitendo hicho licha ya serikali kuweka mazingira rafiki ya kufanya biashara hiyo, baadhi ya wafanyabiashara wachache wanakosa uzalendo na kuharibu.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji Tume ya Madini, Prof. Shukrani Manya, alisema Sharifa Mwalengwa Abdallah, aliyekutwa na shehena ya madini nyumbani kwake na kudai ana leseni ya Hawa Bakari &Company, hafahamiki.

Awali, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, akizungumzia tukio la kukamatwa kwa madini hayo, alisema yalikamatwa kwenye mpaka wa Namanga wilayani Longido yakiwa yamepakiwa katika gari aina ya Scania Perfect lenye namba za usajili T.716 AAC, mali ya Charles Shoo, mkazi wa Arusha.

Alisema gari hilo linafanya safari zake Jiji la Arusha hadi Nairobi nchini Kenya.

Alisema kiasi cha madini kilo 31.59 na Carats kilo 27.24, yenye thamani ya Dola za Kimarekani 416,577.58 sawa na Sh. milioni 958 yaliyofungwa katika vifuko 74.

Aliyataja madini hayo kuwa ni Tanzanite, Sapphire, Spinel, Ruby, Tourmaline, Tsavorite, Grossular na Aquamarine.

Pia msako mwingine ulifanyika majira ya saa 8:00 usiku eneo la Majengo, jijini Arusha nyumbani kwa mmoja wa watuhumiwa hao ambaye alitajwa na dereva wa basi hilo na kubaini mzigo mwingine tena ambao wanafuatilia uhalali wake.

Naye Gavana Mkazi wa Benki Kuu (BoT), tawi la Arusha, Charles Yamo, alisema, jana usiku saa tisa walikabidhiwa madini hayo kama ilivyo sheria na taratibu za nchi.

Alisema madini hayo yanapokabidhiwa BoT yanakuwa yamefungwa na kuwekwa ndani ya chombo maalum na kuwekwa sili maalum na uhifadhiwa hadi hapo serikali itakapoyachukua.

# DC aingia mitaani kukagua vitambulisho vya ujasiriamali

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MKUU wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Selemani Mzee, amefanya operesheni ya kushtukiza ya kuwasaka wajasiriamali wadogo ambao hawajachukua vitambulisho.

Aliongozana na watendaji wa kata na kamati ya ulinzi na usalama lengo likiwa kuendelea kuhamasisha wajasiriamli kuchukua vitambulisho hivyo baada ya kuonekana kuwa kuna kundi kubwa la wajasiriamali hawachukui vitambulisho hivyo.

Akizungumza jana na baadhi ya wajasiriamali wa wilaya hiyo, Mzee aliwataka wajasiriamali ambao hawajachukua vitambulisho hivyo kuvichukua mara moja na kulipia Sh. 20,000.

Alisema wapo waliotimiza wajibu wao wa kusikiliza agizo la serikali la kuwapunguzia gharama za kulipa ushuru kila mwezi au kila siku kwa kuchukua vitambulisho na kukaa mwaka mzima bila kusumbuliwa na kiongozi yeyote juu ya kulipa ushuru kwa kuwa wameshalipia kitambulisho hicho.

Mzee alisema kila mjasiriamali ambaye hana kitambulisho anatakiwa kuwa nacho ili aweze kufanya biashara zake katika mazingira rafiki ya kulipa ushuru wa kila mwezi au siku. Mzee alisema wameamua kuendesha operesheni hiyo ya kupita kila kata kwa ajili ya kukagua wajasiriamali ambao hawajachukua vitambulisho ili kuwapa elimu ya umuhimu wa vitambulisho hivyo.

"Tutaendelea kutoa elimu kwa wajasiriamali kuhusu umuhimu wa kupata vitambulisho ili kila mmoja aweze kuwa na kitambulisho, na kwa yule ambaye hana atajikuta akiwa katika mazingira magumu ya kufanya biashara yake," alisema Mzee.

Alisema vitambulisho bado vipo na wajasiriamali hao wasisite kuvichukua, na kuwa kila ofisi ya kata vinapatikana.

Bakari Juma, mjasiriamali wa mayai, alisema serikali ina dhamira nzuri kwa majsiriamali kwa kuwapatia vitambulisho hivyo, lakini baadhi yao wanashindwa kulipia kwa sababu ya ukosefu wa fedha.




Mkuu wa Kikosi cha Wanamaji cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Kepteni Yahaya Wangwe, akimweleza Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela (wa pili kulia) moja ya vifaa wanavyotumia kukabiliana na majanga baharini, wakati akikagua maonyesho ya mabanda siku ya Mabaharia Duniani inayoadhimishwa kitaifa jijini hapa. **PICHA:DEGE MASOLI**

# SUA yatenga mil. 300/- ujenzi wodi mpya

**Na Christina Haule,** MOROGORO

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kimetenga jumla ya Sh. milioni 300 kwa ajili ya kujenga wodi mpya kubwa katika hospitali ya chuo hicho mkoani hapa ili kutoa huduma za uzazi kwa kinamama chini.

Akizungumza kwenye ziara ya Baraza la chuo hicho kukagua miradi ya chuo iliyotekelezwa kwa kipindi cha miaka 3, Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Raphael Chibunda, alisema fedha hizo zimetengwa kutoka fedha kwenye bajeti ya mwaka fedha 2019/20, na kwamba ujenzi huo utaanza baada ya fedha kupatikana.

Prof. Chibunda alisema hospitali hiyo imeshapewa hadhi ya kuwa hospitali ya wilaya kutokana na kuwa na vifaa vingi vya kutolea huduma. Pia wameona ni vyema ikawa na wodi kubwa za kinamama zitakazosaidia mambo mengi ikiwamo kupunguza vifo visivyotarajiwa vya kinamama na watoto.

"Ni matarajio yetu, unapofika mwisho wa mwaka huu wa fedha hospitali yetu itakuwa na uwezo mkubwa sana wa kuwahudumia kinamama wa Tanzania vizuri juu ya suala la uzazi," alisema Prof. Chibunda.

Naye Daktari Kiongozi wa Hospitali ya SUA iliyopo Kata ya Mazimbu Manispaa ya Morogoro, Dk. Omari Kasuwi, alisema hospitali hiyo ina vitanda 67 vya kulaza wagonjwa, ingawa inakabiliwa na uchache wa watumishi.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la SUA, Prof. Esther Mwaikambo, aliki chuo hicho kwa kutekeleza miradi iliyokuwa kwenye mikakati yao kwa asilimia 80 hadi sasa wanapotimiza miaka 3 ya uongozi wao.

## Wasindikaji wadogo sasa waililia serikali

**Na Beatrice Moses**

WAJASIRIAMALI wasindikaji wadogo wa bidhaa Pwani na Dar es Salaam, wanajipanga kuiomba serikali kuwakumbuka na kuwawezesha kwa kutenga maeneo maalum yatakayotumiwa kwa usindikaji na masoko.

Baadhi ya wasindikaji hao walibainisha jinsi walivyokwama kurasimisha bidhaa zao ikiwamo kushindwa kuthibitisha viwango vya ubora katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kutokana na kushindwa kuwa na maeneo yanayohitajika kwa uzalishaji wa bidhaa wanazotengeneza.

Ester Mtamani akizungumza katika majadiliano kwenye warsha ya vijana wa sekta ya usafirishaji bodaboda na wajasiriamali wa usindikaji iliyoandaliwa na Youth Partnership Countrywide (YPC), alisema bidhaa za usindikaji zinapaswa kuandaliwa kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazosimamia usindikaji wa chakula za nchi.

"Kama msindikaji wa chakula nahakikisha usalama wa bidhaa ninachokitengeneza lakini wengi tunakwamba na kujenga maeneo yenye ukubwa unaopendekezwa, hivyo inakuwa kikwazo cha kukamilisha usajili wa bidhaa zetu," alisema.

Mtamani alisema serikali inaweza kuwasaidia kwa kujenga majengo maalum kwa ajili ya usindikaji kama ilivyofanya kwenye masoko ambapo msindikaji atapangisha, hivyo kulipa ada ya pango na kuendelea na shughuli zake za usindikaji katika mazingira yanayopendekezwa kwa usalama wa bidhaa.

"Pia kuna tatizo la vifungashio ukweli ni kwamba vingi tunavyovitumia havina ubora, unakuta chupa inabonyea, au mifuko mingine inayotumika kuwekea unga inahifadhi unyevuvyevu, hivyo kusababisha bidhaa kupoteza ladha pengine hata ubora unaotakiwa, serikali ivichunguze ijiridhishe na ubora wake," alisema.

Msindikaji mwingine, Rahma Kimambo alisema pia wana changamoto ya kukosa mwamko wa kuvuka kutoka kwenye usindikaji mdogo mdogo kuingia kwenye viwanda, hivyo wanahitaji mafunzo zaidi kama hayo waliyopata kutoka YPC ili kuwajengea uwezo wa kupiga hatua kuingia kwenye mafanikio.

Mwezeshaji katika warsha hiyo, Mchereli Machumbana, alisema kuhusu ajira na kazi zenye staha/tija Tanzania, serikali na wadau wanaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha upatikanaji wa ajira ili kutimiza mahitaji ya uchumi endelevu.

"Ili kutimiza hili, zipo fursa za tathmini ya mipango mbalimbali ngazi ya taifa, kikanda na kimataifa zinazolenga kukuza upatikanaji wa ajira na kuondoa umaskini," alisema. Machumbana alisema kuna changamoto kwa vijana katika kupata kazi na ajira zenye staha katika sekta ya usafirishaji na usindikaji ikiwamo kutokuwa na ujuzi wa kutosha kutokana na kukoswa elimu stahiki, kukosa taarifa sahihi kuhusu upatikanaji wa fursa mbalimbali mitaji, masoko na mafunzo.

"Changamoto nyingine ni kukoswa mitaji kuanzisha biashara, urasimu, elimu, ujuzi, taarifa, ushiriki mdogo kwenye masuala ya kitaifa hasa kwenye serikali za mitaa," alisema.

Ofisa Elimu kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi Tanzania (COTWUT), Elisa Luvigo, alisema kuna mahusiano duni kati ya waajiri na vijana.

## RC Kebwe aipa 5 Petrobena kusaidia vijana walima mpunga

**Na Mwandishi wetu,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kebwe Steven Kebwe, ameipongeza Kampuni ya Petrobena East Africa kwa kufadhili mradi wa kilimo cha mpunga wa eka 50 unaoendeshwa na kikundi cha vijana cha AgriAjira katika Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro.

Akizungumza na waandishi wa habari alipofanya ziara katika shamba la vijana, Dk. Kebwe alisema juhudi za kikundi hicho zitasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao na kutengeneza ajira nyingi kwa vijana.

"Naipongeza sana Kampuni ya Petrobena kwa kufadhili mradi huu kwa kuwapatia pembejeo za kilimo zikiwamo mbegu, mbolea na elimu bora ya kilimo mambo ambayo kwa pamoja yamewafanya kufikia hatua nzuri katika kilimo cha mpunga na kufikia hatua ya kuvuna mpunga safi," alisema.

Alisema mradi wa AgriAjira ni ushahidi tosha kwamba kuwekeza vizuri katika kilimo kutazaa ajira za uhakika kwa asilimia kubwa ya wananchi Tanzania na ambao ni vijana.

"Hatua iliyofikiwa katika shamba hili ni nzuri. Sisi kama serikali nitahakikisha viongozi wa wizara vinazohusika na kilimo, biashara na viwanda wanafika katika eneo hili ili wajionee mradi huu na kuwahakikisha soko la mpunga utakaovunwa," alisema.

Aidha, Dk. Kebwe aliwaomba wadau wa maendeleo kujitokeza kuunga mkono miradi mbalimbali inayoanzishwa na vijana hasa katika sekta ya kilimo ili kuwatengenezea ajira vijana kupitia miradi yenye tija kiuchumi na kijamii kwa maendeleo ya taifa.

"Serikali ya Awamu ya Tano imejielekeza kujenga uchumi wa kati na wa viwanda ambao msingi wake mkubwa unategemea sekta ya kilimo ambayo huzalisha malighafi ambazo zitachochea uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda na kupelekea uchumi wa nchi kukua," alisema Dk. Kebwe.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Petrobena East Africa, Peter Kumalilwa, alisema kampuni yake imejikita katika kushiriki kuendeleza sekta ya kilimo nchini kwa kusambaza mbolea za YARA na pia kutoa elimu na kanuni bora za kilimo ili kukuza uzalishaji mazao nchini.

"Tumefadhili mradi huu wa kilimo cha mpunga lengo tu likiwa ni kutengeza ajira kwa vijana na pia kukuza uzalishaji wa mazao ili azma ya serikali ya awamu ya tano kufikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025 ifikiwe," amesema Kumalilwa.

Mwakilishi wa AgriAjira, January Njavike, alimwomba Mkuu wa Mkoa kuwaunganisha na masoko ili mazao yao yapate soko.

# Kilo 2,432,989 za ufuta za wakulima zanunuliwa

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

CHAMA Kikuu Cha Ushirika wa Wakulima Masasi-Mtwara na Nanyumbu (MAMCU), kimekusanya na kuuza kilo za ufuta 2,432,989, na umeshauzwa na wakulima kulipwa.

Hayo yalisemwa wilayani Masasi na Meneja Mkuu wa MAMCU tawi la Masasi, Joseph Mmole, alipokuwa akizungumzia kuhusu minada mitatu ya ufuta ilivyofanyika tangu kuanza kwa ununuzi.

Alisema chama hicho hadi sasa kimeshakusanya kilo hizo kwa kuzinunua kwa wakulima kwa njia ya mfumo wa stakabadhi ghalani, na kwamba mfumo huu ni wa wazi na umeleta tija kwa wakulima.

Mmole alisema kiasi cha ufuta kilichokusanywa na kuuzwa kimekusanywa baada ya zao hilo kuuzwa kwenye minada mitatu ambayo imeshafanyika hadi sasa na minada hiyo imekuwa na tofauti ya bei iliyouzwa ufuta huo.

Mmole alisema katika mnada wa kwanza uliofanyika wilayani Masasi na mwingine wilayani Nanyumbu kwa siku tofauti, bei ya juu ilikuwa Sh. 2,970 na katika minada hiyo kwa upande wa Halmashauri ya Mji Masasi pekee ilikusanya na kuuza kilo 5,635, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi (213,886) na Wilaya ya Nanyumbu kilo 123,974 na kufanya jumla kuu ya mnada wa kwanza kwa Masasi na Nanyumbu kuwa kilo 343,495.

Alisema katika mnada wa pili jumla ya tani za ufuta zilizouzwa katika wilaya za Nanyumbu na Masasi ni kilo 564,466 na bei ya juu ya iliyouzwa katika minada hiyo ni Sh. 2,966

Mmole alisema mnada wa tatu wa sasa kabla ya kuelekea katika mnada wa nne jumla ya kilo za ufuta 1,525, ziliuzwa kwa bei ya juu ya Sh. 2,800.

"Ingawa kuhusu jumla ya fedha walizolipwa wakulima hawa kwa sasa sina kichwani, lakini wakulima wameshalipwa fedha zao na hadi sasa jumla ya minada mitatu imeshafanyika na tunasubiri mnada wa nne kiukweli hakuna tatizo lolote ambalo limejitokeza mpaka wakulima wamelipwa fedha zao,"alisema Mmole

Alieleza katika minada hiyo mitatu ambayo imefanyika hadi sasa, makasio ya jumla ya ukusanyaji wa zao la ufuta yalikuwa ni kilo 8,026 kwa wilaya za Nanyumbu na Masasi.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima, Yusuph Salumu, alisema hawana malalamiko kwa kuwa kila aliyeuza kupitia ghalani ufuta wake, umeshalipwa fedha zake.

Alisema wanaipongeza serikali kwa maamuzi yake ya ufuta nao kuuzwa kwa njia ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwa kuwa umeondoa mambo mengi ikiwamo mkulima kupunjwa malipo yake.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakichagua mikoba ya mitumba kando ya Barabara ya Morogoro, eneo la Manzese, jana. Wananchi wengi wa kipato cha kati na chini hupendelea matumizi ya bidhaa za mitumba kutokana na unafuu wa bei. **PICHA: JOHN BAD**

# Wanilia serikali kutatua ongezeko ankara za maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kuingilia kati ongezeko la bei ya huduma za maji zilizoongezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA) kutoka Sh. 1,100 kwa uniti moja hadi Sh. 1,688 kwa uniti moja.

Malalamiko hayo waliyabainisha jana kwenye mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Tellack, kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua. Walisema ongezeko hilo limesababisha kuwa na ongezeko la madai kwa wateja wa Kuwasa.

Walisema kuwa ongezeko hilo la bili kutoka Sh. 1,100 hadi Sh. 1,688 kwa uniti moja za maji limesababisha wateja wengi kusitisha huduma za maji kwa kuogopa kuingizwa kwenye orodha ya wadaiwa sugu.

Juma Ramadhani, mkazi wa Kata ya Majengo katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, alisema, mchakato wa kupandisha ankara za maji haukuwashirikisha watumiaji wa maji, jambo ambalo limekuwa likiendelea kuibua malalamiko juu ya ongezeko hilo na wengi kutishia kusitisha huduma.

Rose Masanja, alisema bei hiyo mpya imesababisha wateja wengi kusitishiwa huduma kutokana na kushindwa kulipa kwa wakati ukilinganisha na awali ambapo walikuwa na uwezo wa kumudu ankara hizo kwa wakati mwafaka.

"Hatupingi ongezeko la bei mpya za maji, ila tunaomba mamlaka iwe inashirikisha wateja wake endapo kutakuwa na mabadiliko ya bei ya maji badala ya kuitana wao na baadhi ya wadau ili tuwe na lugha moja wakati wa kupandisha ankara za maji," alisema Masanja.

Akijibu malalamiko hayo, Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Joel Lugemaira, alikili kuwapo kwa ongezeko hilo na kusema liliongezwa baada ya Wizara ya Maji kutangaza kila mamlaka za maji zijitegemee.

Alisema walikaa na EURA na wadau wa maji na kukubaliana kupitisha bei hizo ambapo kwa ndoo moja ya lita 20 itakuwa inauzwa kwa Sh. 33, na kuongeza kuwa ongezeko hilo hakutakuwa na tatizo la kushindwa kuendesha mradi huo.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Kuwasa, Bahati Matala, alisema ongezeko la bei hiyo itasaidia pia kusogeza huduma za maji katika kata na mitaa ambazo hazina maji, na kuwataka wananchi kuendelea kulipa bili hizo kwa wakati kuepuka kusitishiwa huduma hiyo.

HABARI ARUSHA

# RC aagiza umeme bandari kavu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amelitaka Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), kupeleka umeme eneo la Malula wilayani Arumeru, lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu, ili kuandaa mazingira mazuri ya uwekezaji.

Gambo alitoa agizo hilo jana jijini hapa katika mkutano wa Tanesco na wateja wakubwa wa umeme kutoka Kanda ya Kaskazini, ulioandaliwa kwa lengo la kuimarisha sekta ya nishati na ukuzaji wa viwanda nchini.

Alisema eneo hilo lililotengwa na serikali kwa ajili ya uwekezaji lina ukubwa wa zaidi ya ekari 4000.

Mkuu huyo wa mkoa alisema pamoja na kutenga eneo hilo, pia watu wa bandari wameshachukua eneo la ukubwa wa zaidi ya ekari zaidi 400 kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu.

"Sasa nilishaagiza watu wa idara ya maji kupeleka maji eneo hilo na nawaomba nyie pelekeni umeme eneo hilo la Malula ili kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji. Nakaribisha wawekezaji wengine kuja kuwekeza eneo hili kwa ujenzi wa viwanda kwani bado lipo kubwa na lipo jirani na barabara kuu ya Moshi - Arusha na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA)," alisema.

Gambo alisema serikali inajitahidi kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa kuhakikisha kunakuwa na umeme wa uhakika usiokatika na katika hilo wamefanikiwa.

"Siku za nyuma ulikuwa unakatika kila mara ila sasa hakuna tatizo, hivyo ni fursa kwa wawekezaji kuwekeza sababu kuna umeme wa uhakika," alisema.

Pia alipongeza wafanyabiashara wakubwa ambao wamekuwa mstari wa mbele kuchangia pato la taifa kwa kulipa malipo makubwa ya matumizi ya umeme na kodi zao.

"Kama kiwanda cha A to Z kwa mwezi wanalipa bili zao za zaidi ya Sh. milioni moja na kiwanda cha Rodhia kupitia viwanda vyake vidogo vyote vinachangia bili za zaidi ya Sh. milioni 500 kwa mwezi. Haya ni malipo makubwa sababu hata kodi yao ni kubwa hivyo wawekezaji ni watu wa kupongezwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda," alisema.

Pia alitoa wito kwa Tanesco kuhakikisha wanapeleka umeme kiwanda cha bidhaa za mifugo kilichojengwa mpakani Namanga ili kuwezesha kufanya kazi ifikapo Septemba au Oktoba, mwaka huu, kama walivyopanga kukizindua.

Alisema kufanikiwa kwa kiwanda hicho ni ukombozi kwa wafanyabiashara kuacha kupeleka mifugo nchini Kenya na kuondokana na usumbufu wanaoupata njiani wakati wakisafirisha mifugo yao.

Naye Meneja wa Tanesco Kanda ya Kaskazini, Mhandisi Stela Hiza, alisema wana kila sababu ya kujenga miundombinu mizuri ya umeme kwa kuwa mkoa wa Arusha una wateja wakubwa 335 kati ya wateja 150, 263 na wanachangia asilimia 41 ya mapato yote ya Tanesco Mkoa wa Arusha.

## TCRA yataka watoa huduma kufuata sheria

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imewataka watoa huduma wa mawasiliano nchini, kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi, wanapotekeleza majukumu yao.

Akizungumza jana Kaimu Mkuu wa TCRA, Kanda ya Kaskazini, Mhandisi Imelda Salum, alisema hayo jana katika mkutano uliowakutanisha wadau wa sekta ya mawasiliano kutoka mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

Alisema watoa huduma wanapaswa kutoa huduma ya mawasiliano kwa kuzingatia maudhui ya utekelezaji wa kazi zao kwa jamii.

"Mambo muhimu tuliyojadili na watoa huduma wetu ni kupata nafasi ya kuzijua sheria, kanuni, na taratibu zinazosimamia uendeshaji wa shughuli za mawasiliano," alisema Salum.

"Tumewasisitiza wadau kuwa na uelewa wa sheria mbalimbali zinazosimamia sekta ya mawasiliano sambamba na kuwaeleza mpango wa TCRA katika uboreshaji wa huduma na kutoa huduma hiyo katika viwango vya hali ya juu," aliongeza. Kwa mujibu wa mkuu huyo, lengo la mkutano huo ni kujadili mambo yanayohusu sekta hiyo hususani mafanikio na changamoto zinazowakabili watoa huduma.

Alisema katika mkutano huo walipata fursa ya kutambulisha mkataba wa huduma kwa mteja wa TCRA ambao ulizinduliwa rasmi Mei 8, mwaka huu. Ndani ya mkataba wa huduma kwa mteja, alisema kuna taarifa muhimu kwa wadau wa mawasiliano kuzifahamu.

"Fursa hii ilikuwa nzuri kujadiliana namna ya kuboresha sekta ya mawasiliano katika ukanda wa kaskazini na pongezi kwa wadau kujitokeza na kutoa mawazo na michango ya kwa lengo la kuboresha sekta hii," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wadau walioshiriki mkutano huo, Baraka Sunga aliomba mamlaka hiyo kujikita zaidi kudhibiti mawasiliano yasiyokuwa na maudhui kwa kutumia utaalamu wa sayansi na teknolojia kuliko kueleza nguvu kwenye utungaji wa sheria.

"Kaimu Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano napenda kuishauri ofisi yako kujikita zaidi kubuni njia za kudhibiti mawasiliano yote yasiyokuwa na maudhui kwa kutumia maendeleo ya sayansi na teknolojia kuliko kutunga sheria ambazo zimelenga kutoa adhabu tu pindi watu wanakapokosea kwani kwa kufanya hivyo tutaiendeleza na kuikuza sekta ya mawasiliano," alisema Baraka.



Kinamama wafanyabiashara ndogo kama walivyonaswa na kamera yetu wa soko la Kilombero lililopo ndani ya Jiji la Arusha wakiwa wanauza bidhaa zao huku wakisukana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Wadau utafiti haki za binadamu waalikwa

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), imezindua wiki ya maktaba na kuwataka wadau wa sheria kuitumia kwa kufanya utafiti kuhusu haki za binadamu na watu na kutoa ushauri kwa nchi mbalimbali kuhusu haki za binadamu.

Rais wa Mahakama hiyo, yenye makao yake makuu jijini hapa, Jaji Sylvain Oré, alisema hayo wakati wa ufunguzi wa wiki ya maktaba iliyofanyika juzi.

Alisema maktaba hiyo iliyoanza kazi mwaka 2009, hadi sasa ina vitabu 6,100 na inatarajiwa kukua zaidi kwa miaka michache ijayo.

Aidha, alisema maktaba hiyo imejiunga na hifadhi data mbalimbali katika nyanja ya haki za binadamu na masomo yanayohusiana nayo.

Jaji Oré alisema maktaba hiyo ni kielelezo cha raslimali kubwa inayosubiriwa kutumika na wadau mbalimbali kwa ajili ya kuongeza uelewa na elimu kuhusu haki za binadamu na watu.

"Tunawaalika wadau kutumia raslimali ili kuleta mafanikio katika kazi zenu na hususani kulinda na kukuza haki za binadamu," alisema.

Hata hivyo, aliiomba menejimenji ya mahakama hiyo, kuitunza maktaba hiyo, kuiongezea bajeti ya fedha kwa ajili ya kununua vitabu vipya na rasilimali zinginezo ili kuhakikisha kunakuwapo na mwendelezo katika kutoa habari za mahakama na jamii.

Alisema maktaba hiyo imejengwa kwa ushirikiano mkubwa uliopo kati ya mahakama hiyo na taasisi ya Umoja wa Ulaya, Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Chama cha Kimataifa cha Msalaba Mwekundu na Taasisi ya Raoul Wallenberg. Awali, Mkuu wa Maktaba hiyo, Fidelis Katonga, alisema mahakama hiyo ilianza kuadhimisha Wiki ya Maktaba Julai 23-27, 2018 na kwamba tangu wakati huo maadhimisho yao yamepangwa kufanyika kila mwaka kwa lengo la kuhakikisha wanawafikia na kuimarisha ushirikiano mkubwa na wadau wa haki za binadamu na watu.

Katika maadhimisho yanayoendelea wiki hii, baadhi ya shughuli zinazofanyika ni maonyesho ya raslimali za kisasa zilizopo katika maktaba hiyo, maonyesho na maelezo ya namna ya kutumia huduma na raslimali zingine zilizopo katika maktaba hiyo, maonyesho ya video kuhusu shughuli mbalimbali za mahakama na uzinduzi wa boresha ya maktaba.





# Kijiji kupata kituo cha afya cha kisasa

**Na Mary Mosha,** MWANGA

WANAKIJIJI cha Kigonigoni wilayani Mwanga Mkoa wa Kilimanjaro wataondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya baada ya serikali kuongeza huduma za kisasa na kuboresha kituo chao cha afya.

Serikali inawajengea wananchi hao maabara ya kisasa, jengo la upasuaji na wodi ya wazazi katika kituo cha afya cha Kigonigoni.

Hatua hiyo inawaondolea adha ya kutembea kilomita 50 kwenda Usangi ilipo hospitali ya wilaya ya Mwanga ili kupata matibabu.

Umbali huo ulikuwa unawaathiri zaidi kinamama wajawazito, watoto, wazee na wakati mwingine wagonjwa walipoteza maisha.

"Umbali huu ni mrefu sana na umekuwa ni changamoto kwa wananchi wa kipato cha chini hasa nyakati za usiku.

"Hii ni kutokana na kukosekana kwa usafiri pamoja miundombinu ambayo si rafiki," alisema Shaban Mrindoko mkazi wa Kigonigoni.

Wakizungumza wakati wa kuweka jiwe la msingi katika kituo hicho wakati wa ziara ya mbio za Mwenge wa Uhuru, wakazi wengine Fatuma Rashidi na Husen Mvungi, walisema ni mwanzo mzuri wa kupata huduma za afya kwa wakati na wakiomba serikali kuongeza huduma ya upasuaji.

Wakazi hao waliiomba pia serikali iwapatie madaktari pamoja na watumishi wa kutosha ili waweze kupata huduma za afya kwa wakati pindi majengo hayo yatakapokamilika.

Akizungumza katika ufunguzi huo, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa Mzee Ally Mkongea, aliwataka wananchi kutumia miundombinu na inayojengwa kwa umakini na kuitunza ipasavyo.

"Wananchi msifurahie miradi hii bila kuitunza, kumbukeni hizi ni fedha za serikali zinazotokana na kodi zenu wenyewe. Watendaji, serikali haitavumilia kuona mnaikwamisha hatua zitachukuliwa kwa yeyote atakayekaidi kusimamia matumizi mazuri ya fedha za serikali," alionya.

Mkongea pia ameuagiza uongozi wa wilaya ya Mwanga kukamilisha ujenzi wa mradi huo kwa wakati ili wananchi wasiendelee kupata adha ya kutafuta huduma za upasuaji katika hospitali ya wilaya huko Usangi.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wa Wilaya, Musa Njuki, alisema mradi unatarajiwa kutumia Sh. milioni 336 ambazo zimeshatumika huku ujenzi ukiendelea.

Alisema serikali kuu imeshaagiza vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi milioni 300, ili huduma zianze kutolewa mara majengo yatakapokamilika.



Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule (katikati) akitoa maelezo ya mradi wa maji uliofadhiliwa na Rotary Club ya Same kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa mwaka huu, Mzee Mkojea Ali, kabla ya kuweka jiwe la msingi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Umoja wa kidini waleta maridhiano

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KUKUTANA kwa viongozi hao mara kwa mara haimaanishi kuwa na umoja wa dini, bali una maanisha kuwa na ushirikiano utakao sababisha kuelewana, kuchukuliana, kuvumiliana imekuwa ikiwasaidia kubadili mitazamo yao juu ya wengine.

Hayo yalisemwa na Askofu Glorious Shoo wa umoja wa Makanisa ya Kipentekoste mkoani Kilimanjaro, amesema ushirikiano na umoja wa dini mbalimbali ndiyo nguzo ya kuvunja ukuta unaoleta utengano.

Kiongozi huyo alisema ushirikiano na umoja wa dini mbalimbali umevunja ukuta uliokuwapo miongoni mwa viongozi wa kidini ambao walioshindwa kushirikiana katika nyanja mbalimbali.

Alisema hayo katika kikao cha kamati za mahusiano ya dini mbali mbali (Interfaith committee) mkoani Kilimanjaro, iliyo chini ya usimamizi wa Norwegian Church Aid (NCA) kilichofanyika Moshi.

"Kabla ya Interfaith kulikuwa na ukuta mkubwa kati dini zote na hata dhehebu moja na jingine. Hata kukaa pamoja walikuwa wanaogopa.

Lakini baada ya kuundwa kwa kamati hii imejenga umoja wetu kutusaidia kujisafisha mitazamo yetu juu ya wengine," alisema Askofu Shoo.

Aliongeza "Mara nyingine tulikuwa tunakwenda kwenye mazishi ya watu wa dhehebu ama dini nyingine kwa tahadhari. Hatukuwa watu huru tulikuwa tunakwenda kwenye maeneo kwa tahadhari kubwa." Aliongeza Shoo.

Ukuta mwingine ulikuwapo kwenye mambo ya kijamii kwani waliogopa kufanya shughuli za kijamii lakini sasa hawana hofu tena, kwa mujibu wa maelezo.

"Tunaona tumepiga hatua, hofu na ukuta wa kuogopana vimepungua tunakutana viongozi wa dini mbalimbali kuhimizana juu ya namna ya kuishi pamoja na kwa amani na upendo," alisema.

Alisema mambo mbalimbali yanazaliwa katika ushirikiano huo na kugundua ukuta ulikuwa unajengwa kutokana na mitizamo tofauti hakuna mtu anayekwazwa na mwingine kwa kusema juu ya imani yake ikiwa hailingnishwi na nyingine.

Shoo aliongeza kuwa shida inatokea pale watu wanapoinua dini zao juu ya wengine na kuleta utengano.

Makamu Sheikh wa Mkoa wa Kilimanjaro, Sheikh Mlewa Shaaban, alisema kila mmoja ana dini yake, lakini wote wana mwabudu Mungu mmoja.

Alisema hapo mwanzo ilikuwa mashekhe na maaskofu hawawezi kukaka pamoja ila kamati hiyo imewakusanya pamoja na neno lao limekuwa juu ya amani na maendeleo ya Tanzania.

"Tuondoe tofauti zetu tupende maendeleo ya wenzetu ambayo yatatusaidia wote kufika mbali na kuwasaidia wale ambao hawajapata fikra na mwamko wa maendeleo. Mahusiano yetu ndiyo maendeleo yetu," alisema Shabaan.

"Kamati hii imekuwa ni chachu la maendeleo ya jamii zetu kwa kuwa tamko la viongozi wa dini likitoka kwa pamoja serikali inaona kwamba inayo haki na haja ya kutimiza kulingana na umoja wetu ambao ndiyo unataupa nguvu," Sheikh Shaaban alisema.

Ofisa Mradi ambaye ni mchungaji kutoka Norwegian Church Aid ( NCA) Andrew Munisi, NCA imesaidia miradi ya kuwezesha wananchi kiuchumi.

Alitaja uwekezaji katika kilimo cha mboga kwa umwagiliaji wa matone, ufugaji wa kuku, vikundi vya kuweka na kukopa, kilimo bora cha mahindi na masuala ya usimamizi wa rasilimali za umma ni sehemu ya uwezeshaji huo.

## Kampeni ya kurudisha uoto wa asili yazinduliwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KATIKA harakati za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, wadau mbalimbali wa kutunza mazingira wamezindua kampeni maalum ya kupanda miti zaidi 12, 000 katika maeneo yao ili kurejesha uoto wa asili uliopotea.

Wananchi hao wakazi wa Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na kikundi cha Amani 9 Arisi Marangu, kilichoko wilayani humo, watapanda miti maeneo ya taasisi za serikali, za kidini, za watu binafsi na maeneo ya wazi ili kurejesha uoto wa asili.

Katibu wa kikundi hicho, Hance Moshi, alisema kampeni hiyo inatarajia kuhifadhi mazingira katika maeneo tofauti ya wilaya hiyo ikiwamo hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ili kuendelea kulinda theluji yake. "Katika hatua za awali za kampeni yetu, leo tumeotesha miti 780 katika Sekondari ya Mieresini ili kuwahamasisha wanafunzi kuona umuhimu wa hifadhi ya mazingira na tunaamini juhudi hizi watazipeleka katika makazi wanayoishi na itakuwa tabia endelevu," alisema.

Alisema kampeni hiyo inayoendeshwa chini ya Shirika la Mazingira la Floresta Tanzania, itadumu kwa zaidi ya miaka 20 ili kurejesha uoto wa asili ulipotea kutokana na shughuli za kibadamu katika maeneo tofauti ikiwamo vyanzo vya maji na mito pamoja na mabadiliko ya tabia nchi.

Akizungumzia kampeni hiyo, Mkuu wa Sekondari ya Mieresini, Fidelis Barnabas, aliiomba serikali kutunga sheria za kudumu za kutunza mazingira ambapo kila mwanajamii atalazimika kuzifuata badala ya kila taasisi kuwa na utaratibu wake.

"Juhudi zinazofanywa na kikundi hiki ni za kuungwa mkono kwani zimeongeza chachu ya shule yetu katika jitihada ambazo tumeziendeleza kwa muda mrefu, tutajiwekea utaratibu kila mwanafunzi aoteshe mti na kuutunza mazingira hadi anapomaliza shule," alisema Barnaba.



Bandari Kigoma inavyopaa sambamba na uchumi wa majirani Burundi, DRC

Ukurasa 19

# BUFE

Ijumaa Juni 28, 2019
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## MIKOPO ELIMU YA JUU

## Uwekezaji una maana inapotolewa, kipindi cha malipo tafsiri 'inafifia'

Ukurasa 14



Kamanda wa Kikosi dhidi ya Ujangili Kanda ya Kaskazini-Arusha, Peter Mbanjoko. Kwa nyuma ni pikipiki na baiskeli zilizokamatwa zikisafirisha nyara za serikali. **PICHA: SALOME KITOMARI, ARUSHA**

OPERESHENI UJANGILI

## Ujangili wa tembo umeshuka, tabu yahamia mitaa mipakani

Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

Na Beatrice Moses

MIKOPO ELIMU YA JUU

# Uwekezaji una maana kipindi cha malipo taf

"KUKOPA harusi kulipa matanga." Ni misemo ya Kiswahili, inayotumika kwa wadaiwa sugu, ikiwa ni hali ya kuwasimanga walipe madeni yao.

Hilo ni jambo ambalo wanavyuo wanaonufaika na mikopo wanapaswa kukwepa kwa kuhakikisha fedha wanazokopeshwa ili kugharamia masomo na vitabu, malazi wanazitumia ipasavyo.

Wakati maana ya harusi inaangukia katika furaha na chereko, matanga yanajulikana kuwa mkusanyiko wa watu kwa usio na furaha, kwa ajili ya kumaliza msiba. Huzuni inatawala kwa kiasi kikubwa.

Maisha ya mashindano miongoni mwa vijana hasa ya umiliki au matumizi ya vitu vya kifahari na vya anasa ni baadhi ya mambo yanayotajwa kuwaingiza kwenye wakati mgumu wanafunzi wengi vyuoni.

Miongoni mwao, wapo wananufaika na mikopo ya masomo iliyotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) nchini.

Matumizi ya simu zinazouzwa kwa gharama kubwa, mavazi ya gharama, luninga na radio za kisasa yanawavutia wengi. Pia maneno ya dhihaka na kubezwa yamewachochea baadhi kuingia kwenye mkumbo wa kutumia vibaya mikopo hiyo.

Wakati upande wa wazazi ni wazi kwamba wengi hasa kwa kipato cha chini na kile cha kati hushukuru kwa uwepo wa mikopo hiyo, kwa kuwa imesaidia vijana kutimiza ndoto zao za kuwa miongoni mwa wasomi.

Kutokana na gharama za ada na malazi zilivyo kwenye vyuo vingi hasa vya binafsi, hivyo mzazi anapoona jina la mwanawe ni miongoni mwa wanufaika wa mkopo, huwa na uhakika atafanikiwa kimasomo.




Wanafunzi wakifuatilia mikopo HESLB. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

**VIGEZO VIPYA HESLB**

Juni mwaka huu, Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu nchini (HESLB), ilitangaza mwongozo wa utoaji mikopo kwa mwaka wa masomo 2019/2020 unaotaja sifa, vigezo na utaratibu wa kuwasilisha maombi ya mikopo ya elimu ya juu.

HESLB imewasihi waombaji mikopo kuusoma kwa makini na kuuzingatia mwogozo huo, ili waepuke usumbufu kwa kukosea kujaza maelezo yanayohitajika kwenye fomu husika.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, anabainisha katika mwongozo wa mkopo wa HESLB, kwamba lengo linawawezesha waombaji mikopo kuandaa nyaraka muhimu zinazotakiwa.

Anasema katika mwaka wa masomo 2019/2020, serikali kupitia HESLB imepanga kutoa mikopo na ruzuku ya elimu ya juu yenye thamani ya shilingi bilioni 450 kwa jumla ya wanafunzi 128,285.

"Kati ya hao, wanafunzi 45,000 watakuwa wa mwaka wa kwanza, mwaka huu 2018/2019, unaoelekea mwisho jumla ya shilingi bilioni 427.5 zilitolewa kwa jumla ya wanafunzi 123, 000," alisema.

**UREJESHAJI MIKOPO**

Mbali na mwongozo huo, Badru hakusita kuelezea jinsi ambavyo urejeshwaji mzuri wa mikopo ulivyochangia kwa kiasi kikubwa kuongezwa idadi ya wanufaika wa mikopo.

> **"Ni katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano (serikali iliyopo) ndicho kipindi pekee fedha iliyokopeshwa imeweza kurudi kiasi kikubwa zaidi na kwa kasi ya haraka zaidi, kuliko ilivyowahi kuwa zamani," anasema.**

Anabainisha kuwa, serikali imefanikiwa kuongeza bajeti ya mikopo hiyo ya elimu ya juu, kutokana na urejeshwaji mzuri wa mikopo unaofanywa na wanufaika wa awali, ikilinganishwa na miaka iliyopita.

"Ni katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano (serikali iliyopo) ndicho kipindi pekee fedha iliyokopeshwa imeweza kurudi kiasi kikubwa zaidi na kwa kasi ya haraka zaidi, kuliko ilivyowahi kuwa zamani," anasema.

"Kwa sababu mwaka 2015 ilirejeshwa shilingi bilioni 90, lakini katika kipindi cha miaka minne, tunaelekea kurejesha shilingi bilioni 500, hivyo tunapata uhakika wa kukopesha wanafunzi wengi zaidi," anasema Badru.

**'NYUNDO' YA CAG**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Profesa Mussa Assad, alipokutana na waandishi wa habari mkoani Dodoma Aprili mwaka jana, kutoa mukhtasari wa ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18, alieleza kuwa HESLB imeshindwa kuwafahamu wakopaji mikopo ya elimu ya juu yenye thamani ya shilingi trilioni 1.46.

Anasema kiasi hicho cha fedha ni kikubwa sana, ikizingatiwa sheria ya bodi hiyo, inaitaka HESLB inatengeneza mtandao na kushirikiana na taasisi na mashirika mbalimbali, ili kuwatambua wadaiwa na kuwezesha kupata marejesho ya mikopo hiyo.

Pia katika ripoti yake ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali aliyoitoa mwaka 2017, Profesa Assad alieleza kubaini udhaifu katika uchukuaji wa hatua dhidi ya wadaiwa sugu wa madeni ya mikopo.

Anasema katika ukaguzi, bodi hiyo mwaka 2016/2017 ilibainika kuwa na wadaiwa sugu 163,394, wakati kumbukumbu zake zilizowasilishwa kwa



Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru.

# inapotolewa, siri 'inafifia'



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Profesa Mussa Assad.

wakaguzi, zilionyesha kuwapo wachache chini ya idadi hiyo.

Anabainisha kulikuwapo waajiri 70 walioshtakiwa ama kwa kuchelewesha makato ya mkopo au malipo ya madeni



> **Anasema katika ukaguzi, bodi hiyo mwaka 2016/2017 ilibainika kuwa na wadaiwa sugu 163,394, wakati kumbukumbu zake zilizowasilishwa kwa wakaguzi, zilionyesha kuwapo wachache chini ya idadi hiyo.**

waliyokusanya na katika faini iliyotozwa, ni asilimia 21 tu ndiyo iliyokusanywa kwa wakati huo.

Prof. Assad anasema, baada ya kubainisha udhaifu huo alipendekeza HESLB kuandaa kanzidata ya wanufaika wa mikopo yenye viasharia vya hatari na kuiunganisha na mikakati urejeshaji mikopo na ulipaji wa madeni husika, kwamba ni hatua za kuongeza ufanisi katika ugawaji na matumizi ya rasilimali hasa kubaini wanufaika wa mikopo.

Alipendekeza kuwa HESLB kutumia teknolojia inayofaa ikiwezekana kama ile ya malipo kwa njia ya simu ili kurahisisha mchakato wa urejeshaji wa mikopo na ulipaji madeni ya mikopo. Pia, Profesa Assad alipendekeza bodi hiyo kutambua na kuchukua hatua za kisheria mara kwa mara dhidi ya wadaiwa sugu na wanufaika wanaokiuka masharti ya ulipaji mikopo ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wadhamini na waajiri wao.

Alipendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ijitathmini kama ina uwezo wa kuendelea kusimamia utendaji wa moja kwa moja wa HESLB katika urejeshaji wa mikopo, la sivyo iipe taasisi nyingine ya serikali kama vile Wizara ya Fedha na Mipango yenye ujuzi na uzoefu wa masuala fedha.

## Mbunge kutibua biashara Jumuiya Afrika Mashariki?

MATAMSHI ya Mbunge wa Starehe nchini Kenya, Charles 'Jaguar' Kanyi, kuwatishia raia wa kigeni wanaofanya kazi nchini Kenya yaliwasilishwa katika ya kikao cha Bunge la Kenya ili kujadiliwa, yanatibua mambo ya biashara na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Hatua hiyo inajiri huku mbunge huyo akizuiliwa katika kituo cha polisi usiku kucha, ambapo akisubiri kufikishwa mahakamani hapo jana.

Mtandao wa runinga ya Citizen nchini Kenya, ulisema licha ya wabunge wengi kushutumu jinsi ambavyo Jaguar alitoa hoja yake , baadhi yao walikubaliana kwamba kuna suala tata kuhusiana na raia wa kigeni ambalo lilihitaji kuzungumziwa.

Kulingana na mtandao huo suala hilo liliwasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Uhusiano wa Nchi za Kigeni Katoo Ole Metito, katika taarifa yake, akithibitisha kwamba raia wa kigeni hususan kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki wana uhuru wa kufanya biashara nchini Kenya.

"Tunashutumu sana matamshi yoyote ya chuki yanayokiuka msimamo huu unaotuleta sisi pamoja kama taifa na kuthibitisha sera ya kuwakaribisha raia wote wa kigeni," alisema mbunge huyo wa Kajiado Kusini.

Matamshi yake yaliungwa mkono na Mbunge wa Suba Kaskazini John Mbadi, ambaye aliwasihi wabunge wenzake kutotoa matamshi mbele ya umma kwa lengo la kujitafutia umaarufu na badala yake kuchukua tahadhari.

"Kama bara, tunahitaji kukuza uwiano katika mipaka yetu ili kutafuta ajira. Wakenya wako huru kwenda Tanzania kufanya biashara iwapo biashara hiyo ni halali", alisema Mbadi.

"Sio sera ya Kenya kuwafukuza Waganda, Watanzania au Wasomali iwapo wako hapa kwa mujibu wa sheria na wanafanya biashara halali," aliongeza.

HISTORIA FUPI

Charles Njagua Kanyi al maarufu Jaguar ni mwanamuziki, mwanasiasa na mjasiriamali na inaaminiwa kuwa mmoja wa wasanii tajiri nchini Kenya na katika eneo la Afrika Mashariki.

Alizaliwa katika familia ya maskini yenye watoto watatu. Jaguar alisomea katika shule ya msingi mjini Nairobi na akiwa na umri wa miaka 11 alifiwa na mama yake ambaye wakati huo alikuwa ndiye mlezi wake pekee.

Alilazimika kufanya kazi za vibarua ili kujikimu kimaisha na moja ya kazi alizozifanya ilikuwa ni kazi ya ukondakta wa mabasi ya abiria, maarufu daladala au matatu, na kwa msaada wa marafiki aliweza kumaliza shule.

Rekodi ya Jaguar ndiyo ya kwanza iliingia sokoni mnamo mwaka 2004 na baadaye akajiunga na kampuni ya muziki ya Afrika Mashariki Ogopa Deejays mnamo mwaka 2005 na kuipua miziki mmoja baada ya mwingine miongoni mwake ni "kigeugeu." Uliovuma sana na kupokea tuzo nyingi.



Mbunge wa Jimbo la Starehe nchini Kenya, Charles Jaguar Njagua.
**PICHA: MTANDAO**

BIASHARA

ZAO LA OPERESHENI TOKOMEZA...

# Ujangili wa tembo umeshuka, tabu yahamia mitaa mipakani

• Hujuma utalii Arusha katika sura mpya

**Na Salome Kitomari**

SEKTA ya utalii inaongoza kwa kuingiza fedha za kigeni kwa asilimia 25 nchini na inachangia Pato la Taifa kwa asilimia 17.2, ikiajiri zaidi ya watu 600,000 na ajira zisizo rasmi ni milioni 1.4.

Aidha, mwaka 2018 watalii walioingia nchini ni milioni 1.5 ambao waliiingizia nchi Dola za Marekani bilioni 2.4, huku asilimia 28 ya mapato ikipatikana kutokana na Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro (Kinapa).

Eneo lililohifadhiwa kwa ajili ya hifadhi za taifa, mapori ya akiba, hifadhi za jamii, mapori tengefu na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wastani wa mtalii kuishi nchini ni siku 11.

Licha ya umuhimu wa maeneo hayo, bado kuna changamoto ya ujangili wa wanyamapori kwa ajili ya kutokuwapo na biashara, ambao umeshika kasi baada ya jitihada za serikali za kupambana na ujangili wa tembo na faru.

Huko nyuma ujangili mkubwa ulikuwa kwa meno ya tembo na pembe ya faru, ambao kwa sasa umetoweka nchini, baada ya serikali kuunda kikosi kazi cha taifa cha kuzuia ujangili nchini, kinachojumuisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama.

Waandishi wa habari 20 kutoka nchini Thailand na Tanzania walioko kwenye programu maalum ya kuandika habari za ujangili iliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania walitembelea maeneo mbalimbali ya hifadhi.

Ni ziara iliyowafikisha wanahabari katika Hifadhi ya Ngorongoro na Hifadhi ya Wanyamapori ya Burunge (Burunge Wildlife Management Area (WMA) na ofisi za kikosi maalumu cha kupambana na ujangili kanda ya Kaskazini - Arusha.

Lengo kuu ya programu ni kuwawezesha wanyama wanakopatikana na jinsi biashara hiyo inafanyika hadi kwenda Barani Asia.

Walitembelea nchini Thailand, ambako ndiyo njia kuu ya kupitisha bidhaa za ujangili, hasa meno ya tembo na pembe za faru kutoka Afrika na kwingine duniani.

Sheria ya wanyamapori namba tano inakataza watu kumiliki nyara za wanyamapori na kuwinda kiharamu.

**Vita ya ujangili**

Katika mahojiano na Mkurugenzi Msaidizi wa kuzuia ujangili nchini, Robert Mande, jijini Dar es Salaam, anasema ujangili ulikuwa tatizo kubwa miaka 2010 hadi 2014 zaidi ya asilimia 60 ya tembo walitoweka na ndipo iliiamsha serikali kuchukua hatua kwa kuanzia mpango kupambana na ujangili nchini. Anasema mwaka 2013 serikali ilifanya 'Operesheni Tokomeza' iliyounganisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama kukabiliana na tatizo hili na kwamba biashara ya pembe za ndovu na meno ya tembo ilikuwa kubwa kutokana na soko kubwa nchi za Asia.

"Kwa wakati huo kilo moja ya jino la tembo iliuzwa Dola 500 ikiwa Tanzania na Dola 2,000 ikiwa China na kuwaleta watu wenye uchu wa kutajirika ni biashara inahusisha rushwa, utakatishaji wa fedha, ujangili na mengineyo," anasema.

**"Haya ni makosa yanayofanywa na wataalamu walioko serikalini, mashirika ya umma, binafsi ambao wamepewa dhamana ya kusimamia rasilimali na jambo fulani, wakijiingiza kwenye rushwa, utakatishaji fedha au ujangili ni tishio kubwa sana," anasema.**



Mkurugenzi Msaidizi wa Kuzuia Ujangili nchini, Robert Mande (kulia), akimwonyesha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, pembe ya Faru John. **PICHA: MAKTABA.**

**MWENYEKITI MZUIA UJANGILI**

Mande, Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Taifa cha Kuzuia Ujangili, anasema katika kuchambua uhalifu huo walibaini kuna makosa yanayoitwa 'white color crime" ambayo hufanywa na watu wenye madaraka na maamuzi.

"Haya ni makosa yanayofanywa na wataalamu walioko serikalini, mashirika ya umma, binafsi ambao wamepewa dhamana ya kusimamia rasilimali na jambo fulani, wakijiingiza kwenye rushwa, utakatishaji fedha au ujangili ni tishio kubwa sana," anasema.

"Tumegundua hili ni tatizo kubwa kuliko yote, ushiriki wa wataalamu wa maeneo mbalimbali katika hatua mbalimbali unasababisha uhalifu kuendelea na kuwa mgumu kupambana nao ni rahisi mtu kushiriki kwenye uhalifu, bila ya kujulikana kupambana na mhalifu ambaye humjui na ana nafasi kwenye udhibiti wa sheria ni ngumu sana," anabainisha.

Anasema, kikosi kazi cha taifa kimeshirikisha vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama, wanakaa ofisi moja kupambana na makosa ambayo ni ngumu kwa chombo kimoja kufanikiwa.

"Mafanikio ni mengi sana mana hivi karibuni kesi ya Malkia wa Tembo imehukuiwa amefungwa miaka 17 na kulipa faini ya dola milioni 20 ni mafanikio ya kufanya kazi kwa pamoja," anasema.

Anasema, kuanzia mwaka 2016 hadi sasa ujangili wa tembo umeshuka kwa kiasi kikubwa na sasa umeibuka ujangili mwingine wa nyama kwa ajili ya biashara.

**UJANGILI TISHIO**

Kamanda wa Kikosi dhidi ya Ujangili Kanda ya Kaskazini-Arusha, Peter Mbanjoko, anasema katika miaka ya 1970 na 1980, faru na tembo waliuawa sana na baadaye serikali ilianzisha kikosi cha kupambana na ujangili katika kanda za Arusha, Mwanza, Tabora na Iringa.

Anasema, vikosi hivyo vinafanya kazi kwa kushirikiana na taasisi zote za uhifadhi, huku wakiangalia zaidi maeneo ya nje ya NCAA, Game Controlled Area 20, mapito ya wanyama yaani shoroba, WMA maeneo ya mtawanyiko wa wanyama na maeneo mengine ya wazi.

"Kuna aina mbili ya ujangili kwa sasa ambao ni kwa ajili ya kupata kitowewo na nyama kwa ajili ya biashara. Sheria inasema ukikutwa na kiungo chochote cha mnyamapori maana yake umeua na hatua zinachukuliwa dhidi yako," anasema. Kwa Kanda ya Kaskazini yaani mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga, Julai 2018 hadi sasa watuhumiwa 113 walikamatwa wakiwa na nyara za serikali na makosa mengine yanayohusika na ujangili ambao zaidi hutumia nyaya kuwakamata wanyama.

Anasema, kati ya watu 22 walihusika na matukio ya moto, 306 walikutwa na nyara mbalimbali.

Mbanjoko anataja vifaa vilivyokamata na idadi yake kwenye mabano kuwa ni pikipiki (40), baiskeli (29), waya (117), mishale (6), tochi (24), visu (25).

Aidha, takwimu zinaonyesha kuwa mwaka 2018 tembo 12 walikufa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo magonjwa, uzee na mmoja aliuawa kutokana na kusababisha madhara kwa jamii na kwamba wote walikutwa na meno yao.

Kamanda huyo anasema, kati ya kesi 113, kesi 106 zilifunguliwa mahakamani, 12 zinachunguzwa, tisa zilihukumiwa na tatu walihukumiwa miaka 50 jela, watatu waliachiwa na 15 walitozwa faini za Sh. milioni 74,114,650 na 80 zipo katika hatua mbalimbali za usikilizaji.

**UJANGILI ULIVYO**

Mande anasema, ujangili wa tembo ulivyoshuka, ujangili wa wanyamapori umeanza kuongezaka, hasa maeneo ya mpakani mwa Kenya na Tanzania eneo la Serengeti.

"Watu wengi wamefikiri ukiua tembo utakamatwa wamehamia kwenye uhalifu wa nyama kwa ajili ya biashara, kikosi kazi kimejipanga katika kada kumi," anasema.

Anazitaja kanda hizo kuwa ni Serengeti Kaskazini Mashariki, Serengeri Kusini Magharibi, Tarangire Manyara, Kilimanjaro Mkomanzi, Selous Kusini, na Selous Kaskazini, Ruaha Rungwa, Katavi, Moyowosi na Ibanda Rumanyika.

"Tunaanzisha kikosi maalumu cha kuratibu, kila kanda kuna vyombo vyote vya ulinzi na usalama vikishirikiana na taasisi za wanyamapori zilizopo maeneo husika chini ya uratibu wa kikosi kazi taifa," anabainisha.

Anasema, msukumo wanaoupata kwa Rais John Magufuli, katika kupambana na ujangili wanaona matokeo makubwa, ikiwamo sheria ya kulinda rasilimali za taifa na zinufaishe wananchi wote imetoa nguvu zaidi na imetoa uwanja mpana wa kulinda raslimali za taifa.

**WANYAMA WANAOWINDWA**

Anasema eneo lililokithiri ni Bunda mkoani Mara ambako jamii inapenda nyama ya wanyamapori hasa wakati wa kuhama kwa nyumbu, kwa wananchi kutenga nyaya kwenye mapito ya wanyama kuhama.

"Mtu anaweka nyaya 100 hadi 200, wanakaa porini mwezi mmoja hadi miwili wanatega wanyama 1,000 na nyama zinasafirishwa kwenda Kenya," anasema. Anasema uchunguzi wao ulibaini kuwa kuna mtandao wa watu wanawafadhili kwa kuwapa fedha, kuwanunulia chakula ili wazalishe nyama nyingi ya kupeleka Kenya.

"Mtu akiweka nyaya 500 anakamata nyumbu 200, wanaikausha na kuisafirisha nje tani kwa tani, kwa sasa tumeweka kikosi kazi kina watu kutoka taifa, polisi Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) na Taasisi ya Wanyamapori (Tawa) kuhakikisha tunawadhibiti," anasema.

Anasema wanyama wanaolengwa zaidi ni nyumbu, nyati na pundamilia ambao hupatikana kwa wingi na haraka.

Anasema maeneo ya Longido Arusha wanalinda twiga na kwamba mwaka jana wanyama hao waliuawa na uchunguzi ulionyesha ni kwa ajili ya biashara," anasema.



Wataalamu wa USAID Protect Tanzania na Washington Marekani, wakiwa pamoja na wafugaji wa jamii ya Kimasai wanaoishi ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), eneo hilo linajulikana kama Masai Boma. **PICHA: SALOME KITOMARI**

## BIASHARA KATIKA PICHA



Sehemu ya majengo ya biashara yanayoendelea kujengwa kando ya barabara ya Bagamoyo eneo la Kijitonyama jijini Dar es Salaam, ambayo yanaongeza wigo wa upangaji wa ofisi za biashara. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Baadhi ya wananchi wa jijini Dar es Salaam wakiwa kwenye Uwanja wa Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara kufuatilia majina yao ya kuruhusiwa kufanyakazi na biashara ndogo kwenye uwanja huo jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Mchuuzi wa matunda akiwa kwenye sehemu yake ya biashara eneo la Namanga jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Na Jenifer Julius

INGAWA wanawake wana mchango mkubwa katika kufanikisha kila jambo, kutokana na uwezo na umahiri walio nao wa kubeba na kuhudumia familia, inashangaza kuona kuwa wanaachwa nyuma kwenye ulinzi wa mazingira kwa mfano kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mara nyingi kinamama wanaonekana kuwa hawawezi kufanya jambo lolote la maendeleo na kuzushiwa misemo ya kuwakejeli kuwa sehemu sahihi kwa mwanamke si kwingine bali ni jikoni.

Hali hii inawafanya wanaume kujihusisha na mambo mengi na wakati mwingine kuelemewa na mzigo wa majukumu ya kufanya maamuzi na hata kushindwa kufikia malengo kwa wakati.

Kwa mfano utelekezaji wa Makubaliano ya Paris wa kupunguza joto la kimataifa kwa nyuzi joto mbili hauwahusishi wanawake, utoaji wa maamuzi umekuwa wa upande mmoja ingawa wanawake ndiyo waathirika wakuu.

Nipashe inazungumza na Ndivile Mokaela, Mratibu Miradi wa Shirika la Kimataifa la Gender CC, linaloshughulika na haki za wanawake lililoko Afrika ya Kusini kuhusu nafasi ya mwanamama katika mchakato huo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Katika mahojiano hayo, Ndivile Mokoela, anayefanyakazi ya Mratibu wa Mradi Unaoshughulikia Haki za Wanawake, anasema analenga zaidi kuhakikisha kuwa wanaondoa pengo lililopo kati ya wanawake na wanaume katika miradi na shughuli mbalimbali za kiuchumi, maendeleo na kuifanya dunia kuwa sehemu bora ya kuishi. Endelea...

**Nipashe:** Tungeomba kufahamu mnafanya shughuli gani katika mchakato huu?

Ndivile: Shirika letu lipo nchini Afrika Kusini na linashirikiana na kufanya kazi na makundi mbalimbali sehemu mbalimbali kama vile wanaharakati, mashirika ya kiraia, taasisi za kiserikali.

Pia tunashirikiana na wataalamu kutoka kanda za Kusini mwa Afrika wanaofanya kazi na haki za wanawake, usawa wa kijinsia na ushirikishwaji wanawake kwenye masuala ya hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi.

**Nipashe:** Nini hasa madhumuni ya shirika lako?

**Ndivile:** Kama nilivyoeleza mwanzo moja ya masuala tunayoshughulika nayo ni kuhakikisha wanawake wanahusishwa katika vita dhidi ya mabadiliko ya hali ya hewa ili kuweza kufikia Makubaliano ya Paris. Na tunashirikiana na wanaharakati wanaotetea haki za wanawake kutoka mataifa mbalimbali.

Kwa hiyo tumeunda umoja wetu unaoitwa Kituo cha Masuala ya Jinsia au Women Gender Constituency (WGC)) ambacho kipo chini ya Mkataba wa Mfumo wa Mabadiliko ya Tabia Nchi wa Umoja wa Mataifa (UNFCCC).

Lengo kuu ni kuhakikisha Makubaliano ya Paris yanayoelekeza mataifa kutengeneza sera zinazotekelezeka kuhusu uhusishwaji wa wanawake katika vita



Ukosefu wa kuni unaotokana na uharibifu wa misitu unaogeuza nchi kuwa jangwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi unaathiri zaidi wanawake ambao ndiyo wanaotafuta nishati kwa ajili ya kuzihudumia familia: **PICHA:MTANDAO.**

MABADILIKO TABIANCHI

# Mwanamke ana nafasi ya kuleta mafanikio

> **“Vilevile tunafanya ufuatiliaji wa ajenda zinazojadiliwa kuhusu makubaliano ya Paris na kuona kama kwa namna yoyote ile wanawake wanapewa nafasi ipasayo katika kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa.**

dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi.

**Nipashe:** Niambie zaidi kuhusu WGC

**Ndivile:** WGC inajumuisha mashirika 28 kutoka sehemu mbalimbali duniani, yanayofanya kazi pamoja kuhakikisha kuwa sauti ya mwanamke na haki yake ya kupambana na mabadiliko ya tabia nchi inapewa kipaumbele.

Mtandao wetu una watetezi kutoka mataifa 60 yanayowakilisha maelfu ya wanawake duniani.

Kwa vile tunaelekea kwenye mkutano mkubwa wa mabadiliko ya tabia nchi wa Cop 25, tunajaribu kushawishi nchi kuangalia umuhimu wa kubadilisha será zao na kutoa vipaumbele kwa wanawake.

Vilevile tunafanya ufuatiliaji wa ajenda zinazojadiliwa kuhusu makubaliano ya Paris na kuona kama kwa namna yoyote ile wanawake wanapewa nafasi ipasayo katika kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Jambo jingine ni kuonyesha upungufu uliopo katika sera ya ustahamilivu katika mabadiliko ya tabia nchi na kutoa mapendekezo ya nini kifanyike ili kupata ufumbuzi.

Tunalenga pia kukutana, kufanya vikao, kupanga mipango ya baadaye hasa tunapoelekea kwenye mkutano mkubwa wa mabadiliko ya tabia nchi duniani, ambao ajenda nyingi zinakwenda kumalizika. Tunataka kuona ni kwa jinsi gani uhusishwaji wa wanawake utawekewa uzito katika mkutano huo.

**Nipashe:** Sawa, unaweza kutuambia kwa ufupi ni upungufu gani mwingine mliouona katika sera hizo zinazowaweka nje ya uwanja wanawake?

**Ndivile:** Kuna upungufu mwingi lakini kikubwa ni wanawake kuwakilishwa kwa kiwango kidogo katika makubaliano kuhusu sera ya mabadiliko ya tabia nchi.

**Nipashe:** Unafikiri kwa nini utekelezaji wa mipango ya kuwashirikisha wanawake unadorora?

**Ndivile:** Jukumu la kufanya utekelezaji lipo chini ya nchi na kuna mambo mengi yanayochangia, mojawapo ni makubaliano ya Paris kutochukulia suala la wanawake kwa namna ya kipekee, lakini pia usimamizi mbovu, nia potofu zilizojengeka kwamba wanawake hawawezi kufanya kitu kikubwa katika jamii zaidi ya kuhudumia familia.

**Nipashe:** Kitu gani unataka Makubaliano ya Paris yakipe kipaumbele kuhusu uhusishwaji wanawake?

**Ndivile:** Ni kila nchi iweke kipaumbele kuhusu ushirikishwaji wa wanawake katika miradi na mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kulingana na muktadha wa mataifa yao.

Sera za ustahimilivu katika mabadiliko ya tabia nchi ziangalie data sahihi katika tukio husika mfano ni nani anaathirika zaidi kunapotokea majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi? Kama kimbunga, mafuriko, joto kali, ukame na magonjwa?

Imeshathibitishwa kuwa wanawake ndiyo waathirika wakuu kunapotokea majanga kwa sababu mbalimbali kwa sababu ndiyo wanaoweka maslahi ya watoto wao mbele.

Mwanaume ana uwezo wa kujiokoa mapema lakini mwanamke anachelewa kwa sababu anawaza kuokoa wengine kama watoto kwanza.

Kwa hiyo tukiangalia hizi data za wanawake wangapi wameathirika na wanaume wangapi wameathirika kura nyingi zinamwangukia mwanamke na ndipo sera itungwe ikielekeza kwa anayeathirika zaidi ambaye ni mwanamama.

Tukija upande wa athari za mabadiliko ya tabianchi zinamgusa mwanamke moja kwa moja. Mfano kutafuta maji umbali mrefu, kuathirika moshi unaotokana na vyanzo hatarishi vya moto.

Mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri afya ya mwanadamu lakini mwanamke ndiye anayeathirika zaidi hasa katika masuala ya uzazi hatarishi kama vile kutumia vifaa hatarishi zikiwamo kemikali.

Lakini linapokuja suala la kufanya maamuzi na kutengeneza sera, anaongelewa zaidi lakini hatekelezwi au huguswi na utekelezaji.

**Nipashe:** Ni kweli, unafikiri nchi zinazoendelea zinahitaji sera ya namna gani katika kuhusisha wanawake katika vita dhidi ya mabadiliko ya tabianchi?

**Ndivile:** Ndiyo, nchi zote zinahitaji kuchukua hatua za ziada kwa sababu ukiangalia muda umeshatutupa mkono, lakini nchi zinazoendelea zinahitaji uangalizi wa karibu ikiwezekana msaada kutoka nchi zinazoendelea kwa sababu wenzetu wameathirika na masuala ya mila na utamaduni hasa sehemu za vijijini.

Na niseme kwamba haitokuwa rahisi kufanya utekelezaji kwa mfano nchini kwetu Afrika Kusini tuna sera inayojitegemea kuhusu masuala ya kijinsia, nafikiri nchi zinazoendelea zinatakiwa kufanya hivyo.

**Nipashe:** Ndiyo, ni vitu gani unafikiri vikiwapo katika sera ya mabadiliko ya tabia nchi vitasaidia kuhusisha wanawake kwa urahisi.

**Ndivile:** Unajua, tumeongea na watengeneza sera na watoa maamuzi, na unajua kundi hili la wanawake limefanya utafiti na kuja na masuluhisho kadha wa kadha.

Moja ya mambo tulioyaona yanahitajika ni kuwako na mfuko unakaokuwa unawasaidia wanawake pekee ikitokea majanga.

Na pesa hizo zinasaidia pia katika kufanya uhamasishaji na kuwaingiza wanawake katika mapambano. Kuwaonyesha wanawake fursa zinazopatikana ndani ya athari hizi ambazo zitasaidia kupunguza joto la dunia.

UCHUMI

**Na Mary Geofrey, aliyekuwa KIGOMA**

KATIKA mwendelezo wa makala za ziara ya kukagua maendeleo ya bandari nchini, baada ya ushuhuda wa kwingineko, safari hii ni yaliyojiri Kigoma. Fuatilia...

NI vigumu kwa mtu kuuzungumzia umuhimu wa bandari katika kukuza maendeleo ya uchumi wa Taifa, hasa katika zama iliyopo ya kutimiza ndoto ya "kuelekea Tanzania ya Viwanda' pasipo kuitaja Bandari ya Kigoma, iliyoko katika Ziwa Tanganyika.

Hiyo ni bandari muhimu, pia kwa uchumi wa nchi jirani zinazoitumia za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Burundi, Zambia na Rwanda.

Bandari ya Kigoma, kiungo cha kati inayobeba umaarufu wa sura mbili, kuvusha bidhaa kwa nchi hizo zinazonunuliwa kutoka Tanzania, pia wanazozinunua kutoka nchi za mbali zikipitia Bandari ya Dar es Salaam.

Bandari hii iko Magharibi mwa Tanzania na ilijengwa kuanzia mwaka 1922 na ikachukua miaka mitano kukamilika mwaka 1927.

Historia inaonyesha bandari hiyo muhimu ilijengwa na Serikali ya Wakoloni wa Ubelgiji waliokuwa wakitawala Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Burundi na Rwanda na ikaanza kufanya kazi mwaka huo 1927.

Kwa sasa inasimamiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Meneja Mkuu wa Bandari za Kigoma, Ajuaye Msese, ndiye mwenye jukumu la kusimamia bandari zote zilizopo mwambao wa Ziwa Tanganyika kwa upande wa Tanzania, ikijumuisha bandari ndogo za Kasanga, Kipili, Kibirizi, Kabwe, Kagunga na Sibwesa pamoja na bandari ndogo nyinginezo maarufu kama 'Cluster Ports.'

Msese anasema, utendaji kazi wa bandari hizo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa Tanzania na nchi jirani, jukumu linaloenda sambamba na bandari nyingine ndogo anazosimamiwa.

Anazitaja bandari ndogo zilizopo mkoani Kigoma kuwa ni Ujiji, Mwamgongo, Mtanga, Ilagala, Karago, Tongwe, Sigunga, Kaparamsenga, Herembe, Rukoma, Lagosa na Kalya. Msese anasema bandari zilizopo katika mkoa wa Katavi ni Ikola na Kalema, wakati zilizopo katika mkoa wa Rukwa ni Kasanga, Korongwe, Kirando (Mtakuja), Ninde, Msamba, Wampembe na Kala.

Anasema pia bandari hizo zina gati ambazo ni miundombinu muhimu katika kuhudumia meli, abiria na mizigo.

Msese anabainisha kuwa, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2013/2014 hadi 2017/2018) mtiririko wa shehena umekuwa ukipanda, kutokana na ufanisi wa huduma inayotolewa na bandari sambamba na ukuaji uchumi katika nchi jirani, zinazosafirisha shehena kupitia Bandari ya Kigoma.

"Dira ya Bandari ya Kigoma ni kuwa 'gateway' ya mizigo ya maziwa makuu," anaeleza meneja huyo na kuongeza kuwa, uchumi wa nchi wateja wake; DRC na Burundi unakua kwa kasi kutokana na hali ya utulivu wa kisiasa.



Mwonekano wa Bandari ya Kigoma. **PICHA: MARY GEOFREY**

# Bandari Kigoma inavyopaa sambamba na uchumi wa majirani Burundi, DRC

- Meneja: Miaka 4 ijayo tutapanda mara nne
- Asifu ufanisi reli ya kati inampa 'ulaji'

Msese anataja sababu nyingine ni ongezeko la shehena na kuimarika kwa reli ya kati.

**MELI ZINAZOHUDUMIWA ZAONGEZEKA**

Meneja huyo anasema, idadi ya meli zinazohudumiwa katika Bandari ya Kigoma zimeongezeka katika kipindi cha miaka mitano kutoka 296 zenye uwezo wa kuchukua tani 200,000 mwaka 2013/14 hadi meli 434 mwaka 2017/18. Ni wastani wa asilimia 146.

Anasema, katika mwaka 2014/15 meli zilikuwa 378; mwaka 2015/16 zilikuwa meli 315 na mwaka 2016/17 zilikuwa meli 307.

Pia, anasema shehena inayohudumiwa katika bandari hiyo imeongezeka kutoka tani 88,390 mwaka 2013/14, hadi tani 196,844 mwaka 2017/18. Msese anasema katika mwaka 2014/15 walihudumia tani 99,386, mwaka 2015/16 walihudumia tani 139,570 na mwaka 2016/17 walihudumia tani 136,573.

"Bandari ya Kigoma inahudumia shehena mchanganyiko, mafuta na makasha. Shehena inayopita katika bandari hii imekuwa ikiongezeka pamoja na matatizo ya njia za usafirishaji hususani reli," anasema Msese. Anasema shehena wanazohudumia katika bandari hiyo ya Kigoma, ni mchanganyiko wa mafuta na makasha yanayotoka na kuelekea katika nchi hizo mbili; DRC na Burundi.

"Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2013 hadi mwaka 2018, idadi ya meli tunazohudumia katika bandari hii imeongezeka, pamoja na idadi ya shehena tunayohudumia jambo lililosababisha bandari kukusanya Sh. milioni 18.446 sawa na ongezeko la asilimia 29.2 katika kipindi hicho," anaeleza Msese. Kuhusu mapato hayo, anasema mwaka 2013/14 walikusanya Sh. milioni 2.793 hadi Sh. milioni 6.752 mwaka 2017/18.

Anasema bandari hiyo iliyodumu kwa miaka 100 inategemea reli ya kati na kwamba mwaka 2014/15 walikusanya Sh. milioni 2.090; mwaka 2015/16 walikusanya Sh. milioni 2.669 na mwaka 2016/17 walikusanya Sh. milioni 6.752.

Kwa mujibu wa Meneja Msese, matarajio ni mapato hayo kupaa mara nne zaidi katika kipindi cha miaka minne ijayo.

Anasema Bandari ya Kigoma, inatoa huduma kwa wateja wa aina mbili, kwa maana ya meli na mizigo na asilimia 60 ya mizigo inayopita katika bandari hiyo inaelekea DRC.

**VIFAA**

Meneja huyo anasema, pia katika kutekeleza majukumu kwa ufanisi mamlaka imeendelea kuboresha vitendea kazi kwa kufanya manunuzi ya vifaa vipya.

Anasema vifaa hivyo ni 'scanne' mpya moja katika Bandari ya Kigoma na mashine ya kuinulia mizigo yenye uwezo wa tani 15.

"Aidha, kwa mwaka wa fedha 2019/20 mamlaka imepanga kununua 'forklift' mbili kwa ajili ya Bandari ya Kipili na 'Terminal Tractor' yenye uwezo wa kubeba tani 40," anasema.

Msese anaitaja Kigoma kuwa ni kiungo muhimu kiuchumi na kijamii kwa kuwa ipo karibu na nchi za ukanda wa Maziwa Makuu za Burundi na DRC.

**KINACHOIPAISHA KIGOMA**

Anasema kuwapo kwa njia ya reli inayounganishwa na Bandari ya Dar es Salaam na Kigoma, inaifanya bandari hiyo kuwa kiungo muhimu sana cha usafirishaji wa shehena kwenda au kutoka nchi za Burundi na DRC.

Aidha, anasema kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi katika nchi za Burundi na DRC, kunatoa fursa ya kuongezeka shehena bandarini Kigoma, hivyo kusaidia kukua kwa uchumi wa mkoa wa Kigoma na taifa kwa ujumla.

Msese anafafanua kuwa, kuanzishwa kwa Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZ) katika Mkoa wa Kigoma, ni matarajio ya kuongeza fursa za kibiashara kwa bandari hiyo tajwa. Anasema kwa upande wa usalama wa mizigo na abiria, TPA Kigoma imeimarisha ulinzi katika maeneo yote ya bandari, hali ambayo ni kigezo muhimu cha kibiashara kwao.

**UBORESHAJI WA BANDARI**

Ili kuhakikisha Bandari ya Kigoma inaongeza ufanisi katika kuhudumia meli, mizigo na abiria, Msese anasema TPA imewekeza katika miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile; ujenzi wa gati katika Bandari ya Kagunga; ujenzi wa gati ya Bandari ya Sibwesa iliyopo katika Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa.

"Mamlaka (TPA) ina jukumu la kujenga na kuendeleza miundombinu ya bandari katika mwambao wa Ziwa Tanganyika na inatekeleza miradi kadhaa," anasema.

Msese anataja mradi mwingine ni ujenzi wa gati katika wa ufukwe wa Kibirizi, unaotumiwa na majahazi na boti kwa ajili ya kusafirisha abiria na mizigo, pamoja na ujenzi wa ofisi za utawala bandarini.

"Miradi mingine ni ujenzi wa gati katika Bandari ya Ujiji na ujenzi wa gati katika Bandari ya Lagosa," anasema meneja huyo.

Msese anazungumzia miradi mingine ambayo TPA imewekeza na ipo katika hatua mbalimbali, ni pamoja na uendelezaji wa Bandari ya Kasanga, ujenzi wa barabara katika Bandari ya Kipili na ujenzi wa Bandari Kavu ya Katosho, itakayosaidia kupunguza mrundikano wa mizigo bandarini.

Hiyo inaelezwa ni kutokana na mipango iliyopo ya kuimarisha miundombinu ya reli na barabara, huku akifafanua kuwa, TPA itaendelea kuwekeza katika miundombinu na vifaa kwa kushirikiana na wadau wake.

Anawataja wadau hao ni wawakilishi wa meli, taasisi za umma na binafsi, wakala wa forodha na vyombo vya ulinzi na usalama, ili kuweza kuendelea kutoa huduma bora kwa meli, abiria na mizigo.

**DC KIGOMA**


Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Samson Anga, anasema kuwapo bandari hiyo na reli ya kati, kunasaidia kukuza uchumi wa mkoa huo na taifa kwa ujumla.

Anasema TPA wamekuwa wakitekeleza miradi mikubwa ya uboreshaji wa bandari za mkoa wa Kigoma ambayo itasaidia kukuza uchumi wa wananchi pindi itakapokamilika.

"Kwanza nimpongeze Rais John Magufuli kwa kuwezesha kukua kwa uchumi wa Taifa. Pia, wenzetu wa TPA ambao wanatekeleza miradi mbalimbali katika wilaya hii kuhakikisha wanakuza sekta hiyo na uchumi wa wakazi wa Kigoma," anasema.

Anasema kupitia miradi iliyopo katika wilaya hiyo itawezesha kuzalisha ajira za vijana wakati wa ujenzi na baada ya kukamilika kwa miradi hiyo.

UCHUMI




Mkuu wa Fedha wa Kampuni ya simu ya Huawei, Meng Wanzhou ambaye pia ni binti wa mmiliki wa kampuni hiyo ya China. **PICHA: MTANDAO**

# Kukua biashara ya nje Afrika, kuongezeka mivutano mataifa makubwa

**Na Nimi Mweta**

SERA za kukuza biashara duniani kwa wakati huu zimeingia katika mazingira yasiyo ya kawaida na nchi za Afrika zinajikuta katika lindi la mivutano ya kibiashara kati ya mataifa makubwa. Hata hivyo hakuna kanuni za wazi ni kwa njia gani masuala hayo yanaweza kutatuliwa.

Ingawa wengi katika vyombo vya habari na hasa majukwaa mitandaoni wanasikika wakisema tatizo hasa ni uongozi wa sasa nchini Marekani, kuwa haufuati taratibu za kawaida za biashara kimataifa kwa mfano suala zima la ushindani wa wazi, ukweli ni kuwa tatizo ni kubwa zaidi.

Hali halisi ni kuwa Marekani ina nafasi maalum katika mfumo wa biashara duniani, inayozua migongano kila wakati, na mara moja au mbili katika karne hufikia kuuweka mfumo mashakani.

Kinachotokea sasa kimsingi ni kilele cha mabadiliko katika mfumo wa biashara duniani ambayo Marekani iliyalazimisha katika miaka ya 1970, kutokana na kutoridhika na matokeo ya mfumo wa biashara uliokuwapo awali, wa aina fulani ya soko huria baada ya Vita Vikuu vya Pili kufikia tamati mwaka 1945.

Marekani kupitia taasisi changa za Umoja wa Mataifa, hasa Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia iliweka mifumo ambako takribani nchi zote zingeweza kuuza bidhaa zao Marekani kwa kuweka wenyewe bei ya kubadilisha thamani ya sarafu zao na dola ya Marekani.

Hapakuwa na mfumo wa kimataifa wa kudhibiti bei ya sarafu kwa dola ya Marekani, hivyo nchi nyingi zikaanza kujitutumua na thamani bandia ya sarafu zao, kibiashara.

Hali hiyo ikaanza kuwa mwiba kwa Marekani kwani mlingano wa thamani halisi ya bidhaa na huduma zinazolipiwa kwa dola ya Marekani ikaanza kupungua pale sera za uthabiti wa thamani ya sarafu kati ya Marekani na nchi nyingine zikipishana. Marekani kwa mfano haina mashirika ya umma katika uzalishaji au sekta yoyote ya uchumi ila mamlaka kadhaa za usimamizi wa sekta tofauti, kuhakikisha kuwa hakuna kampuni inayopiga dili na kuanza kutawala soko.

Nchi za Ulaya kwa upande mwingine zilikuwa na mifumo ya serikali kushiriki kwa mapana na marefu katika uzalishaji, na thamani ya sarafu zao ikawa inaendana na tija, ila wanaamua wao thamani rasmi, hali iliyofikia utawala wa Rais Richard Nixon wa chama cha Republican kama alivyo Donald Trump hivi sasa kuuvunjilia mbali mfumo huo. Matrilioni ya nchi changa yakayeyuka.

Mwaka 1969 Rais Nixon aliondoa ubadilishaji fedha za Marekani kwa mpangilio maalum wa dola 35 kwa wakia moja ya dhahabu safi, akaacha sarafu ya Marekani ijitafutie thamani au bei yake kwa sarafu nyingine katika soko, kwa ushindani kati ya wanunuzi na wauzaji.

Ndiyo hapo sarafu za nchi zenye uchumi dhaifu usio wa soko zikaanza kuyumba na kupoteza thamani, wakati nchi za Afrika zenye uchumi wa soko kama Kenya hazikupoteza sana thamani ya sarafu zao.

Hata hivyo kuyumba kwa sarafu kulisaidia kukuza uwekezaji kwani amana kama viwanja, nyumba, hisa zilikuwa rahisi kwa wawekezaji wa nje ukilinganisha na Kenya na hali hiyo kimsingi haijabadilika bado.

> **Mwaka 1971 Marekani ikapunguza rasmi thamani ya fedha yake na baadaye mtindo wa kuacha ipate thamani yake kupitia soko ukabaki kama mfumo.**

Mwaka 1971 Marekani ikapunguza rasmi thamani ya fedha yake na baadaye mtindo wa kuacha ipate thamani yake kupitia soko ukabaki kama mfumo.

Ugomvi wa Marekani na nchi kadhaa kubwa duniani, hasa China, ni mpangilio tofauti ila una mizizi katika hali kama ile ya kwanza, kuwa Marekani kuna sekta binafsi pekee na ushindani katika uzalishaji, soko, mikopo, n.k. China kwa upande mwingine inatawaliwa na uchumi wa sekta ya umma, kwani njia kuu za uchumi zimeshikwa na serikali, hali inayomaanisha kuwa makampuni yake yanakuwa na uwezo usio wa kawaida katika kujijengea raslimali, kutengeneza na kuuza vitu nchi za nje.

Ushiriki wa serikali na taasisi kuu za fedha ambazo zinamilikiwa na serikali (yaani dola) zinavuruga uwezo wa kampuni ya nje kushindana, hivyo Marekani ambayo ndiyo nchi pekee duniani inayoweza kuikemea China, inaamua 'kufanya kweli.'

Ukiangalia kwa mfano ugomvi wa kukata na shoka kuhusu kushiriki kwa kampuni ya Huawei katika soko la simu nchini Marekani na kwingineko, unakuta wasiwasi huu kuwa kampuni hii ina uhusiano wa karibu na serikali ya China, hivyo inaweza kutumika kuhujumu (kutoa data za mawasiliano kati ya wateja wake).

Licha ya suala hilo kuchukua nafasi kubwa katika vyombo vya habari duniani, watu wengi waliona kuwa Huawei wanafanyiwa fitina, kuwa wasiwasi huo ni wa kubuni tu.

Mwanzilishi wa Huawei ni ofisa wa zamani wa Jeshi la Ukombozi la Watu wa China.

Ila kuna hitilafu ya kimfumo ukiangalia soko la simu ndani ya China, hasa simu za ngazi ya juu zinazopigiwa kelele (4G na 5G mpya zinazoanza sasa). Huawei inakamata asilimia 92 ya soko na kampuni nyingine asilimia nane.

Hivi ni kwa sababu kampuni kubwa ya Marekani na Ulaya kama Apple, Nokia au Siemens hazina uwezo wa kushindana, au ni mifumo isiyo rafiki na soko iliyowekwa kuhakikisha nafasi ya Huawei katika soko la China ni thabiti?

Sasa kama Huawei wamekamata asilimia 92 ya soko la simu nchini kwao, wapewe asilimia ngapi huko nje?

Ndiyo hapo unafikia kampeni ya utawala wa Marekani kwa nchi za Afrika ambako hivi karibuni (au labda katika mwaka mmoja uliopita) ulalamishi wa Marekani kuwa kampuni za China zinacheza 'fauli' katika soko la sekta tofauti (ujenzi, mawasiliano) barani Afrika.

Moja ya hoja za awali ni kuwa kampuni za China zilikuwa zinafumbia macho rushwa au yako tayari kutoa 'kitu kidogo' kutia saini mikataba ya ujenzi.

Hilo eneo lipo lakini kutokana na miradi ya China kusambaa kila mahali, ikafika mahali wanataka uhakikisho kimkataba, wasiingiliwe katika uendeshaji wa mradi husika.

Ndiyo ugomvi wa mikataba ya bandari za Mombasa na Bagamoyo. Hata hivyo, haitakuwa rahisi kwa Marekani 'kukoromea' uelekeo wa nchi za Afrika, kubadilisha jinsi zinavyoteua kampuni ya kupewa kandarasi, wapendelee kampuni ya Marekani na siyo ya China.

Ikumbukwe viwango vya faida na gharama za utaalamu au hatimiliki ya vifaa au raslimali ambazo kampuni za Marekani zitaingiza au kudai katika miradi ni tofauti na madai ya kampuni za China, na kwa Afrika bado ni soko kubwa la walaji maskini.

Marekani inaweza ikaingia katika baadhi ya maeneo tena kwa taabu tu. Haitakuwa rahisi kwa serikali za Afrika kusema tu 'acha China, chukua Marekani;' gharama za mradi na ulipaji deni unaweza kupanda hata mara mbili kama tahadhari hazichukuliwi, lakini baadhi ya wataalamu wa Idara ya Biashara ya Nje ya Marekani wanasema nchi hiyo inaweza ushindani Afrika.





# RC atengua uhamisho uliofanywa Tamisemi

**Na Nebart Msokwa**, KYELA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amebatilisha uhamisho wa Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Dk. Mariam Ngwere, ambaye Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (Tamisemi) ilimwandikia barua ya kumtaka ahamie katika Halmashauri ya Wanging'ombe mkoani Njombe.

Chalamila alitoa uamuzi huo jana wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kilichokuwa na ajenda ya kupitia na kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Kiongozi huyo wa mkoa aliweka wazi kuwa uhamisho wa mtumishi huyo wa umma una shaka.

"Mimi kama Mkuu wa Mkoa, siwezi kuwa laini kama mlenda, hivyo natamka kuwa kwangu mimi kuanzia muda huu, ninapozungumza, barua hiyo ya uhamisho wa DMO wa halmashauri hii ni batili," Chalamila alisema na kuongeza:

"Hakuna anayepinga uhamisho kwa sababu ni wajibu na ni haki ya mtumishi yeyote wa umma kufanya kazi mahali popote nchini, lakini hatukubali uhamisho wenye mashaka."

Chalamila alisema atawasiliana na Katibu Mkuu wa wizara husika kumshauri abatilishe uhamisho huo kwa kuwa amebaini una shaka na kwamba kama ni lazima ahamishwe kwenda eneo lingine, anapaswa apandishwe cheo kabla ya kuhamishwa.

"Kama kweli uhamisho huu hauna shaka ndani yake, basi inastahili mtumishi huyu apandishwe cheo ili iwe sababu ya yeye kuhamishwa na kwenda sehemu nyingine kulingana na cheo chake," Chalamila alisema.

Mkuu wa Mkoa huyo aliwataka madiwani na watumishi wa halmashauri hiyo wawe na umoja na kufanya kazi kwa ushirikiano ili waiongoze vizuri halmashauri yao na kuwaletea wananchi maendeleo.

Alisema halmashauri hiyo inakabiliwa na migogoro mingi ambayo baadhi yake inasababisha hata baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati na baadhi kutelekezwa.

Katika kikao hicho, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariamu Mtunguja, alieleza kushangazwa na uamuzi wa Halmashauri ya Kyela kukopa fedha kwenye mfuko wa amana kwa ajili ya uendeshaji wa Halmashauri na kuwaagiza waache utaratibu huo.

"Acheni utaratibu huo na mlipe fedha zote ambazo mmekopa, hizi fedha ni za watu wameziweka huko ili zifanye shughuli zao, lakini ninyi mnakopa kwa ajili ya uendeshaji, hapana hatuwezi kufika kwa mwendo huo," Mtunguja alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Dk. Hunter Mwakifuna, aliwaomba madiwani wa halmashauri hiyo kuungana na watendaji wa serikali katika kutekeleza majukumu ya ukusanyaji wa mapato.

Alisema halmashauri hiyo imepata hati ya kuridhisha na kwamba kwa sasa wataendelea kufanya kazi kwa bidii na kusimamia matumizi ili wapate hati safi.



Mmoja wa wanufaika wa mitaji kutoka Shirika la SOS Children's Village, Hashim Mhandu (aliyevaa koti jeusi), akielewana bei na mteja wa vikapu wakati wa maadhimisho ya miaka 70 ya kuanzishwa kwa shirika hilo yaliyofanyika Nyamagana, jijini Mwanza. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

## Polisi watoa neno hukumu majambazi jela miaka 30

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limewatahadharisha watu wanaojihusisha na ujambazi mkoani humo kuwa litaendelea kuwadhibiti na kuwachukulia hatua.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Ulrich Matei, baada ya watuhumiwa wawili wa ujambazi kuhukumiwa na Mahakama ya Wilaya ya Mbeya kutumikia kifungo cha miaka miaka 30 jela baada ya kuwatia hatiani kwa kosa la ujambazi.

Waliohukumiwa kutumikia kifungo hicho ni Richard Jackson (30) na David Mwashinani (32), wote wakazi wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Kamanda Matei alisema Novemba 28, mwaka jana, wawili hao walimvamia Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Kasumulu, Habib Moris, akiwa amelala nyumbani kwake maeneo ya Iwambi jijini Mbeya na kumcharanga mapanga kisha kuchukua mali zake.

Alisema taarifa za tukio zililifikia Jeshi la Polisi ambalo liliwasaka majambazi hao na kuwakamata wakiwa na baadhi ya mali za meneja huyo.

"Baada ya kuwakamata, tuliwafikisha mahakamani ambako kesi yao iliendeshwa na wanasheria wa serikali na kwa kuwa tuliwakamata na ushahidi wa kutosha, wametiwa hatiani na kuhukumiwa miaka 30 jela," Kamanda Matei alisema.

Aliishukuru Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali kwa kusimamia kesi hiyo vizuri na Mahakama ya Wilaya ya Mbeya kwa kutenda haki kwa kuwahukumu majambazi hao kwenda jela.

Kamanda Matei alitoa wito kwa watu wenye tabia ya kufanya ujambazi, kuacha mara moja tabia hiyo kwa kuwa Jeshi la Polisi liko makini na limejiandaa kukabilia na uhalifu wowote na kuchukua hatua.

"Wenye tabia za kihalifu hasa majambazi, nawashauri tu kwamba waache tabia hiyo maana tukiwakamata watafungwa kama walivyofungwa hawa majambazi," Kamanda Matei alisema.

# Shehena mbao 'haramu' kutengeneza madawati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHEHENA ya mbao ambazo zilikamatwa na Wakala wa Misitu (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zikiwa zimevunwa na majangili kwenye misitu ya asili wilayani Chunya mkoani Mbeya, imekabidhiwa kwa Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila ili zitumike kutengeneza madawati.

Mbao hizo 544 zilikabidhiwa kwa Mkuu wa Mkoa juzi na maofisa wa TFS wakiongozwa na Kaimu Meneja wa Kanda hiyo, Jane Kihwele, ambaye alisema wameamua zitumike kutengeneza madawati ili kupunguza tatizo la uhaba wa samani hizo shuleni.

Alisema mbao hizo zilikamatwa kwenye operesheni mbalimbali za kulinda misitu baada ya majangili waliokuwa wanazivuna kuzikimbia walipobaini wanafuatiliwa na maofisa wa wakala huo.

Kihwele alisema walizikusanya mbao hizo na kuzihifadhi mpaka walipopokea maombi ya Mkuu wa Mkoa akiomba zitumike kutengeneza madawati kwa ajili ya shule za serikali.

"Sisi tunaunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha sekta ya elimu ndiyo maana tuliamua kuwa mbao hizi ambazo wahalifu walikuwa wanazivuna kinyemela, zitumike kwenye utengenezaji wa madawati," Kihwele alisema.

Aliongeza kuwa wataendelea kushirikiana na serikali ya mkoa katika kulinda misitu yote iliyohifadhiwa na kuwadhibiti majangili wanaovamia misitu na kuvuna mbao, kuendesha shughuli za kilimo na uwindaji.

Ofisa wa TFS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Hamza Omary, alisema mbao hizo zina thamani ya Sh. milioni 10 na zilikamatwa katika vipindi tofauti kuanzia mwaka jana.

Aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na serikali katika shughuli za kulinda misitu kwa kutoa taarifa za watu wanaofanya shughuli za kibinadamu kwenye misitu bila vibali maalum vya kuwataka kufanya shughuli hizo.


Alisisitiza misitu ni muhimu kwenye maisha ya binadamu kwa kuwa inahifadhi vyanzo vya maji, kuvutia watalii hivyo kuingiza fedha za kigeni na kusaidia kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.

Akipokea mbao hizo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila, alisema ofisi yake iliziomba mbao hizo kwa ajili zitumike kutengeneza madawati kutokana na matarajio ya kuwa na ongezeko la wanafunzi wapya watakaoandikishwa darasa la kwanza mwakani.

Alisema kwa sasa, mkoa huo kama ilivyo kwa mikoa mingine, una upungufu wa idadi ya madawati ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi na kwamba ofisi yake inakabiliana na changamoto hiyo kwa njia mbalimbali.

Alisema wanakusudia kukiomba Chuo cha Ufundi Stadi (Veta) kutengeneza madawati kwa kutumia mbao hizo na wanaamini kitatengeneza madawati mengi na imara. "Tumeanza jitihada kubwa za kupambana na upungufu wa madawati, tunaunga juhudi za Rais wetu za kuboresha sekta ya elimu na sasa tunataka mpaka kufikia mwezi Januari mwakani, tusiwe na upungufu wa madawati," Chalamila alisema.

Mkuu wa Mkoa huyo aliishukuru TFS kwa kukubali ombi lake na kutoa mbao hizo na kuwaomba wadau wengine kuungana na serikali kukabiliana na changamoto ya madawati kwenye shule za umma.





# Wabunge wanolewa kuhusu mimba za utotoni

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WABUNGE wametakiwa kuhamasisha wazazi kutoa elimu ya stadi za maisha kwa watoto wao wa kike na kiume ili kujiepusha na mimba za utotoni.

Wito huo ulitolewa jana na Mratibu wa Muungano wa Utepe Mweupe wa Uzazi Salama Tanzania (Wratz), Rose Mlay, alipokuwa akiwasilisha mada ya athari za mimba za utotoni katika mkutano wa wabunge wa uzazi salama, jijini hapa.

Mlay alisema mimba za utotoni zimekuwa zinaathiri uchumi na kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa mwaka 2013 na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (Unfpa), takribani Dola za Kimarekani bilioni 5.22 zinapotea kutokana na watoto wanaokatiza masomo kwa ujauzito.

Alisema ni vyema wabunge wakatumia mikutano yao kwenye majimbo kuhamasisha jamii kukemea kitendo chochote kinachosababisha mimba hizo ikiwamo ubakaji, kurubuni watoto na ndoa za utotoni. "Wabunge hamasisheni pia walimu wawafundishe wanafunzi stadi za maisha wakatae kurubuniwa, wakatane kitu chochote kinachosababisha kubakwa. "Tunaomba katika mihadhara yenu wabunge muwahamasishe wazazi wazungumze na watoto wao wakiwa wadogo waseme 'Hapana' kwa yeyote anayewashika sehemu za siri," alisema.

Mlay pia aliwaomba wabunge kuzungumza na serikali kutilia mkazo Sheria ya Kumlinda Mtoto ya mwaka 2009 kuwa atakayempa mimba mtoto chini ya miaka 18 ni mhalifu na achukuliwe hatua za kisheria na wanaoficha ushahidi wachukuliwe hatua kisheria.

Kuhusu uzazi wa mpango, mratibu huyo aliwataka wabunge kuishauri serikali kuwekeza katika njia za kisasa za uzazi wa mpango.

"Wabunge katika mihadhara yenu hamasisheni wanandoa au wenzi watumie njia za kisasa za uzazi wa mpango ili wawe na nafasi ya miaka miwili hadi mitatu kati ya mtoto na mtoto kwa ajili ya afya ya mama, mtoto na maendeleo ya familia na ya nchi, badala ya mama kuzaa kila mwaka. Akipangilia atapata nafasi kulea watoto na kuchangia uchumi wa nchi," alisema.

Naye mwakilishi kutoka taasisi ya Options, Moke Magoma, alisema hadi kufikia mwaka 2023 kama mimba zisizotarajiwa zitazuiwa, zitaokoa Sh. bilioni 762.

Akichangia katika mkutano huo, Mbunge wa Iramba Magharibi, Mwigulu Nchemba, aliwataka wabunge kubadilisha fikra na mitazamo ya jamii kuanzia majimboni wanakotoka ili kukomesha mimba hizo.

"Mimi wakati nikiwa kijana nikiaga nyumbani baba akinisindikiza ananiambia mwanangu mimi bado kijana nina uwezo wa kulea ukienda huko ukipata wajukuu niletee nilee. Lakini mama yeye aliniambia niwe makini huko ninakokwenda kuna Ukimwi. Hivyo hivyo ndivyo hali ilivyo majimboni kwetu watu wana fikra tofauti," alisema Mwigulu.

Kwa upande wake, Mbunge wa Viti Maalum, Azza Hilary, alisema mila na desturi zinachangia sana uwepo wa ndoa za utotoni hivyo elimu zaidi inahitajika kwa jamii.

Alisema mzazi anaona mwanae akiolewa na asipoolewa yuko radhi aende kwa mganga wa kienyeji ili mtoto wake aweze kuolewa mapema.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa, akitoa maelekezo kwa mkandarasi M/S Superb Builders And General Supplires (hayupo pichani), anayejenga daraja la mfuto (drift) katika mto Nguyami linalounganisha kijiji cha Iyogwe na Gairo mkoani Morogoro. Daraja hilo linaunganisha Barabara ya Iyogwe-Chakwale-Ngilori yenye urefu wa kilomita 42. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kituo kipya mabasi Dodoma kama 'airport'

**Na Ibrahim Joseph**, DODOMA

MRADI wa ujenzi wa kituo kipya cha mabasi jijini Dodoma unatarajiwa kukamilika Septemba, mwaka huu, na utakuwa na huduma za kama za uwanja wa ndege.

Hayo yalielezwa jana na Mhandisi Idrisa Noorane alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mradi ujenzi wa kituo hicho kilichopo eneo la Nzuguni jijini hapa.

Noorane alisema mradi awamu ya kwanza unatarajiwa kukamilika Septemba, mwaka huu, na utakuwa na huduma kama zilivyo kwenye viwanja vya ndege maarufu.

"Hii stendi ni ya aina yake na itakuwa ya kwanza nchini kutokana na huduma zake zitakazokuwa zinapatikana humu. Ni tofauti kabisa na stendi zingine kwa sababu itakuwa sawa na uwanja wa ndege," alisema.

Alibainisha kuwa kituo hicho kitakuwa na sehemu za watu maalum (VIP) ambayo itakuwa na huduma za chakula na viburudisho na watakuwa wanategemea kwa huduma hizo.

Alizitaja baadhi ya huduma zitakazokuwapo ndani ya kituo hicho kuwa ni maduka makubwa, hoteli kubwa, sehemu kuu nne za kupumzikia abiria na wageni wengine wanaofika kupata huduma.

Aidha alisema jengo hilo lenye ghorofa moja litakuwa na njia tofauti kati ya abiria wanaosafiri na abiria wanaoingia ndani ya kituo hicho.

Aliongeza kuwa kituo hicho kitakuwa na mageti 20 yatakayotumika ndani pamoja na sehemu maalumu za kila basi kusimama kutokana na maelekezo ya waongoza kituo.

"Hatua za ujenzi wa kituo hichi upo katika hatua za mwisho kwa kumalizia sehemu ya paa na sehemu mbalimbali za ndani ya jengo hilo na baadhi ya vyumba vimeanza kupakwa rangi," alisema.

Mkurungenzi Mtendaji wa kampuni ya ujenzi ya Mohammed Builders Ltd, Mohammed Jaferj, alisema mradi huo unatekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza wataikabidhi Jiji la Dodoma Septemba na utekelezaji wa mwingine utafanyika kwa awamu kulingana na matakwa ya jiji.

Alisema kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kuhudumia mabasi 250 kwa wakati mmoja na sehemu moja ya kupumzikia itakuwa na uwezo wa kuhudumia watu 300 kwa wakati mmoja.

Pia alisema kampuni hiyo inatekeleza ujenzi wa miradi mikubwa mitatu jijini hapa ambayo mbali na kituo kikuu cha mabasi, mingine ni soko na mradi wa Chinangali na yote itagharimu Sh. bilioni 35.44.

# Takukuru yatoa somo Zimamoto

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) imelitaka Jeshi la Zimamoto na Ukoaji, kuzingatia viapo ili kujiepusha na vitendo vya rushwa vitakavyolitia aibu jeshi hilo.

Akizungumza jana katika kikao cha mwaka kilichojumuisha maofisa wa jeshi hilo kutoka mikoa mbalimbali nchini, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema askari akikamatwa kwa tuhuma za rushwa ni aibu kwa jeshi hilo kutokana na kazi anayoifanya katika jamii inayomzunguka.

Kibwengo alisema jeshi hilo lisipozingatia kiapo cha kazi, katika baadhi ya maeneo wanayofanyia kazi yanaweza kuwasababisha kufanya vitendo vya rushwa.

"Kwa mfano kwenye kuidhinisha ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto na uokoaji visivyokuwa na kiwango kinachokatiwa, kuandaa taarifa za ukaguzi ambazo si sahihi, kuidhinisha michoro ya ujenzi ambayo haijakidhi kiwango kinachotakiwa, mnatakiwa kuwa makini katika kazi zenu kwa sababu ni rahisi kuwasababishia vitendo vya rushwa," alisema Kibwengo.

Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, aliwataka makamanda wa mikoa wa jeshi hilo kukutana na makamanda wa Takukuru ili kupata elimu ya rushwa.

Alisema elimu ya rushwa ni jambo ambalo linatakiwa kuzingatiwa kila wakati kwa kuwa rushwa inaangamiza taifa kwa haraka.

Aliwatoa hofu wananchi utendaji wa jeshi hilo hautakwama baada ya kuimarisha vitengo vyake 11.

Andengenye alisema vitengo hivyo kwa sasa vimepata watendaji kazi ambao wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha jamii inapata huduma nzuri toka kwa jeshi hilo.

Naye, Naibu Kamishna wa Zimamoto na Ukoaji, Kennedy Komba ambaye ni Mkuu mpya wa Chuo cha Zimamoto kilichoko Kampasi ya Chogo mkoani

Tanga, alisema chuo hiko kinatarajia kutoa mafunzo kwa askari, maofisa na raia kwa ujumla ili kusaidia kutoa msaada wa majanga ya moto katika maeneo ambayo moto umetokea.




Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Lilian Mwalongo (katikati), akikabidhi moja ya boksi lenye msaada wa simu za mkononi 247 kwa Amina Njoka ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama Wamachinga, mkoani Arusha jana. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti, Iddi Hussein. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Balozi Njoolay ashauri hati za ardhi ziombewe mikopo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya uongozi ya Ofisi ya Mpango wa kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge (Mkurabita), Balozi mstaafu Daniel Ole Njoolay, amewataka wananchi waliokabidhiwa hati za ardhi kuzitumia vyema kwa ajili ya kuombea mikopo itakayowasaidia kupambana na umaskini wa kipato.

Balozi Njoolay alitoa wito huo katika hafla ya kuwakabidhi wananchi 54 wa Mpendae mjini Zanzibar hati hizo baada ya kukamilisha masharti ya usajili.

Alisema Serikali ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zimeazimia kuwakomboa wananchi wake na umaskini wa kipato kupitia njia mbalimbali ikiwamo kuwapatia hati za ardhi zitakazowasaidia katika harakati zao za kimaendeleo.

Aliwataka wananchi hao kuzitumia hati hizo ili kuomba mikopo kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwamo benki kwa ajili ya kuendeshea maisha yao.

"Wenzetu nje ya nchi hati hizi zinakuwapo katika benki huzitumia kikamilifu kuomba mikopo ya kuwasaidia kuendeleza miradi yao ya kimaendeleo ambayo wanaianzisha hivyo hapa Tanzania tunawajibu wa kuyaiga hayo," alieleza Balozi Njoolay.

Kwa upande wake Mratibu wa Mkurabita, Dk. Seraphia Mgembe, aliwaomba wananchi hao hasa wazee kuzitumia hati hizo ili kukamilisha ndoto zao walizoshindwa kuzifanya wakati wa ujana wao.

Alisema kabla ya kupata hati hizo kuna mambo mengine muhimu walishindwa kuyatekeleza kwa kukosa mikopo hivyo kupitia hati hizo wana uwezo wa kuzitumia kukamilisha ndoto zao.

Alisema ili mwananchi awe na uchumi mzuri kunahitajika mipango endelevu itakayomsaidia kupata mtaji wa kufikia maendeleo aliyojipangia.

"Inawezekana mmoja wenu alitamani kufanya mambo makubwa, lakini akashindwa kwa kukosa kielelezo cha hati ambacho kingemfanya kupata mkopo, hivyo kuanzia leo hata kama ni mzee fursa sasa unayo ya kukopa ukafanya mambo yako unayoamini bado ni muhimu," alishauri Dk. Seraphia.

Naye Mrajisi wa Ardhi Zanzibar, Dk. Abdul-Nasser Hikmany, aliwataka wananchi waliopatiwa hati hizo kuzitumia vyema ili zilete mabadiliko ya kiuchumi kwa kuzitumia kutafuta mitaji kutoka taasisi za kifedha nchini.

Alisema mwelekeo wao ni kuhakikisha maeneo yote Unguja na Pemba yanapimwa na wamiliki wake kupatiwa hati ambazo watazitumia kama rasilimali muhimu na kupunguza migogoro ya ardhi.

Mmoja wa waliokabidhiwa, Mmanga Omar, aliishukuru serikali kwa kutoa hati hizo ambazo zitakuwa kielelezo muhimu cha wao kupata misaada mbalimbali ya kujiendeleza na maisha.

Alisema ataitumia kama fursa muhimu ya kukopa benki ili kuwatengenezea mustakabali mwema watoto wake ikiwamo kuwasomesha na kuwafungulia biashara.

# Serikali kuyakarabati majengo ya kihistoria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, imesema wamejipanga kuhamasisha na kutangaza utalii wa ndani kwa kuyafanyia ukarabati mkubwa majengo ya kale yaliyobeba historia ya Zanzibar.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Chum Kombo, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Ahmada Yahya Abdul Wakil, aliyetaka kujua mikakati ya wizara katika kukuza utalii wa ndani.

Aliitaja mikakati hiyo ni kuendeleza maeneo ya historia ikiwamo majengo ya kale kama Kwa Bihole huko Unguja, na Mkamandume huko Pemba.

Vile vile, alisema maeneo ambayo yatafanyiwa ukarabati mkubwa ambayo yamebeba historia ya Zanzibar ni Mwinyimkuu huko Dunga, Wilaya ya Kati.

# Wakulima wahimizwa kulima mazao ya viungo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Viwanda imeanza kuwahimiza wakulima wa mazao ya viungo ikiwamo pilipili hoho ambazo soko lake nje ya nchi lipo la uhakika.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni, Shekhe Hamad Matar, aliyetaka kujua mikakati ya wizara katika kuimarisha kilimo cha mazao ya viungo kibiashara.

Hafidh alisema wameweka utaratibu mpya wa kilimo hicho kulimwa kwa kuyashirikisha makundi mbalimbali ya vijana vijijini.

"Wizara ya Biashara na Viwanda kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC), kuimarisha kilimo cha viungo cha pilipili hoho kwa kuvikusanya vikundi vya vijana vilivyopo vijijini Unguja na Pemba," alisema.

Alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa imebainika kwamba soko la biashara la viungo lipo la uhakika nje ya nchi zaidi katika nchi za Bara la Asia ikiwamo India na Falme za Kiarabu.

Kwa mfano aliyataja baadhi ya mazao ya viungo ambayo soko lake la uhakika ni mdalasini, uzile, pamoja na pilipili manga.

"Mazao haya ya viungo soko lake lipo nje ya nchi la uhakika na kazi ipo kwa wakulima vijijini kujipanga zaidi na kuona kilimo hicho kinaleta tija," alisema.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga na kuona kwamba inarudisha hadhi yake ya kuwa miongoni mwa visiwa vilivyokuwa vikiongoza katika uzalishaji wa mazao ya viungo duniani.

## Tigo yatoa simu 247, miavuli 100 kwa wamachinga

**Na Mwandishi Wetu**

KUPITIA Chama cha Wamachinga Mkoa wa Arusha, kampuni ya Tigo kitengo cha Tigo Business imetoa simu 247 na miavuli 100 kwa wateja wake ambao ni wanachama wa umoja huo wa wafanya biashara wadogo.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kuwakabidi vifaa hivyo kwa wateja hao 247 juzi, Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Lilian Mwalongo, alisema zawadi hizo ni utaratibu wa kawaida wa kampuni hiyo kuwazawadia na kuwashukuru wateja wake waliopo kwenye vikundi na unalenga kuboresha biashara zao pamoja na mazingira wanayofanyia kazi.

"Leo kampuni ya Tigo inayofuraha kukabidhi vifaa hivi kwa wateja wetu ambao ni wanachama wa Umoja wa Wamachinga hapa mkoani Arusha. Ni utaratibu wetu wa kawaida kuwapa zawadi wateja waaminifu kama hawa na tunaamini vifaa hivi vitawasaidia kuboresha biashara zao, huku wakifurahia huduma bora kutoka Tigo," alisema.

Lilian alifafanua kuwa, kampuni ya Tigo hutoa zawadi mbalimbali ikiwamo simu za mkononi kwa wateja wa malipo ya baada waliopo kwenye vikundi na ambao hutumia huduma za Tigo wakiwa na mkataba wa miezi 12 au 24.

"Ili mteja aweze kunufaika na zawadi hizi, anatakiwa kujiandikisha kama mteja wa walipo ya baada (postpaid) na ni lazima awe katika kikundi au kampuni kubwa au ndogo. Hivyo basi, tunakaribisha vikundi, kampuni pamoja na taasisi kwa ajili ya kupata huduma zetu nzuri na za uhakika za mawasiliano," alifafanua.

Meneja huyo pia aliwataka wanufaika wa zawadi hizo kuendelea kutumia mtandao wa Tigo na kuongeza kuwa Tigo inajali na kuwekeza kwa wateja na wabia wake wa biashara ili kuhakikisha kuwa Watanzania wote wawanufaika na huduma bora za mawasiliano.

# Mfumo kuwaondoa wapigadebe, mawakala ukataji tiketi mbioni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeandaa mfumo rasmi wa kielektroniki katika ukataji tiketi za abiria wa mabasi yanayofanya safari zake mikoani utakaowaondoa rasmi wapigadebe na mawakala wa mabasi nchini.

Aidha, mfumo huo utaanza kutumika kwa majaribio katika njia itakayoainishwa na utaanza kutumika nchi nzima Septemba mwaka huu na baadaye kwenye mabasi ya mjini (daladala).

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Kamwelwe alisema katika kuzishughulikia changamoto zilizopo katika sekta ya usafiri wa mabasi nchini, serikali kupitia Taasisi ya Udhibiti wa Usafiri Nchikavu (LATRA) na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Takwimu (NIDC) wameandaa mfumo huo ili kuzipatia majibu.

"Mfumo huo umetengenezwa ili kuboresha utoaji wa huduma za usafiri kwa abiria na kuwaondolea kero ya ulanguzi wa nauli ambao unafanyika katika mazingira ambayo siyo rasmi kutokana na kukosekana kwa taarifa sahihi," alisema Kamwelwe.

Alisema changamoto hizo huwaathiri watumiaji wa huduma hasa katika kipindi chenye mahitaji makubwa ya usafiri ambapo fedha nyingi za abiria huchukuliwa na mawakala au wapigadebe nje ya nauli halisi inayotakiwa.

Pia, alisema kwa kuzingatia mahitaji ya wadau mbalimbali, mfumo huo utakuwa na taarifa zote muhimu zinazoweza kutumiwa na taasisi mbalimbali kama vile LATRA, Polisi, Mamlaka ya Mapato (TRA), Uhamiaji, vyuo vya elimu ya juu na watafiti.

Alizitaja faida ambazo zitapatikana kutokana na kuwapo kwa mfumo huo ni kuondoa upotevu wa mapato kupitia mawakala na wapigadebe.

Alisema pia mfumo huo utawezesha kutunza hesabu na kuaminiwa na taasisi za fedha,kupunguza gharama za uendeshaji kwa kutumia Tehama, kuongeza uwekezaji na mapato kwenye sekta, kupata taarifa za mauzo na fedha kupitia simu ya mkononi au kompyuta.

Alisema kwa abiria na wananchi mfumo huo utawasaidia kukata tiketi wakiwa majumbani mwao au popote walipo na kuwapunguzia gharama za kwenda ofisi za watoa huduma na baadaye kurudi kwa ajili ya safari.

"Mfumo huu pia utaondoa kero ya uholela kwenye vituo vya mabasi na kufanya usafiri kuwa wa heshima, lakini pia utaondoa vitendo vya upandishaji holela wa nauli hasa kipindi cha uhitaji mkubwa wa huduma," alisema.

Kadhalika, mfumo huo utakuwa rahisi kutumiwa na wanachi wa aina zote kwa kununua tiketi kupitia simu za mkononi na kwa wale ambao hawana au wanaopandia njiani watapata tiketi zao kupitia mashine ndogo aina ya POS, ambazo zitakuwa kwenye mabasi na ofisini.

Waziri Kamwelwe aliwataka LATRA, kutoa elimu kwa wadau wote na umma kwa ujumla kuhusiana na mfumo.



Mafundi wakiendelea na kazi za awali za maandalizi ya ujenzi wa daraja jipya la Salender litakaloanzia eneo la Aga Khan Upanga hadi ufukwe wa Coco, Oysterbay, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Chuo cha ubaharia chapewa changamoto

**Na Dege Masoli,** TANGA

CHUO cha mafunzo ya ubaharia cha Dar es Salaam Martime Institute (DMI) kimetakiwa kwenda mbali zaidi kwa kuwa na mitaala maalumu ya kufundisha mabaharia ili wahitimu wake kukidhi haja na viwango vya kimataifa.

Kwa kufanya hivyo, imeelezwa kuwa wahitimu hao pia wataingia kwenye ushindani wa soko la dunia.

Ushauri huo ulitolewa na Meneja wa Usajiri, Ukaguzi na Udhibiti wa Vyombo vya Majini wa Shirika la Wakala wa Meli nchini (TASAC), Alfred Wariana, wakati wa warsha ya mabaharia na wanafunzi inayofanyika jijini hapa ikiwa ni sehemu ya sherehe za Siku ya Mabaharia Duniani inayoadhimisha kitaifa mkoani hapa. Wariana aliitaka DMI kuhakikisha wanaandaa mtaala wa kuwafundishia mabaharia ambao utakiwezesha kutoa wataalamu wenye viwango stahiki kwa kuzingatia uhitaji wa soko la dunia.

Akizungumzia kazi ya mamlaka hiyo, Wariana alisema ni pamoja na kuhakiki usalama wa vyombo majini kwa mujibu wa sheria kwa kufanya ukaguzi kabla ya chombo kuanza kazi na kujiridhisha viwango na sifa za wafanyakazi wanaotakiwa kuwamo melini.

Alisema kwa mujibu wa sheria, pamoja na mambo mengine, kigezo cha mmiliki wa chombo husika kuajiri asilimia 75 ya wafanyakazi kinazingatiwa hususani katika nafasi za ngazi ya chini ambazo hazihitaji utaalamu mkubwa.

Naye Kepteni Hilal Salimu akiwasilisha mada, alikieleza chuo hicho pekee Afrika Mashariki kilichoanzishwa miaka 42 iliyopita kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ya kiteknolojia na hali ya kiuchumi.

Salimu aliiomba serikali na taasisi kukisaidia chuo hicho kupata vyombo kwa ajiri ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi ambavyo vitawawezesha kufanya majaribio pamoja na kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa ngazi ya chini ambao hawana uwezo kugharamia masomo hayo.

Awali wakichangia mjadala baadhi ya washiriki wa warsha hiyo waliiomba serikali kufanya uwekezaji katika mazao ya baharini kama inavyofanya kwenye sekta mbalimbali nchini, na kwamba kufanya hivyo kutaongeza pato la taifa kwa maelezo kuwa bahari ndiyo eneo pekee lenye fursa ya kufanya uwekezaji mkubwa duniani.

# Polisi waamriwa kuondoa vitambi

**MEXICO CITY, Mexico**

MAOFISA wa polisi wanaotaka kujiunga na kikosi kipya cha ulinzi wa taifa nchini Mexico wamepewa kipindi cha miezi sita kupunguza uzito na kuondoa vitambi la sivyo watafutwa kazi.

Makamanda hao walipewa agizo hilo wakati wanaendelea na shughuli ya kukabiliana na wahamiaji haramu.

Maofisa 625 tayari wamefeli vigezo vya kiafya vya kujiunga na kikosi hicho kitakachohudumu katika mpaka wa Kaskazini na Kusini mwa nchi hiyo kwa miezi sita au zaidi, lilisema gazeti la El Financiero katika ripoti yake.

Lilisema maofisa ambao hawatafikia vigezo hivyo watalazimika kubakia katika vitengo vingine vya ulinzi wa taifa lakini pia wanakabiliwa na tishio la kufukuzwa kazi kwa sababu kuna mpango wa kuunganisha idara ya polisi na vitengo vingine vya ulinzi na usalama wakati wowote kuanzia sasa.

Taarifa hiyo ilifichuka baada ya kanda iliyorekodiwa yenye sauti ya Kamanda wa Polisi Raúl Ávila Ibarra, kuvuja na kupatikana na gazeti la El Universal, ambayo ofisa huyo wa ngazi ya juu alisikika akijaribu kuwashawishi maofisa wadogo kujiunga na kitengo kipya cha huduma ya uhamiaji huku akiwaelezea kuwa kitengo hicho kipya kinalipa vizuri kuliko cha polisi.

"Wengine wetu tulio na uzito mkubwa tuna hadi miezi sita kubuni mbinu ya kutimiza masharti tuliyopewa," Ávila Ibarra alisikika akisema.

El Financiero linasema kuwa maofisa wanaotoa maombi ya kazi wa kitengo kipya cha ulinzi wa taifa hawatakiwi kuwa na uzito mkubwa wala kutoboa sehemu yoyote ya miwili wala kuwa na tatuu ambayo itaonekana watakapovalia sare za kazi.

Uchunguzi uliofanywa na Shirika la Kitaifa la Takwimu na Jografia mwaka 2017 lilibaini kuwa asilimia 79 ya maofisa wa polisi walikuwa na uzito mkubwa kupita kiasi, ilinukuu ripoti ya gazeti la Mexico News.

**"Wengine wetu tulio na uzito mkubwa tuna hadi miezi sita kubuni mbinu ya kutimiza masharti tuliyopewa," Ávila Ibarra alisikika akisema.**

*BBC*

# Mbunge mtuhumiwa 'uchochezi' kuendelea kubaki rumande

**NAIROBI, Kenya**

MBUNGE wa Kenya aliyekamatwa kwa kutoa maneno ya chuki dhidi ya wafanyabiashara wa kigeni bungeni, ameendelea kusota rumande kwa siku ya pili wakati dhamana yake ikishughulikiwa.

Polisi walimfikisha Charles Njagua Kanyi maarufu 'Jaguar' mahakamani jana lakini hakusomewa mashtaka. Kwa mujibu wa mahakama, uchunguzi unafanyika kuhusu madai ya kupanga kuvamia mali za watu na kuwashambulia raia wa kigeni walio nchini Kenya.

Mwendesha mashtaka aliitaka mahakama kuendelea kumshikilia mshtakiwa kwa majuma mawili wakati wakimalizia uchunguzi wao. Mahakama itatoa uamuzi kuhusu ombi la dhamana ya Jaguar kesho.

Mbunge Kanyi alikamatwa juzi kwa madai kuwa alitoa kauli za kichochezi dhidi ya wafanyabiashara wa kigeni katika soko kuu la Gikomba nchini Kenya.

Alipokuwa akizungumza kuhusu kuwepo kwa ushindani wa kibiashara na wageni usio na usawa, alisema: "Wakenya ni sharti wafanye biashara zao bila kushindana na watu kutoka mataifa mengine. Raia wa Pakistan wametawala biashara za kuuza magari nchini humu, Watanzania na Waganda wanatawala katika masoko yetu. Tunasema imetosha iwapo hawatarajeshwa nyumbani katika saa 24 tutawashika na kuwapiga na hatuogopi mtu yeyote," alinukuliwa akisema.

Kauli hiyo iliibua hisia kali kwenye mitandao ya kijamii. Hisia hizo ziliibuka kufuatia matamshi aliyotoa mbunge huyo dhidi ya wageni wanaoendesha biashara nchini Kenya.

Katika mkanda wa video uliosambazwa nchini Kenya na katika nchi jirani ikiwamo Tanzania, mbunge huyo, alisema hawatokubali watu wa nje waje kuendesha biashara nchini kwao.

"...Ukiangalia soko letu, Watanzania na Waganda wamechukua biashara zetu, sasa sisi tumesema enough is enough," alisema mbunge huyo ambaye ni mwanamuziki, mwanasiasa na mjasiriamali tajiri nchini Kenya na katika eneo la Afrika Mashariki na moja ya nyimbo alizoimba ni 'Kigeugeu'. *BBC*




Polisi akiwa kwenye doria Mexico. **PICHA : BBC**

# Tatizo jipya lagundulika ndege ya Boeing Max 8

**WASHINGTON, Marekani**

WAKAGUZI wa ndege nchini Marekani wamegundua tatizo jipya katika ndege ya kampuni ya Boeing chapa 737 Max 8, ambalo huenda likachelewesha kurudisha huduma za ndege hiyo angani.

Utawala wa safari za anga nchini Marekani-Federal Aviation Administration (FAA) umesema umegundua kile kilichoitwa kuwa ni "inayowezekana kuwa hatari" wakati wa majaribio ya ndege hizo, lakini haukufichua matokeo wala hatari mpya.

Ndege hiyo (pichani) inayouzwa kama njugu kwa wateja mbalimbali wa kampuni ya Boeing ilisitishwa mnamo Machi baada ya ajali mbili za ndege, mojawapo ikitokea nchini Ethiopia. Kampuni hiyo inaimarisha mfumo wa kutua kwa ndege hiyo, ambao unachunguzwa na maofisa wa uchunguzi wa ajali ya ndege.

Katika ujumbe kwenye twitter, FAA ilisema: "Katika suala la hivi karibuni, FAA imetambua na kubaini hatari zinazowezekana kuwepo. FAA hivi karibuni liligundua hatari inayowezekana kuwepo ambayo ni lazima Boeing iitatue."

Mwezi uliopita, FAA liliashiria kuridhia mabadiliko ya Boeing kwa ndege hiyo ya 737 Max ambayo yanaweza kuidhinishwa mwishoni mwa mwezi huu. Hatua hiyo ingeruhusu ndege hizo kufanyiwa majaribio mapema mwezi ujao wa Julai.

Awali kulikuwa na matumaini kuwa ndege ya 737 Max itarudi angani wakati wa msimu wa joto, lakini mpangilio huo ulisukumwa mwishoni mwa mwezi huu hata kabla ya taarifa hiyo ya jana.

Reuters, shirika la habari ambalo lilitangulia kuripoti kuhusu tatizo hilo kwanza limesema kuwa wakati wa kufanyiwa majaribio kwa usukani ambao mfumo wa kutua uliidhinishwa, ilichukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa kupata udhibiti wa ndege hiyo.

Vyanzo vingine vinasema tatizo linahusiana na nguvu ya kompyuta ya ndege hiyo na huenda haukuwa na uwezo wa kupokea maagizo kwa kasi inayohitajika.

Boeing ilisema: "Tunashirikiana kwa karibu na FAA kuirudisha kuhudumu ndege ya Max " na kwamba tunaamini suluhu kwa mfumo huo utalitatua tatizo lililopo.

Iwapo wakaguzi hawatoridhishwa na suluhu hiyo kwa mfumo huo, itabidi ubadilishwe na huenda ikachelewesha muda wa kurudi kuhudumia kwa ndege hiyo zaidi ya ilivyodhaniwa hapo awali.

Ajali ya ndege ya Ethiopia ET302 mnamo Machi mwaka huu ni ajali ya pili iliyosababisha vifo vya watu kadhaa iliyohusisha ndege hizo zenye chapa ya 737 Max 8 katika muda wa miezi mitano.

Ndege inayokaribia kufanana na hiyo, inayomilikiwa na kampuni ya Indonesia Lion Air, ilianguka baharini kutoka Jakarta mnamo Oktoba 2018 na kuua abiria wote. Ripoti za awali katika ajali zote ziliashiria zilisababishwa na matatizo katika mfumo wa ndege kutua uliochelewa kufanya kazi kwa muda muafaka kutokana na hitilafu katika sensa yake.

*BBC*

# Bunge lafuta adhabu Sheria ya Takwimu

INATOKA UK. 2

yasiyo ya kiserikali (NGO'S) ili kumwezesha kuzuia shirika lisilo la kiserikali kutekeleza majukumu yake endapo shirika litakuwa linatekeleza majukumu yake kinyume cha sheria na kutathimini shughuli zinazotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali."

Hata hivyo, Mwanasheria Mkuu ameeleza kuwa kifungu kipya cha 4A kinampa Msajili mamlaka ya kufanya uchunguzi wa mwenendo wa shirika lolote lililo chini yake.

Pia, kila baada ya miaka 10, shirika lisilo la kiserikali litapaswa kuzingatia masharti ya kifungu cha 17 cha sheria hiyo ambacho kinaweka ukomo wa vyeti vya usajili na utaratibu wa kuhuisha vyeti hivyo.

**SHERIA YA TAKWIMU**

Katika marekebisho ya Sheria ya Takwimu (Sura ya 351) iliyosomwa Bungeni na Prof. Kilangi, yanaeleza kuwa marekebisho ya jumla yanayopendekezwa katika sheria hiyo yanalenga kubainisha dhahiri haki ya kuchapisha au kutoa taarifa za takwimu kwa umma.

Kwa maelezo ya Mwanasheria Mkuu huyo wa serikali, mapendekezo hayo yanakusudia kuanzisha Kamati ya Kitaalamu (Technical Committee) ambayo jukumu lake litakuwa kupokea kujadili malalamiko yanayotokana na wadau kuhusu usahihi wa takwimu zilizotolewa kwa umma. "Katika jedwali la marekebisho, inapendekezwa kufuta vifungu vya 24A na 24B na kuviandika upya, pia kuongeza vifungu vipya vya 24C, 24D, 24E na 24F kwa lengo la kuweka utaratibu wa kutoa matokeo ya takwimu zinazotofautiana na takwimu rasmi zilizotolewa na serikali," alisema Kilangi.

Kwa mujibu wa Mwanasheria Mkuu, marekebisho hayo yanatoa fursa kwa mtu yeyote kutoa takwimu zinazotofautiana na zilizotolewa na serikali, iwapo atakuwa amezingatia misingi ya kitakwimu iliyowekwa katika miongozo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa inayosimamia utoaji wa takwimu.

Lakini, sambamba na marekebisho hayo sheria hiyo inapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 37 (4) kinachotoa adhabu kwa mtu anayetoa taarifa za takwimu bila kupata kibali cha Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

**MABANDA YA VIDEO KURASIMISHWA**

Wakati anatoa maelezo yake kuhusu marekebisho ya Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (Sura ya 230), Prof. Kilangi alisema lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kwamba kumbi na vibanda vinavyotumika kuonyesha video vinapaswa kurasimishwa chini ya kifungu cha 10 cha sheria hiyo.

"Kwa mujibu wa kifungu kipya cha 6A, mtu au kampuni ya kigeni inayotaka kutumia eneo lolote la Tanzania kutengeneza filamu, itapaswa kuwasilisha nakala ya awali iliyotumika kutengeneza filamu husika, kubainisha maeneo ya Tanzania ambayo yametumika katika kuandaa filamu husika.

"Na pia kuwasilisha kwa Bodi ya Filamu nakala ya filamu iliyotengenezwa na kuruhusu filamu au kipande cha picha jongevu kutumiwa na Serikali ya Tanzania kutangaza maliasili na utalii, mila na tamaduni za Mtanzania."

**SHERIA YA VYAMA VYA KIJAMII**

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema katika Sheria ya Vyama vya Kijamii (Sura ya 337) marekebisho yanayofanywa hivi sasa, yanalenga kuondoa mkanganyiko kati ya Msajili wa Jumuiya za Kijamii na Taasisi zingine za usajili kama vile NGO's na Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (Brela).

Vile vile, marekebisho hayo yanayopendekezwa yanakusudia kuhuisha adhabu zilizopitwa na wakati ili ziweze kuendana na hali ya sasa.

Miswada mingine iliyosomwa bungeni na kujadiliwa na wabunge ni pamoja na Sheria ya Makampuni (Sura ya 212), Sheria ya Haki Miliki (Sura ya 218), Sheria ya Uwakala wa Meli (Sura ya 415) na Sheria ya Miunganisho ya Wadhamini (Sura ya 318).



Naibu Spika wa Bunge na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akiongoza semina ya kuwajengea uwezo awamu ya pili (LSP II), wajumbe wa tume ya utumishi wa Bunge, iliyofanyika katika Ofisi za Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

## Wabunge watofautiana mabadiliko sheria NGO

INATOKA UK. 2

ambao tupo humu ndani. Sasa kwa mazingira hayo tunawezaje kuepuka kuitwa sisi tumekuja kuidhinisha mapendekezo ya serikali na si kuyajadili?" Alihoji.

Naye Mbunge wa Malindi (CUF), Ally Saleh, alisema serikali inatakiwa ibadilike kwa jinsi ambavyo imekuwa ikiwasilisha miswada yake.

"Tumejadili sheria nane kwa siku mbili na kwa wadau mbalimbali kwa 'pressure' kubwa. Mtu akisema wapinzani wanapinga hatutendewi haki, tukiinuka hatupingi tunataka kutengeneza mazingira ili tusirudi hapa. Sheria hizi ziwe rafiki kwa wawekezaji. Serikali ibadilike katika kuwasilisha miswada yake," alisema.

Mbunge wa Madaba (CCM), Joseph Muhagama, alisema mashirika yasiyo ya kiserikali ni muhimu lakini akashangaa muswada wa marekebisho ya sheria hiyo kuleta kelele.

"Hii agenda ya NGO imeleta kelele nyingi sana. Naomba ieleweke kwamba mashirika yasiyo ya kiserikali ni muhimu yanatusaidia kufanya utafiti, yanachangia katika halmashauri na maendeleo makubwa huwezi kuondoa mchango wa NGO, wenzetu wasipeleke tofauti.

"Mchango ni mkubwa sana na baadhi ya wadau humu ndani tusiwapotoshe wananchi. Sheria hii inalenga kuziratibu na kujengea mazingira rahisi ya kufanya kazi sasa imechukuliwa tu upande mmoja kwamba zinatakiwa kufutwa. Mbunge huyo alishauri kuwe na kipindi cha kukagua ripoti za NGO tofauti na sasa ambapo hukaguliwa mwishoni mwa mwaka.

Emmanuel Mwakasaka (Tabora Mjini-CCM), aliunga mkono mabadiliko ya sheria kwenye sheria ya takwimu hasa kipengele cha adhabu kwa mtu anayetoa taarifa bila kupata kibali cha Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

"Wadau wengi waliokuja kwenye kamati yetu, walishindwa kufafanua ni nchi gani zinaachia mtu atoe tu takwimu. Sisi kamati tunaiunga mkono serikali kwa marekebisho kwani bila kudhibiti zitatuletea shida kubwa," alisema Mwakasaka ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Aidha, Mbunge wa Buyungu (CCM), Christopher Chizza, alisema NGO ni lazima ziwekewe sheria ya kuzisimamia kwa kuwa nyingi zimekuwa zikitumia fedha kwa makusudio tofauti na yale yaliyokusudiwa.

"Hizi NGO ni lazima ziwe na regulation (udhibiti) kama watu tu wanadhibitiwa, wao kwa nini wasidhibitiwe. Zipo NGO zinaingia mpaka vijijini zinajinasibu kwamba zinapeleka misaada, lakini mwisho wa siku fedha hazifiki. Ukija kutazama zimenufaishaje huoni," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Najma Giga, alisema lazima kuwe na uwazi katika taasisi ambazo zinaingiziwa fedha ikiwa ni pamoja na kufanya makusudio yaliyokusudiwa.

## Vigogo waliopenyeza majina ya ndugu jeshini kikaangoni

INATOKA UK. 2

majibu ya uongo atakamatwa, waliowashawishi kughushi watakamatwa, waliotengeneza vyeti bandia, waliohusika kuwaandikisha vijana hao bila kuwa na vigezo, viongozi wote waliohusika kupenyeza majina wa ndani na nje ya jeshi nao watachukuliwa hatua kupitia mamlaka zao husika," alisema.

Alisema hatua zitakazochukuliwa hazitaangalia wadhifa au cheo cha mtu kwa sababu lengo ni kusafisha nchi iwe na viongozi waadilifu na wanaofuata sheria na taratibu.

Alisema baadhi ya viongozi hao walikuwa wakipenyeza majina 10 hadi 20 ambapo hofu yao ni kwamba lengo lake ni nini katika taifa.

"Napenda kuwaeleza wale wanaojiunga na JKT, hii siyo tiketi ya kupata ajira serikalini au vyombo vya ulinzi, mimi mwenyewe sijaajiriwa, nimeandikishwa," alisema.

Ilonda alisema baadhi ya vijana hujiunga na JKT kwa lengo la kupata ajira mara wamalizapo mikataba yao ambapo dhana hiyo siyo sahihi.

"JKT kazi yake ni kuwajengea vijana uwezo wa uzalendo, kuwapatia stadi mbalimbali ili warudipo kwenye jamii waweze kujitegemea, baadhi ya vijana hulazimisha wapatiwe ajira na vyombo vya ulinzi na usalama," alisema.

Ilonda alisema wamebaini kuwa katika uandikishaji huo ambao unaendelea mikoa mbalimbali nchini, baadhi ya viongozi wanakwenda na orodha ya majina ya vijana ambao ni ndugu, jamaa na marafiki zao kuwaombea nafasi Makao Makuu ya JKT kinyume cha utaratibu.

Alisema wamebaini viongozi wa serikali na ndani ya jeshi hilo wakihusika katika ukiukaji wa taratibu wa uandikishaji.

Ilonda alisema wamebaini kuwa baada ya nafasi kugawiwa kwa uwiano katika mikoa Tanzania Bara na Visiwani na sifa zilizoainishwa, baadhi ya vijana wamekuwa wakienda kwenye mikoa mingine kujiandikisha kinyume cha taratibu.

"Tumebaini vijana wengi wametoa taarifa za uongo ili kujipatia nafasi na wengine kufanya vitendo viovu vya kushawishi na kujaribu kutoa rushwa na hatimaye kughushi vyeti vya kuzaliwa na vya elimu," alisema.

Alisema wamebaini kuwapo kwa utapeli katika uandikishaji huo kupitia baadhi ya watu wasio waaminifu ambao wamekuwa wakiwarubuni vijana na wazazi na kuwataka watoe fedha ili waweze kuwaingiza vijana wao JKT.

Pia, alisema tatizo lingine walilolibaini ni baadhi ya wazazi na vijana kupuuza taratibu zilizowekwa na kusisitiza wachukuliwe nje ya utaratibu au wakiwa na mapungufu katika sifa zilizotajwa kama vile elimu, umri na afya.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

## NAFASI ZA KAZI


**TANZANO LA KAZI,** Mtu wa IT diploma anahitajika na Mesenger form four au six. Mawasiliano: justinatemba22@gmail.com, 0715 885533


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**



## KUPOTEA KWA CHETI



115297602

**Juma Julius Shabani** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.2303-0120** kilichotolewa Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Nyiendo . Yeyote atakaekiona ataoe taarifa kituo chochocte cha Polisi.
Polisi Taarifa: **TAN/RB/6642/2016**


## CHETI KIMEPOTEA



115298302

**ZAINA SALINGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1603/0086** kilichotolewa na **NYOLOLO SEKONDARI mwaka 2007.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAR/RB/2541/2012.**

## CHETI KIMEPOTEA



115298402

**RAMADHAN ABDUL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0320-0288** kilichotolewa na **KIGOMA SEKONDARI SCHOOL CENTRE** October, 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBE/MBE/RB/86058/2019.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;135/2019**

**Ombi la SARAH ALLAN KUSHOKA**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi**
**marehemu ALLAN MARKO KUSHOKA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 26/06/2019.

115298902

## BIDVEST INTERNATIONAL COMPANY LIMITED


**Reg No. 134081**

Bodi ya wakurugugenzi kwa pamoja na wamiliki wakampuni ya BIDVEST INTERNATIONAL COMPANY LIMITED wameamua kufunga kampuni yao baada ya kuendeshwa kwa hasara. Kwa Taasisi au mtu yeyete mwenye madai na kampuni hii awasiliane na mmoja kati ya wanahisa wa kampuni ya BIDVEST INTERNATIONAL COMPANY LIMITED .

**P.O.BOX**
**DAR ES SALAAM**
**29TH November, 2018**
**AFISA MTENDAJI MKUUWAKALA**
**USAJILI WA BISHARA NA LESENI (BRELA)**
**S.L.P. 9393**

215298702

## KUPOTEA KWA VYETI



115297502

**Alex Jumanne** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1589-0009** kilichotolewana Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2005 katika shule ya **Sekondari Mwanza Baptist.** Na cheti cha kuzaliwa na Secondary living certificate Yeyote atakaviona ataoe taarifa kituo chochocte cha Polisi.
Polisi Taarifa: **MWA/RB/4349/09**

## KUPOTEA KWA CHETI



115298202

**Restituta Cosmas** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0772/0030** kilichotolewana Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2005 katika shule ya Sekondari Isevya mkoani Tabora. Yeyote atakaekiona ataoe taarifa kituo chochocte cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/KIJ/RB/88191/2019**

## KUPOTEA KWA KADI

**Emmilian Herman Riwa** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa namba **T309 ALX aina ya NISSAN PICK-UP,** Yenye chasis namba **SMD21001016.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Control Namba: **991088443959**

115298102

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Audax Allex William** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye usajili wa namba **MC 300 BEM** aina ya **BOXER BM150,** Yenye chasis namba **MDZAZIBZ4DWK49866.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Control Namba: **991088444168**

115298002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HASSAN ABASS MWINYIJUMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.900 CAK** AINA YA MITSUBISHI CENTA RANGI NYEUPE. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **MBE/RB/89275/2019.**

115299302

## KUPOTEA KWA CHETI



115297902

**Kibola Adam** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0342-0556** kilichotolewana Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2000 katika shule ya **Sekondari Shaaban Robert.** Yeyote atakaekiona ataoe taarifa kituo chochocte cha Polisi.
Polisi Taarifa: **KW/RB/241/019**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRANCIS RWAHAMA NYARALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 755 DKW TOYOTA MARK X.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. ***Control No. 1927421.***

115298802


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# DE LIGT KUJIFUNGA JUVE MIAKA MITANO

**TURIN, Italia**

JUVENTUS inakaribia kuinasa saini ya Matthijs de Ligt kutoka Ajax, kwa mkataba wa miaka mtano hapo kwenye viunga vya Turin.

Baada ya miezi mingi ya uvumi kuhusu hatima yake, De Ligt aliamua wapi anakwenda kucheza msimu ujao na kuzitosa klabu za Barcelona, Paris Saint-Germain na Manchester United ambazo zilikuwa kweye mbio moja ya kuwania saini ya nyota huyo wa Uholanzi.

Lakini habari zilizothibitishwa na Goal.com, De Ligt ambaye ni beki wa kati anajiunga na Juventus kwa dili ambalo ada yake ni euro milioni 70.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, atasaini mkataba wa muda mrefu wa kukaa na Bianconeri hao na mshahara wake utakuwa euro milioni 12 kwa msimu baada ya kukatwa kodi.

Na kwa mujibu wa wakala wake, Mino Raiola mkataba wa De Ligt una kipengele cha kumuuza kwa euro milioni 150 iwapo ataondoka hapo Juventus.

Hadi sasa rekodi ya usajili ghali kwa beki bado anaishikilia Virgil van Dijk ambaye ni Mholanzi mwenzake na De Ligt na wanayecheza naye timu ya Taifa, ambaye alijiunga na Liverpool kwa pauni milioni 84.5 Januari mwaka jana akitokea Liverpool.

De Ligt atawasili Italia huku akiwa na matumaini makubwa ya kuwa kwenye kikosi cha kwanza hasa baada ya kuwasaidia Ajax kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

## MAHREZ, MKEWE WATAKIWA KUMLIPA YAYA WALIOMTOSA

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Klabu ya Manchester City na Algeria, Riyad Mahrez pamoja na mkewe, Rita wameamriwa kulipa zaidi ya pauni 3,600 kama mshahara ambao hawakumlipa mfanyakazi wao wa ndani wa zamani maarufu kama yaya.

Wanandoa hao walimkata fedha hizo mwanamke huyo ambaye jina lake ni Catalina Miraflores bila idhini yake, lakini sasa jaji wa mahakama ya ajira ya hapa Manchester amewaamuru kumlipa.

Pia wameagizwa kulipa zaidi ya dola 150 kama fidia ya hasara aliyopata dada huyo baada ya kutomlipa fedha hizo.

Miraflores aliliambia Gazeti la The Sun kuwa: "Nilifanya kazi kwa bidii kulipwa fedha hizo."

Man City ilivunja rekodi yake kwa kumsainisha winga huyo mwenye umri wa miaka 28 kwa dau la pauni milioni 60 kutoka Klabu ya Leicester mwaka 2018.

Alikuwa miongoni mwa wachezaji wa kikosi cha Man City kilichoshinda mataji matatu ya nchini England.

The Sun liliripoti kwamba Miraflores aliajiriwa mwaka 2018 na mchezaji huyo ambaye analipwa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki - ili kuwaangalia watoto wake wawili wa kike.

Katika uamuzi uliochapishwa, Jaji John Sherrat alisema: "Watuhumiwa walikata mshahara wa mfanyakazi huyo na sasa wanaagizwa kulipa pauni 3,612. Kwa kukiuka mkataba wa mfanyakazi huyo, walishinda kutomlipa gharama ya mlalamikaji na sasa wameagizwa kumlipa pamoja na fidia ya pauni 150."

Awali madai ya kufutwa kazi kwa uonevu yaliowasilishwa na Miraflores kwake yalikataliwa na ndipo alipoamua kwenda mahakama ya kazi kwa ajili ya kupata haki yake.

# Man City kumnasa Rodri kwa pauni milioni 63

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City ina matumaini ya kukamilisha usajili wa kiungo wa Atletico Madrid, Rodri Hernandez wiki ijayo, kwa mujibu wa ESPN FC.

Bayern Munich nayo ilikuwa kwenye harakati za kumwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, lakini ni wazi kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania safari yake ni pale Man City.

Kama usajili wake utakamilika na kutua pale kwenye dimba la Etihad, maana yake ni kwamba atakuwa ameweka rekodi ya usajili kwa bei kubwa zaidi kwenye hitoria ya kikosi hicho chini ya kocha, Pep Guardiola.

City watalipa kiasi cha pauni milioni 63 kwa Atletico ili kumwachia mchezaji huyo kutua kwao.

Kwa sasa ndani ya Man City mchezaji anayeshikilia rekodi ya kusaini kwa fedha nyingi ni Riyad Mahrez ambaye ada yake ilikuwa ni pauni milioni 60 wakati akitua hapo akitokea Leicester City.

Aprili mwaka huu, ESPN FC iliripoti kwamba Rodri ndiye alikuwa mchezaji wa kwanza anayewaniwa na Guardiola katika usajili wa kipindi hiki cha majira ya joto.

Rodri anatajwa kwamba atakuwa mrithi wa kiungo, Fernandinho, ambaye mwezi uliopita alitimiza umri wa miaka 34.



HABARI MICHEZO

# LUKAKU

## SAFARI KUTUA INTER MILAN YAKARIBIA



**MILAN, Italia**

Inter Milan inaandaa pauni milioni tisa kwa ajili ya kutoa ofa ya kuipata saini ya mshambuliaji wa Manchester United, Romelu Lukaku kwa mkataba wa mkopo wa miaka miwili.

Dili hilo pia litahusu ruksa ya kumnunua Mbelgiji huyo jumla kwa kiasi cha pauni milioni 54.

Wakala wa Lukaku, Federico Pastorello Jumanne alikuwa Milan kwa mazungumzo na Inter, ambayo itakuwa huru kuipata saini yake Juni 30, mwaka huu wakati watakapoachiwa na Uefa kufuatia makubaliano yaliyowekewa kuhusu kusajili kulingana na mapato ya klabu (FFP).

Wakati alipoulizwa endapo Inter walikuwa wakijaribu kuipata saini ya Lukaku majira haya ya joto, Pastorello alisema: "Ndiyo, ametangaza hadharani mipango na matamanio yake. Tutaona nini kitatokea.

"Lukaku ni ndoto, mmoja ambaye ni mgumu kuweza kufanikisha hilo, lakini ninaamini hakuna linaloshindikana. Sio haiwezekani na Inter inajaribu sana."

Kocha wa Inter, Antonio Conte alijaribu kumnunua Lukaku mwaka 2017 wakati akiwa anainoa Chelsea lakini mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alichagua kujiunga na United badala yake.

Lukaku alihamia Old Trafford kwa ada ya awali kiasi cha pauni milioni 75 akitokea Everton na alifunga mabao 42 katika mechi 96 alizocheza.

## BARCELONA SASA YAAMUA KUMFUNGIA KAZI NEYMAR

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imetuma ofa yake ya kwanza kwa ajili ya kumrudisha nyota wake Neymar kwenye dimba la Camp Nou kipindi hiki cha majira ya joto, baada ya rais wa klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu kufanya mazungumzo na PSG.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alihamia jijini Paris kwa ada iliyoweka rekodi miaka miwili iliyopita, yenye thamani ya euro milioni 222- lakini mambo yalikwenda tofauti na yalivyotarajiwa.

Neymar amekumbwa na majeraha ya mara kwa mara na kushindwa kucheza kila wiki kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, huku PSG ikishindwa kupata mafanikio kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya mambo yote hayo, sasa Neymar ameona njia pekee ni kurudi kwa miamba wa Catalunya ambako alicheza kwa mafanikio makubwa.

Gazeti la AS la nchini Hispania limedai kwamba, Rais wa Barca, Bartomeu amefanya mawasiliano kwa mara ya kwanza kwa ajili ya uwezekano wa kukamilisha usajili huo.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, Blaugrana hao watalazimika kuvunja rekodi ya usajili ya euro milioni 222 ili kukamilisha usajili huo, huku taarifa nyingine zikisema kwamba, usajili huo unaweza kumhusisha Philippe Coutinho au Ousmane Dembele, ambao wamekuwa kwenye wakati mgumu wa viwango vyao kupanda na kushuka.

Aidha, taarifa zaidi zinaeleza kwamba, klabu hiyo imeshafanya makubaliano binafsi na Neymar na kwamba atarudi hapo na kutia saini ya mkataba wa miaka mitano kucheza hapo Nou Camp.

# Benfica yaifikiria ofa ya Atletico kwa Felix

**LISBON, Ureno**

BENFICA imeripotiwa kwamba inaizingatia ofa ya euro milioni 126 waliyopewa na Atletico Madrid kwa ajili ya kumuuza mshambuliaji wa kimataifa wa Ureno, Joao Felix.

Ofa hiyo imeizidi ile iliyoweka kwenye kipengele cha mkataba wake wa kumuuza nyota huyo mwenye umri wa miaka 19 ya euro milioni 120, lakini klabu hiyo ya La Liga inataka kulipa kwa mafungu.

Usajili wa Felix utakuwa wa tano kuwa ghali zaidi katika historia ya soka duniani nyuma ya Neymar, Kylian Mbappe, Philippe Coutinho na Ousmane Dembele.

Alianza kuichezea timu ya wakubwa Agosti na msimu uliopita alifunga mabao 15.

Felix pia atakuwa mchezaji wa pili




kijana ghali zaidi baada ya Mbappe ambaye alisajiliwa kwa euro milioni 180 kutoka Monaco kwenda Paris St-Germain mwaka 2018.

"Atletico Madrid imetuma ofa kwa Felix ya euro milioni 126 ambayo imeainishwa," ilisema taarifa ya Benfica.

Mchezaji huyo wa zamani wa timu ya vijana ya Porto FC, alianza kuichezea timu yake ya Taifa ya Ureno dhidi ya Uswisi kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mataifa ya Uefa mwezi uliopita.

Alifunga mabao matatu 'hat-trick' dhidi ya Eintracht Frankfurt kwenye mchezo wa Ligi ya Europa Aprili, na kuwa mchezaji kijana zaidi wa Benfica na Ureno kufunga mabao matatu Ulaya na mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga idadi hiyo ya mabao kwenye mchezo mmpoja katika Ligi ya Europa.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ZAHA AITAKA ARSENAL, AUBA, TORREIRA SOKONI?

Tatizo kubwa kwa Gunners ni bajeti yao ya pauni milioni 45, wakati Palace wakitaka pauni milioni 80 ili...

**LONDON, England**

WINGA wa Crystal Palace, Wilfried Zaha anataka kujiunga na Arsenal majira haya ya joto, lakini suala la bajeti ndilo linaloelezwa kuwa kikwazo kwa miamba hiyo ya Emirates kuweza kumpata hususan wakati huu klabu hiyo ikiwa imetenga kiasi cha pauni milioni 45 tu za usajili, kwa mujibu wa BBC.

Hata hivyo, Arsenal inaweza kulazimika kumuuza mshambuliaji wake, Pierre-Emerick Aubameyang ili kupata fedha za kumsajili Zaha ambaye Palace inaaminika kuhitaji pauni milioni 80 ili kumwachia.

Lakini hazina yao nyingine muhimu, kiungo wa kimataifa wa Uruguay, Lucas Torreira, aliyetua Emirates majira ya joto yaliyopita akitokea Sampdoria na ambaye amekuwa akihusishwa na kurudi Italia, anaweza kuwa mchezaji mwingine wa kupelekwa sokoni ili kuwezesha fedha za kuipata saini ya Zaha.

Kocha Unai Emery amekuwa akivutiwa zaidi na nyota huyo wa Palace baada ya kuwa na msimu mwingine wa kuvutia zaidi kwenye Ligi Kuu ya England, lakini kushindwa kwao kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, kunaweza kuwa kikwazo cha kuipata saini ya nyota huyo.

Ikiwa imefuzu kwa msimu wa tatu mfululizo kucheza kwenye Ligi ya Europa, bajeti ya usajili ya Arsenal kwa kipindi hiki cha majira ya joto ni pauni milioni 45, ambazo haizitatosha kumsainisha Zaha.

Kwa mujibu wa BBC, Arsenal walikuwa wanajiamini kupata fedha kwa ajili ya kumsajili Zaha kama wangefuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, wangeshinda Kombe la Ligi ya Europa katika fainali dhidi ya Chelsea.

Lakini sasa 'Washika Bunduki' hao watalazimika kutafuta fedha zaidi kama wanataka kumnunua mchezaji huyo wa Palace mwenye umri wa miaka 26.

Na ripoti zinadai kwamba, sasa Arsenal inaangalia uwezekano wa kumuuza mshambuliaji wake wa kimataifa wa Gabon, Aubameyang ama Torreira ili kupata fedha za kufanya usajili wa wachezaji.

Hata hivyo, linaweza kuwa pigo kubwa kwa Arsenal kama wakimuuza mfungaji huyo bora wa Ligi Kuu ya England msimu uliopita. Aubameyang alifunga mabao 22 msimu uliopita na kuibuka kuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu ya England pamoja na nyota wa Liverpool, Mohamed Salah na Sadio Mane ambapo wote walifunga idadi kama hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, alijiunga na Arsenal akitokea Borussia Dortmund ya Ujerumani, Januari mwaka 2018 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 56 na tangu kutua kwake kwenye dimba la Emirates amekuwa na kipindi cha kuvutia.

## KWA UFUPI

**UNITED YAJIONDOA KWA MAGUIRE**
Manchester United imejiweka kando katika mbio za kuipata saini ya beki wa Leicester City na England, Harry Maguire, 26, baada ya kuelezwa mchezaji huyo ataigharimu pauni milioni 100. ***(Mirror)***

**VIEIRA, GERRARD WATAJWA NEWCASTLE**
KOCHA wa Nice, Patrick Vieira, 43, kocha Rangers, Steven Gerrard, 39, na kocha msaidizi wa Manchester City, Mikel Arteta, 37, wote wapo katika orodha ya wanaotakiwa kwenda kurithi mikoba ya Rafa Benitez pale Newcastle. ***(Telegraph)***

**ARTETA KUMRITHI GUARDIOLA CITY**
MHISPANIA Mikel Arteta, 37, anaandaliwa kuinoa Manchester City wakati Pep Guardiola atakapoachana na klabu hiyo. ***(Evening Standard)***

**UNITED KASI ZAIDI KWA FERNANDES**
Manchester United itakutana na wakala wa kiungo Mreno, Bruno Fernandes, 24, kujaribu kukamilisha dili la kuinasa saini yake mchezaji huyo wa Sporting Lisbon kwa pauni milioni 70. ***(O Jogo, via Talksport)***

**POGBA AIPELEKA JUVE ADIDAS**
Juventus imeomba msaada wa kifedha Adidas ili kuweza kuipata saini ya kiungo wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba, 26. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

**TORREIRA AIKANA MILAN**
KIUNGO wa Arsenal na Uruguay, Lucas Torreira, 23, amesema AC Milan haijafanya mawasiliano naye kuhusu kumrejesha Serie A. ***(Talksport)***

**DEMBELE AWINDWA BAYERN**
Bayern Munich imefanya mazungumzo na Barcelona na wakala wa mshambuliaji Mfaransa Ousmane Dembele, 22, kuhusu uwezekano wa kujiunga na klabu hiyo. ***(Mirror)***

**PSG YAMFUATA DONNARUMMA MILAN**
PSG imefungua mazungumzo na AC Milan kuhusu uwezekano wa dili la pauni milioni 46 la kuipata huduma ya kipa Mtaliano Gianluigi Donnarumma, 20. ***(Mail)***

**SMITH LULU CELTIC, STOKE**
BEKI wa Huddersfield Town, Muingereza Tommy Smith, 27, anatakiwa na wapinzani wao wa Championship, Stoke City na mabingwa wa Scotland, Celtic. ***(Huddersfield Examiner)***

**GALENO AIVUTIA READING**
Reading inavutiwa kuipata huduma ya winga Mbrazil Wenderson Galeno, 21, kwa mkopo kutoka Porto. ***(Futebol365)***

**DERBY YAMKANA GERRARD**
MWENYEKITI wa Derby County, Mel Morris ameelezea kuwa taarifa zinazoihusisha klabu hiyo na kocha wa Rangers, Steven Gerrard ni "upuuzi kabisa". Kocha wa Derby, Frank Lampard ameruhusiwa kufanya mazungumzo na Chelsea. ***(Derby Telegraph)***

**FOSU KUTUA OXFORD UNITED**
WINGA wa Charlton Athletic, mzaliwa wa London, Tariqe Fosu, 23, amekubali kujiunga na miamba ya League One, Oxford United. ***(South London Press)***



# KMC YAANGUKIA KWA TP MAZEMBE KAGAME CUP

**Na Mwandishi Wetu**

KMC imeangukia kundi la kifo kwenye michuano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame inayotarajiwa kuanza kufurukuta jijini Kigali, Rwanda kuanzia Julai 6 hadi 21, mwaka huu, kufuatia kupangwa Kundi A pamoja na TP Mazembe ya DR Congo, imefahamika.

Kwa mujibu wa ratiba ya michuano hiyo iliyotolewa jana na Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), Nicholas Musonye, inaonyesha michuano hiyo itapigwa katika viwanja vitatu, Uwanja wa Kigali, Huye na Umuganda, ambapo KMC ya Tanzania ipo Kundi A pamoja TP Mazembe (DR Congo), Atlabara (Sudan Kusini) na wenyeji Rayon Sports ya Rwanda.

Mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Azam FC ya Tanzania wapo Kundi B pamoja na Bandari FC (Kenya), KCC (Uganda) na wenyeji Mukura Victory ya Rwanda.

Kundi C linaundwa na wenyeji wengine, APR ya Rwanda, Green Eagles (Zambia), Heegan (Somalia) na Proline (Uganda), wakati Kundi D likiwa na Gor Mahia ya Kenya, DCMP (DR Congo), KMKM (Zanzibar) na AS Ports ya Djibouti. Michuano hiyo itafunguliwa kwa mechi mbili ambapo APR watavaana na Proline Julai 6, mwaka huu majira ya saa 10:00 jioni katika mchezo utakaopigwa Uwanja wa Kigali ukitanguliwa na ule wa Heegan dhidi ya Green Eagles utakaopigwa dimbani hapo saa saba mchana.

Wawakilishi wa Tanzania katika michuano hiyo, KMC na Azam FC wataanza kuipeperusha bendera ya nchi Julai 7 kwa kuvaana na Atlabara na Mukura Victory katika Uwanja wa Huye na ule wa Kigali, wakati kesho yake KMKM ikishuka dimba la Umuganda kuivaa AS Ports. Kibarua kigumu kwa KMC katika michuano hiyo kitakuwa Julai 9, itakaposhuka Uwanja wa Kigali kuivaa TP Mazembe katika mechi yake ya Kundi A.

Katika taarifa hiyo, Musonye alisema: "Tumeamua kuandaa mashindano ya kuaminika ambayo yatakumbuka kwa miaka mingi ijayo. Shukrani nyingi kwa Rais Paul Kagame na watu wa Rwanda kwa kujitoa kwao kuwezesha Cecafa kuandaa tukio hili kubwa."

## WANAUME WA KAZI...



Baadhi ya wachezaji wa kikosi cha Taifa Stars wakiwa mazoezini katika Uwanja wa Petrosport jijini Cairo, Misri juzi kabla ya jana kuivaa Harambee Stars kwenye mechi yao ya pili ya Kundi C ya michuano ya Afcon 2019. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Misri, Nigeria zatangulia 16-Bora Afcon

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

USHINDI wa mabao 2-0 walioupata wenyeji Misri (Mafarao) dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) umewapa tiketi ya kutinga hatua ya 16-bora ya michuano ya Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019 inayoendelea nchini hapa.

Mabao hayo yalifungwa na Ahmed El Muhammad na Mohammed Salah na kuifanya Misri ifikishe pointi sita na kuongoza Kundi A, huku ikizima ndoto za DRC kusonga mbele katika mashindano hayo.

Kwa ushindi huo, Misri imekuwa timu ya pili kutinga hatua hiyo baada ya Nigeria iliyokuwa ya kwanza kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya kikosi cha Guinea, katika mechi iliyotangulia juzi usiku.

Bao pekee la Nigeria maarufu Super Eagles, katika mchezo huo lilifungwa na beki, Keneth Omeruo ambaye anacheza soka la kulipwa nchini Hispania.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Omeruo, alisema wanajisikia furaha sana kupata nafasi ya kusonga mbele katika fainali hizo huku wakiwa na mchezo mmoja mkononi.

Omeruo alisema watahakikisha pia wanapata matokeo mazuri katika mechi yao ya mwisho ya hatua ya makundi dhidi ya Madagascar na kuwapa furaha zaidi mashabiki wao waliopo jijini hapa na nyumbani kwao Nigeria.

"Najisikia furaha sana, kwangu binafsi na timu nzima, tulicheza kwa bidii kubwa licha ya changamoto ya hali ya hewa, naishukuru pia familia yangu, mke wangu na mtoto wangu kwa mafanikio niliyopata katika mechi hii," alisema Omureo ambaye alikuwa mchezaji bora wa mchezo huo dhidi ya Guinea.

Fainali hizi zinaendelea tena leo kwa mchezo kati ya Tunisia dhidi ya Mali wakati Morocco wataikabili Ivory Coast na Afrika Kusini watavaana na Namibia.

Cameroon ndio mabingwa watetezi wa fainali hizi zinazoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika, Caf.

## Mayanga kuanza na Kagame KMC

**Na Shufaa Lyimo**

HUKU timu yake ikiwa imepangwa Kundi A linaloaminika kuwa la 'kifo' kwenye michuano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati (Kagame Cup) kutokana na kuundwa na timu imara, kocha mpya wa Klabu ya KMC FC, Mganda Jackson Mayanja ameahidi kuifikisha mbali timu hiyo katika mashindano hayo na kwenye msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Jana Baraza la Michezo Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) kupitia kwa Katibu wake Mkuu, Nicholas Musonye, lilitangaza ratiba ya michuano ya Kombe la Kagame inayotarajiwa kuanza Julai 6 hadi 21, mwaka huu jijini Kigali, Rwanda.

Katika ratiba hiyo itakayorindika kwenye viwanja vitatu; Uwanja wa Kigali, Huye na Umuganda, KMC ya Tanzania ipo Kundi A pamoja TP Mazembe (DR Congo), Atlabara (Sudan Kusini) na wenyeji Rayon Sports ya Rwanda.

Akizungumza na Nipashe juzi kabla ya ratiba hiyo kupangwa, ikiwa ni mara baada ya kusaini mkataba wa mwaka mmoja wa kuinoa KMC, Mayanja alisema atahakikisha anaipa mafanikio makubwa timu hiyo kwenye Ligi Kuu na michuano ya Kagame.

"Nimefurahi kujiunga na KMC, naahidi kuifikisha timu yangu mbali na pia ninaomba ushirikiano kutokana kwa uongozi pamoja na wachezaji," alisema Mayanga huku akiongeza kuwa ana uzoefu mkubwa kutokana na kuzifundisha timu mbalinbali.

## Z'bar kufukuza upepo kesho

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MASHINDANO ya riadha ya kimataifa ya wazi ya Nusu Marathon yanatarajiwa kutimua vumbi kesho visiwani hapa huku yakishirikisha wafukuza 'upepo' zaidi ya 200.

Katika mashindano hayo ambayo yatakuwa na wanariadha kutoka ndani na nje ya nchi yatashirikisha mbio za kilomita 21, kilomita 10 na kilomita tano.

Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Riadha Zanzibar (ZAAA), Muhidini Yasin aliliambia gazeti hili kuwa mbio za kilomita 21 zitaanzia Ngome Kongwe hadi Chukwani na kurudia Chukwani, wakati kilomita 10 zikianzia Ngome Kongwe hadi kwenye mzunguko wa ZRB na kurudia Ngome Kongwe na kilomita tano zitaanzia Ngome Kongwe hadi Fire kurudia Ngome.

Alisema mashindano hayo yatashirikisha jinsi zote na rika tofauti huku yakiwa na lengo la kuhamasisha wanawake kuwa na maamuzi katika mambo yao lakini pia kuibua vibaji.

Alifafanua kuwa kupitia mashindano hayo, ZAAA inatafuta pesa kwa ajili ya kuwasaidia wanawake na kwamba yameandaliwa kwa ushirikiano wa Taasisi ya Upendo na ZIFF.

Michezo
Ijumaa Juni 28, 2019
Nipashe




## Zaha aitaka Arsenal, Auba, Torreira sokoni?

HABARI UK 30

HAMNIWEZI...



Mshambuliaji wa Uganda (The Cranes), Patrick Kaddu, akijaribu kufunga kwa kichwa kwenye mechi ya fainali za Afcon dhidi ya Zimbabwe ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1 juzi. Bao la Uganda lilifungwa na Emmanuel Okwi. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAZIDI KUNOGA

**Upana wa kikosi sasa kupiku cha msimu uliomalizika, yafunguka kushusha majembe zaidi na sababu Kotei kuondoka...**

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI ambao tayari wamesajiliwa na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ni baadhi tu kati ya nyota wa kimataifa wanaotarajiwa kuunda kikosi cha 'Wekundu wa Msimbazi' hao ambao msimu ujao watai-peperusha tena bendera ya Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imeelezwa.

Kuelekea msimu mpya wa 2019/20, tayari Simba imejiimarisha kwa kuinasa saini ya kiungo mkabaji kutoka Al hilal ya Sudan, Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman, beki wa kati mwenye uwezo pia wa kucheza kama kiungo mkabaji, Mbrazil Gerson Fraga Vieira na mshambuliaji kiraka Wilker Henrique da Silva raia wa Brazil pia anayemudu kucheza nafasi zote za ushambuliaji.

Mbali na kusajili wachezaji wapya Simba ipo katika mchakato wa kuwaongezea wachezaji wake mikataba na tayari nahodha John Bocco na msaidizi wake Mohammed Hussein 'Tshabalala' pamoja na kipa Aishi Manula na beki Erasto Nyoni, wamesainishwa mikataba mipya.

Kadhalika, viungo Jonas Mkude, Mzambia Clatous Chama na mshambuliaji Meddie Kagere raia wa Rwanda, wameongezewa mikataba kwa ajili ya kuunda kikosi imara cha mabingwa hao wanaopania kufika mbali zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya msimu huu kuishia robo fainali.

Jana pia, Simba iliutambua umuhimu wa beki kiraka Shomari Kapombe kwa kumsainisha mkataba mpya wa miaka miwili wa kuendelea kuichezea baada ya kuwa nje kwa muda mrefu akiuguza majeraha aliyoyapata akiitumikia timu ya Taifa, Taifa Stars Novemba mwaka jana.

"Beki bora wa kulia nchini Shomari Kapombe amesaini mkataba mpya wa miaka miwili ambao utamwezesha kuendelea kuwa sehemu ya kikosi cha mabingwa. Shomari kwa sasa yupo fiti kucheza na atakuwa sehemu ya kikosi ambacho kitaenda nje ya nchi kujiandaa na msimu mpya," ilisema taarifa ya Simba jana.

Aidha, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alinukuliwa juzi akisema kuwa klabu hiyo inaendelea kujiimarisha na lengo lao ni kuwa na wachezaji bora zaidi ili kuwa na kikosi kipana kitakachoweza kutoa ushindani kwenye michuano ya kimataifa.

Alisema wachezaji wanaowasajili wamezingatia ubora na hawakurupuki kufanya usajili kwa kuwa wanafahamu ugumu wa mashindano yaliyopo mbele yao.

Na alipoulizwa kuhusu sababu ya kumwachia James Kotei kujiunga na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, Magori alisema kiungo huyo mkabaji alimaliza mkataba wake na Simba na juhudi za kumwongeza zilishindikana kutokana na ofa kubwa aliyopewa na klabu hiyo ya Sauzi. "Haikuwezekana, ofa aliyopewa ni kubwa sana, hivyo haikuwa rahisi kuweza kumzuia kujiunga na Kaizer Chiefs, lakini tuna uhakika wachezaji tunaowasajili ni bora zaidi," alisema.

Alisema mashabiki, wapenzi na wanachama wa Simba hawana sababu ya kuwa na wasiwasi kwani usajili wa wachezaji wanaofanya ni bora na wanalenga kuweza kufanya vizuri zaidi katika michuano ya kimataifa.

Msimu uliomalizika Simba ilifika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kabla ya kutolewa na TP Mazembe ya DR Congo kwa jumla ya mabao 4-1.

Msimu huu Simba na Yanga zitapeperusha bendera ya nchi kwenye michuano hiyo wakati Azam FC na KMC zikiwa na kiparua kigumu cha kuhakikisha zinaiwakilisha vema Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

## Okwi, kocha sasa hesabu kwa Misri

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Uganda (The Cranes), Sebastien Desabre, baada ya timu yake kulazimishwa sare ya bao 1-1 na wenzao wa Zimbabwe katika mchezo wa Kundi A wa fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019 uliochezwa juzi usiku jijini hapa, amesema bado wana kazi ngumu.

The Cranes sasa imefikisha pointi nne na iko katika nafasi ya pili kwenye kundi hilo, nyuma ya vinara Misri wenye pointi sita na ambao wameshafuzu hatua ya 16-bora ya mashindano hayo wakati huu wakisubiri kuvaana na Waganda hao Jumapili katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi.

Desabre aliliambia gazeti hili kwamba watacheza kwa kiwango cha juu zaidi katika mchezo wa mwisho dhidi ya wenye Misri ili wapate ushindi na kusonga mbele katika fainali hizi zitakazomalizika Julai 19, mwaka huu.

Kocha huyo raia wa Ufaransa alisema kuwa mechi zote ni ngumu na hali hiyo walitarajia kukutana nayo tangu walipokuwa wanajiandaa na mashindano haya.

"Tuna pointi nne, tunahitaji kufanya vizuri katika mechi yetu ya mwisho ili tutimize malengo yetu, tunaamini tutafanya kile tunachokitarajia, wachezaji wangu wanajua tunachokitafuta," alisema Desabre.

Naye mshambuliaji wa timu hiyo, Emmanuel Okwi, alisema watacheza kwa bidii zaidi katika mchezo wao dhidi ya Misri, ingawa wanafahamu kikosi cha wenyeji hao ni kigumu kufungika.

"Mechi zote ni ngumu, hakuna timu ndogo au timu kubwa, wote tumekuja katika mashindano haya kusaka ushindi, ingawa tunajua mpira una matokeo matatu, tunajipanga kurekebisha tulipokosea ili tusipoteze pointi katika mchezo wetu wa mwisho," Okwi alisema.

Aliwataka mashabiki wao kutoka Uganda kuendelea kuwapa sapoti kwa sababu wanahitaji kuingia uwanjani kuwakabili Misri wakiwa na nguvu zaidi ya walivyokuwa katika michezo iliyopita, na wanahitaji ushindi au sare yoyote ili kusonga mbele.

Mechi nyingine ya Kundi A itakayochezwa Jumapili itakuwa ni kati ya Zimbabwe na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ambayo itakuwa inakamilisha ratiba baada ya kufungwa mechi zote mbili zilizopita.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002